# Nipashe

Jumatano Novemba 23, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581138

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

SUPA JACKPOT TZS.1,053,232,366 KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU! SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mfumo** waandaliwa wanaume kuripoti vitendo vya ukatili

UKURASA 3


Uteuzi Faina ZEC

Wanachama ACT kuamua mustakabali maridhiano

• AFP yaungana kumpinga
• TADEA yasita 'kumfosi' Rais



UKURASA 13



# Kilio mgawo wa umeme kila kona

UKURASA 2



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini (wa pili kushoto), akishuhudia uteketezaji wa silaha haramu 6,208 katika viwanja vya shabaha Kunduchi, Dar es Salaam jana. Kulia ni Kamishna wa Polisi Fedha na Lojistiki, Liberatus Sabas na (kushoto) Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### RAIS ATOA MIL. 70/- KWA WATOTO NJITI



Rais Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. milioni 70 kwa Doris Mollel Foundation (DMF) ikiwa ni kuunga mkono jitihada za taasisi hiyo za kuboresha...

## Waathirika ajali ndege waitwa kupatiwa ushauri madai ya fidia

UKURASA 3

## Sumaye asema 2025 Samia CCM

• **Aahidi** kumpigia debe kila mahali, asisitiza anaupiga mwingi... *Ukurasa 2*

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA

COSOTA

**TAARIFA KWA UMMA**

**ONYO KWA WANAOFANYA UHARAMIA KWA KAZI ZINAZOLINDWA NA SHERIA YA HAKIMILI NA HAKISHIRIKI NA. 7 YA MWAKA 1999**

Ofisi ya Hakimiliki Tanzania inatoa onyo kwa watu wote wanaokiuka Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 kwa kutumia kazi zinazolindwa na sheria hiyo bila kufuata utaratibu na kujiingizia kipato.

Kazi hizo zinazolindwa na Sheria hiyo ni pamoja na Maudhui yote ya Vipindi/Matangazo ya vyombo vya habari yenye mikataba ya hakimiliki, Kazi za Muziki, Filamu ambazo hufanyiwa udurufu bila kibali cha mmiliki pamoja na kazi zote za ubunifu, ambazo zimekuwa zikisambazwa bila kufuata utaratibu wa kuwa na mkataba au kibali cha mmiliki husika na kujiingizia kipato au kuwa na leseni kutoka Ofisi ya Hakimiliki Tanzania huku mmiliki wa kazi akiwa hanufaiki na kazi hiyo.

Hivyo basi, Ofisi inatoa onyo kali kwa watu wote wanaofanya vitendo vinavyovunja sheria husika kuacha mara moja na opereshereni kali itafanyika nchi nzima, iwapo utakamatwa kwa kuvunja sheria hii, hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

Aidha, na kwa Wamiliki wote wa Hoteli, Mabasi, Kumbi za Starehe, Kumbi za Sherehe, Televisheni na Redio wanaotumia kazi za Muziki na Filamu katika biashara zao au maeneo ya wanatakiwa kuhakikisha wanalipia matumizi ya kazi hizo kwani kutolipia matumizi ya kazi hizo ni kosa kisheria.

Kwa mujibu wa sheria hii kutumia kazi yoyote inayolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki na kujiingizia kipato bila kibali cha mmiliki ni kosa la uharamia na adhabu yake ni Kifungo cha Miaka Mitano au Faini isiyopungua Milioni Ishirini au vyote kwa pamoja.

**EPUKA UHARAMIA, ZINGATIA SHERIA**

**Imetolewa na : Ofisi ya Hakimiliki Tanzania**
**17/11/2022**

21760602



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na wananchi wa Wilaya ya Kondoa jana alipokuwa njiani kuelekea wilayani Babati, mkoani Manyara, kwa ajili ya kuanza ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo. **PICHA: IKULU**

# Kilio mgawo wa umeme

**Na Waandishi Wetu**

MAKALI ya mgawo wa umeme yameshika kasi nchini huku maeneo ya vijijini hali ikiwa mbaya zaidi kutokana na watu kukaa zaidi ya wiki moja bila huduma hiyo wala taarifa yoyote ya kuharibika kwa miundombinu kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Aidha, wananchi wa vijijini wamejikuta wakishindwa kuwasiliana na ndugu zao kwa simu na wengine kufanya shughuli za uzalishaji zinazotegemea umeme.

Pia maeneo ya mjini nako mgawo umeshika kasi kwa baadhi ya maeneo unakatika kuanzia alfajiri hadi jioni, huku hakuna taarifa yoyote ya mgawanyo au kuharibika kwa miundombinu.

Wananchi wa kata za Msangeni na Kifula, Mwanga mkoani Kilimanjaro ni miongoni mwa waathirika wakubwa wa kukosekana kwa umeme huku wakisema ni kawaida kukaa siku tatu hadi wiki bila huduma hiyo.

"Hatuelewi ni mgawo au kuna miundombinu imeharibika kwani hatujatangaziwa lakini kila siku wanakata umeme. Wakati mwingine haupo kabisa kwa wiki nzima, hatuwezi kuchaji simu, kuwasiliana na kufanya shughuli za kiuchumi. Ni bora TANESCO watutangazie kuliko mgawo wa kimya kimya wenye maumivu uliopo," alisema mmoja wa wananchi wa Kifula.

Mkazi wa Kijiji cha Balangai, Kata ya Mazinde mkoani Tanga, Oliver Kisaka, alisema umeme unakatika kwa muda mrefu wakati mwingine inakwisha wiki hakuna taarifa yoyote, hali inayowafanya wananchi kushindwa kuchaji hata simu na kuwasha taa.

"Umeme tunatumia kwenye taa, kuchaji simu na shughuli za kuchomelea, mashine kusaga, saluni na viwanda vidogo," alisema.

Diwani wa Mkuzi, wilayani Muheza, George Chambai, alisema: "Kwa wiki hizi mbili tatu unakatika mara kwa mara. Wanasema kuna changamoto ya ukame, chanzo cha Hale maji yamepungua, hivyo wanalazimika kuzima ili yajae. Pia miundombinu ni mibovu kwa kuwa nguzo zinaanguka, jana usiku tunaangalia mpira tukiwa dakika ya sabini umeme ulikatika," alisema.

Flora Shemweta Mkazi wa Kilole, wilayani Korogwe, alisema wamekuwa na mgawo wa saa 12 kwa baadhi ya laini za umeme kwa muda wa mwezi sasa hali inayoathiri biashara yake.

"Kuna baadhi ya laini hazina kabisa mgawo, lakini sisi tunaotumia laini ya Hale, kuna mgawo ambao hata haueleweki, kuna siku unakatika saa sita mchana hadi sita usiku, halafu unakatika tena saa 12:00 asubuhi hadi jioni, kwa wafanyabiashara ni hasara kubwa," alisema.

"Kuna saa nawaona wateja wangu wakinipita na kwenda kununua soda za baridi kwenye maduka ya mtaa wa pili, kwa sababu hawana mgawo wa umeme, sio siri mauzo yameshuka, kwa sasa naweza kuuza soda tatu kwa siku wakati nilikuwa nauza hadi soda 15," alilalamika Flora.

Elizabeth Anthony, mkazi wa Kihonda mkoani Morogoro, alisema wamekuwa na mgawo huo kwa wiki mbili bila kupatiwa taarifa yoyote na TANESCO hali iliyoathiri biashara yake ya barafu.

"Kwa kweli hata sisi hatuelewi huu mgawo unakuwaje maana hatuna taarifa yoyote, tunashangaa tu umeme unakatika saa 6:00 mchana hadi saa 6:00 usiku. Ukipiga simu TANESCO kuuliza hupewi majibu yanayoridhisha," alilalamika.

Salma Athumani Mkazi wa Mwenge, Dar es Salaam, alisema: "Mbona huo mgawo upo tu na ushazoeleka? Kila siku upo tu huku kwetu na hakuna taarifa yoyote wanayotoa watu wa TANESCO. Umeme unakatika kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 6:00 usiku. Leo (jana) umekatika tangu saa 1:00 asubuhi. Yamekuwa maisha yetu ya kawaida", alisema.

Michael Lusonzo Mkazi wa Mbagala, alisema umeme ni wa mgawo umekuwapo kwa njia za umeme zinazotumiwa na watu wengi huku zinazotumiwa na watu wachache zikiepushwa na adha hiyo.

John Mcharo mkazi wa Madale, Dar es Salaam, alisema: "Wamekata umeme tangu saa 10 jioni hadi saa sita usiku, watu wenye biashara wanashindwa kufanya, wanataka kuonyesha Kombe la Dunia ila hawawezi maana hakuna umeme, kama kuna mgawo bora TANESCO iseme kuliko huu ukimya na makali yaliyopo."

Mmoja wa wafanyabiashara hao wa duka la samaki na nyama Kihonda Maghorofani, Sheila Matondo, alisema TANESCO wamekuwa wakikata umeme kuanzia majira ya saa 12.00 asubuhi na kurudisha saa 1:00 usiku bila taarifa yoyote.

Mmiliki wa ofisi inayotoa huduma za viandikia na vifaa vya shule katika kata ya Boma, Salmin Majali, alisema umeme umekuwa ukikatwa pasipo kutolewa taarifa na hawajui kama kuna mgao wa kimya kimya unaendelea na kama upo ni muhimu kuambiwa.

Wafanyabiashara wa mchele katika eneo la Kalumbulu, wilayani Kyela mkoani Mbeya,walelalamikia umeme kukatika kunakowakwamisha kukoboa mpunga.

Zaituni Mwenda alisema analazimika kubaki nyumbani kuendelea na majukumu mengine kutokana na tatizo hilo ambalo limechangia maisha yake kuwa magumu.

Wajasiriamali wa parachichi katika soko la Tandale, Kiwira wilayani Rungwe walisema kukatika kwa umeme mara kwa mara imesababisha kushindwa kufanya shughuli zao nyakati za usiku.

Buponelo Alfredy alisema wanalazimika kutumia vibatari na mishumaa nyakati za usiku ili kuuza bidhaa zao na kwamba matumizi ya nishati hizo ni gharama kubwa hivyo nishati ya umeme ingewasaidia.

**KAULI YA TANESCO**

Jana, TANESCO ilitoa taarifa ya kueleza upungufu wa umeme nchini kwa megawati 155, unaochangiwa na mabwawa ya kufua umeme ya Kihansi, Mtera, Nyumba ya Mungu, Hale na Pangani kupungua uzalishaji.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mtambo wa Kidatu wenye uwezo wa kuzalisha megawati 50 umepata hitilafu na mitambo miwili ya Ubungo yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 40 iko kwenye matengenezo kinga, hivyo kufanya upungufu wa umeme wa maji na gesi kuwa kati ya megawati 245 hadi 300 kutegemea mahitaji ya siku.

Hata hivyo, ilisema hali inatarajiwa kuimarika Desemba, mwaka huu, kwa kurudisha megawati 160 kwenye uzalishaji baada ya mtambo wa Kidatu na Ubungo III kutengemaa na Kinyerezi I kukamilika ufungaji wake.

***• Imeandikwa na Jenifer Gilla (DAR), Ashton Balaigwa (MOROGORO) na Grace Mwakalinga (MBEYA).***

# Sumaye: 2025 ni Samia CCM

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Frederick Sumaye, amempigia chapuo Rais Samia Suluhu Hassan katika kugombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Sumaye amesema pamoja na kumpigia chapuo, ameahidi kumnadi katika maeneo mbalimbali kuhakikisha anachaguliwa kuendelea kuongoza hadi mwaka 2030, huku akibainisha kuwa wananchi wa Manyara watakuwa pamoja naye.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo mstaafu, Rais Samia ana sababu za kuendelea kushika nafasi hiyo kwa sababu anafanya kazi kubwa kwa ajili ya wananchi wa ngazi zote.

Sumaye ambaye alikuwa Waziri Mkuu mwaka 1995 hadi 2005 wakati wa uongozi wa serikali ya awamu ya tatu chini ya Hatari Benjamin Mkapa, aliyasema hayo jana baada ya kukaribishwa kusalimia kwenye ziara ya Rais Samia Suluhu mkoani Manyara, aliposimama kuwasalimu wakazi wa Bonga wilayani Babati.

"Mimi kaka mzee wa mkoa huu na hata jana nilikuwa kwenye kikao cha uchaguzi, ambacho tumemwambia mwenyekiti mpya wa chama ni kuhakikisha chama kinaendelea kuongoza dola.

"Pia nakuhakikishia kwa niaba ya wananchi hapa hiyo bendera tutaendelea kukukabidhi wewe Samia. Tunayasema hayo siyo kwa kukupendelea, tumeona mambo makubwa unayoyafanya," alisema.

Katika ziara hiyo ambayo ilikuwa inarushwa mubashara kupitia mtandao wa Ikulu, Sumaye alisema kwa watu wanaoangalia mambo kwa upeo mkubwa, wanaona mbali kuwa kuna matokeo mazuri ya uongozi wa Rais Samia, ambayo yataonekana miaka ya hivi karibuni.

"Tunakusapoti (tunakuunga mkono) na kukusimamia na si kwa sababu yoyote lakini kwa sababu na wewe unapiga kazi kwa ajili ya Watanzania wa ngazi zote," alisema Sumaye.

Katika ziara hiyo, Rais Samia alizindua mradi wa vihenge na maghala Makatanini, mkoni Manyara.

Waziri wa Kilimo, Husein Bashe, alisema mradi huo umeigharimu serikali Sh. bilioni 19 na kwamba maghala hayo ya kisasa yana uwezo wa kuzuia unyevunyevu, hivyo kuepuka sumukuvu. Maghala hayo ni miongoni mwa miradi mitatu mingine iko Rukwa na Katavi.

Waziri Bashe alisema maghala hayo ya Manyara yana uwezo wa kuhifadhi tani 40,000, hivyo yameongeza uwezo sasa wa kitaifa wa kuhifadhi tani 341,000 lengo lililopo likiwa ni kuhifadhi nafaka tani 500,000.

Rais Samia pia alizindua barabara ya kiwango cha lami ya kilomita nane na kuwahakikishia wakazi wa Babati kuwa watapata tena kilomita zingine tano za lami. Kwa mujibu wa Rais Samia, mji wa Babati unatakiwa kuboreshwa ili kuwawezesha wananchi kufanya biashara na shughuli zingine usiku na mchana.

Awali, Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo, alimshukuru Rais Samia kwa ujenzi wa daraja ambalo lilikuwa kero kwa miaka 50 ambalo limejengwa ndani ya miaka miwili, hivyo kusaidia usafiri kuwa wa uhakika.

Pia alisema kuna ujenzi wa vituo vya afya na madarasa na kuwezesha upatikanaji wa pembejeo na kwamba wakulima wanapokea mbolea za ruzuku bila matatizo .

Mbunge wa Babati Mjini, Pauline Gekul, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, alitumia nafasi hiyo kumshukuru Rais Samia kwa kufanikisha kupatikana kwa mamilioni ya fedha ambazo miongoni mwazo zimepelekwa katika jimbo hilo na kusaidia katika ujenzi wa shule na vituo vya afya.

Gekul pia alisema fedha hizo pia zimesaidia kupatikana kwa huduma ya maji na umeme kwenye maeneo mengi.

## HABARI KITAIFA




Askari wa kikosi cha usalama barabarani, akiangalia ajali ya lori lililoacha barabara na kutumbukia mtaroni baada ya dereva kushindwa kulimudu, jijini Tanga juzi. Hakuna mtu aliyejeruhiwa kwenye ajali hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waathirika ajali ndege waitwa kupatiwa ushauri madai ya fidia

**Na Beatrice Moses**

BARAZA la Ushauri la Watumiaji Huduma ya Usafiri wa Anga (TCAA-CCC), limewataka majeruhi na ndugu wa karibu wa marehemu wa ajali ya ndege ya Precision kufika katika baraza hilo ili kupata ushauri wa kitaalamu wa kudai fidia.

Lengo ni kuwasaidia kufanikisha utaratibu wa kupata malipo wanayostahili.

Katibu Mtendaji wa TCAA-CCC, Innocent Kyara, aliyasema hayo jana, alipozungumza na Nipashe kuhusu tathmini ya awali waliyoifanya ya athari za moja kwa moja kwa watumiaji wa usafiri wa anga, kutokana na ajali ya ndege ya kampuni ya Precision Air iliyotokea Novemba 6, mwaka huu, mkoani Kagera.

Alisema katika tathmini waliyoifanya, walibaini mambo matatu ikiwamo uwapo wa ombwe kuhusu taarifa za utaratibu wa madai ya fidia na kiwango kinachopaswa kulipwa kwa waathirika wa ajali.

"Baraza linaamini uwapo wa ombwe hilo bila kuwapo kwa ufafanuzi kwa mujibu wa sheria kunatoa nafasi ya upotoshaji ambayo madhara yake yanaweza kuwa makubwa yatakayopoteza uaminifu wa watumiaji na umma kwa ujumla katika sekta ya usafiri wa anga," alisema Kyara.

Alisema masuala ya fidia kwa walioathirika kwa ajali ya ndege yanaongozwa na Kanuni ya Usafiri wa Anga ya mwaka 2008 aya 20 na 24 zikisomwa pamoja na mambo mengine zimeweka ukomo wa kiwango cha fidia kisichozidi dola za Kimarekani 120,000 kwa kila aliyeathirika kwa ajali ya ndege.

"Kiwango hili kimekusudiwa kuweka uwajibikaji kwa mashirika ya ndege, hivyo fidia hulipwa na mtoa huduma kulingana na mkataba wa safari, yaani tiketi kwa safari husika. Tunashauri watumiaji pia kukata bima za safari ili kupata ziada ya fidia pindi wanapokumbwa na majanga kama haya," alisema.

Kyara alisema mambo mengine waliyobaini ni kupungua kwa uwezo wa utoaji wa huduma kwa baadhi ya mashirika ya ndege hali ambayo inasababisha baadhi ya safari kuahirishwa au kusitishwa, hivyo kuzua usumbufu kwa wateja.

Jambo lingine, alisema ni uwapo wa vitendo vya uchochezi ambavyo vinatengeneza hofu kwa watumiaji wa usafiri wa anga juu ya usalama wa viwanja na usafiri huo kwa ujumla.

Ajali ya ndege ya Kampuni ya Precision Air yenye namba za usajili 5H-PW aina ya ATR 42-500 iliyokuwa ikifanya safari zake kutoka Dar es Salaam, Mwanza na Bukoba ilianguka katika ziwa Victoria mita 500 kutoka kwenye Uwanja wa Ndege wa Bukoba na ilisababisha vifo vya abiria 19 na majeruhi 24.

# Mfumo waandaliwa wanaume kuripoti ukatili wanaofanyiwa na wenza

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema kutokana na kuwapo kwa matukio ya wanaume kufanyiwa vitendo vya ukatili na wenza wao lakini hawatoi taarifa, imeamua kuweka mifumo saidizi ngazi zote ikiwamo madawati ya jinsia, ili wawe huru kujitokeza badala ya kuendelea kufanya matukio makubwa ndani ya jamii.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa kuelekea siku 16 za maadhimisho ya kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia yatakayofanyika kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10, mwaka huu. Mkutano huo uliandaliwa na WiLDAF kwa kushirikiana na wizara.

Akizungumza na wananchi katika soko la Kigogo Fresh B, Ukonga, jijini Dar es Salaam, alisema wanaume wamekuwa wakifanyiwa ukatili na wenza wao lakini hawapendi kutoa taarifa.

"Mwisho wa kuvumilia wanafanya matukio makubwa ya kikatili katika jamii. Ninawaomba wanaume wote wajitokeze watengeneze mitandao yao ili wawe na sauti moja kama wanawake wanavyofanya na sauti zao zinakuwa kubwa.

"Chama cha Wanaume Wazee kimezinduliwa, Chama cha Wanaume Wanaokatiliwa na Wake zao kipo lakini cha ajabu wanaume wenzake ndio wanaompinga vita mwanzilishi, matokeo yake tunakuwa na wanaume wanaokatiliwa hawasemi wanaona aibu," alisema.

"Ili kuwasaidia tutaweka mifumo saidizi kwenye ngazi zote kwenye madawati ya jinsia yawe pia na wanaume, tutatoa mkeka wa namba ili wanaume wajitokeze wawe huru kusema katika madawati hayo," alisema.

Waziri huyo alisema maadhimisho hayo yataongozwa na wakuu wa mikoa wakishirikiana na wakuu wa wilaya na utekelezaji utafanyika ngazi zote hadi kijiji na mwisho wa kampeni utafanyika ufuatiliaji na kutangaza waliofanya vizuri.

Kuhusu watoto wanaokatiliwa alisema asilimia 60 hufanyika nyumbani na asilimia 40 nje ya nyumba ikiwamo shuleni na utafiti wa mwaka 2021 unaonyesha waliobakwa walikuwa 5,899 na waliolawitiwa ni 1,114 ambapo hesabu hizo zikigawanywa maana yake zaidi ya nusu waliokatiliwa nyumbani.


# CONDOLENCES

The Board of Directors, Management and Employees of TOL Gases Ltd are deeply saddened by the accident that occurred on **6th November 2022** which involved Precision Air flight no **PW-494** enroute to Bukoba from Dar es Salam which claimed the lives of **19** passengers onboard.

We join hands with all Tanzanians and send our condolences to the Government of the United Republic of Tanzania, families and friends of the passengers that have lost their lives or have been injured and to Board of Directors, Management and employees of Precision Air Limited.

**God Bless Tanzania.**

TOL Gases Limited
We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

117159802

# Wahukumiwa kunyongwa kwa kuua

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala ya Mwanza, imewahukumu kunyongwa hadi kufa wafanyabiashara watatu baada ya kukutwa na hatia ya kumuua Philemon Kimaro kwa kumchoma kisu sehemu mbalimbali za mwili kisha kumpora Sh. 80,000 na simu.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji Mwanabaraka Mnyukwa baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote na kujiridhisha pasipo shaka kuwa walihusika na mauaji hayo.

Wafanyabiashara hao ni Daud Mathias kwa jina maarufu Dau, Pastory Malaba maarufu Pasi na Antony Dominic.

Awali, ilidaiwa mahakamani humo kuwa Aprili 21, 2019, Kimaro aliuawa katika eneo la Machinjioni, Nyamagana jijini Mwanza, kwa kukatwa shingoni, kifuani na kwenye mabega.

Kutokana na tukio hilo, wafanyabiashara hao walishukiwa kutenda kosa, wakakamatwa na kufikishwa mahakamani kwa kosa la kuua bila kukusudia, lakini walikana.

Jaji Mnyukwa alisema kwa mujibu wa ushahidi tukio lilianzia kwenye grosari ya Rose, washtakiwa pamoja na Kimaro na mteja mwingine walikuwa wakistarehe.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa walibaini Kimaro alikuwa na Sh. 80,000 pamoja na simu mfukoni mwake na kwamba walimtoa nje kwa nguvu, wakamburuza hadi kwenye kibanda cha Wamasai.

Alisema mshtakiwa wa kwanza alitoa kisu alichokuwa amefieha sehemu za siri na kumchoma kifuani na kuanguka akiwa anavuja damu, wakampora kisha wakaondoka.

Jaji Mnyukwa alisema upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi watatu, vielelezo vitano na ulikuwa unawakilishwa na Wakili wa Serikali, Sabina Choghogwe na Janeth Kihwelo.

Washtakiwa wote watatu walikuwa wakiwakilishwa na mawakili Steven Kaijage, Machere Mkaruka na Constantine Ramadhan.

Katika utetezi wake, mshtakiwa wa kwanza alidai alikamatwa Mei 28, 2019 majira ya mchana, eneo la Igoma alipokwenda kununua kava la simu, alichukuliwa hadi Kituo cha Polisi cha Mwatex, alipelekwa kwenye chumba cha mahojiano na shahidi namba tatu wa Jamhuri, alimwamuru kukaa chini kisha akapewa maelezo atie saini.

Alidai askari mwingine walimpiga rungu na mikanda kwenye kiuno na kwenye makalio huku wakimtishia kumuua iwapo hatasaini maelezo.

Katika utetezi wake alidai alichomwa na kitu aina ya kisu miguuni upande wa kulia karibu na goti, na aliionyesha mahakama hiyo jeraha alilonalo ambalo alipelekwa hospitali akakataliwa.

Jaji alisema mahakama imeona ushahidi wa Jamhuri uliegemea katika ushahidi wa shahidi wa pili bodaboda ambaye alidai alishuhudia kwa macho tukio na katika gwaride la utambuzi, aliwatambua watuhumiwa wawili.

"Mbali na ushahidi huo, upande wa mashtaka uliegemea kwenye maelezo ya onyo ya washtakiwa ambao walikiri kumuua marehemu, katika kuchambua mambo hayo muhimu, mahakama itazingatia ushahidi wa pande zote mbili kabla ya kuamua hatima ya kesi.

"Katika jambo la kwanza la utambuzi, shahidi wa pili ambaye ni shahidi pekee aliyeshuhudia alitoa ushahidi kuwa aliwaona washtakiwa wakimuua marehemu, tukio lilitendeka saa tatu usiku akiwa na abiria wake katika eneo hilo," alisema Jaji.

Alisema ushahidi wa shahidi wa pili unadai katika eneo la tukio kulikuwa na mwanga wa taa na tukio lilikuwa la dakika 20, alimtambua mshtakiwa wa kwanza akidai alikuwa na kovu karibu na jicho, alikiri kuwafahamu mshtakiwa wa kwanza na watatu kwa takribani miaka saba kwa kuwa wote wanafanya kazi zao eneo la Machinjioni.

"Ushahidi lazima upimwe ili kuondoa makosa ya aina yoyote yanayoweza kutokea, katika kesi hii hakuna shaka mauaji yalitokea saa tatu usiku na shahidi wa pili katika ushahidi wake aliwatambua washtakiwa kupitia mwanga wa taa uliokuwa katika kibanda hicho cha ugoro.

"Kuaminika kwa shahidi wa pili ni pale alipoeleza kuwa alitoa taarifa kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi muda mfupi baada ya tukio kutokea, naendelea kuona kuwa ushahidi wake ulikuwa wakuaminika sambamba na kipo chake," alisema.

"Ni wazi kuwa mshtakiwa wa kwanza na watatu walitambuliwa ipasavyo,

pamoja na mambo mengine upande wa mashtaka umeweza kuthibitisha utambuzi wa mshtakiwa wa kwanza na watatu, maelezo ya onyo yameweza kuthibitisha kwamba washtakiwa walikuwa na nia ya kumuua marehemu.

"Washtakiwa walikana mashtaka yao tu bila kutoa ushibitisho wa kuwatoa hatiani, yote yaliyosemwa yanaonesha wazi upande wa Jamhuri umethibitisha mashtaka dhidi ya washtakiwa wote pasina kuacha shaka hivyo mahakama inawatia hatiani washtakiwa wote.

"Kwa kuwa mahakama imewatia hatiani washtakiwa wote, nawahukumu kunyongwa hadi kufa," alisema na kuwaambia wanayohaki ya kukata rufani.



Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Majohe, Dar es Salaam, Tabu Kilonge, akichangia mada kuhusu umuhimu wa jinsia katika uongozi, wakati wa mafunzo yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mabibo, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mikoa mitatu vinara silaha haramu

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sigini, ameliagiza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kuwapo silaha haramu nyingi kwenye mikoa mitatu nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla ya uteketezaji wa silaha 6,208, Sagini alisema serikali iliendesha kampeni ya kukusanya silaha haramu kuanzia Oktoba hadi Novemba, mwaka huu.

Sagini alisema katika kipindi hicho zaidi ya silaha 1,220 zilikusanywa na idadi ya mikoa kwenye mabano ni Tabora (247), Pwani (111) na Tanga (488).

Kwa mujibu wa naibu waziri huyo, serikali ina utaratibu wa kutekeleza silaha haramu kila mwaka zilizowasilishwa kwa hiari na zingine kukamatwa kwenye operesheni mbalimbali ili kupunguza uhalifu.

"Nawapongeza polisi na wadau kwa kukusanya silaha hizo 6,208, kama zisingepatikana zote hizi usumbufu kwa wananchi wenzetu, ikiwamo na sisi wenyewe bila shaka ungekuwa mkubwa sana," alisema.

"Nitoe maelekezo kwa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama, kufuatilia kwa nini mikoa hii mitatu na mingine inayofuatana kwa wingi wa silaha zimekuwa na silaha nyingi na kujua zinatoka wapi na chanzo chake, sambamba na kuandaa mikakati mbalimbali ya udhibiti wake," aliongeza.

Sagini alisema ulinzi na usalama ni muhimu kwa maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla na kwamba bila usalama watu hawawezi kutulia katika shughuli za uzalishaji mali kwa lengo la kujipatia kipato, akieleza kwamba silaha haramu zinachangia kwa kiasi kikubwa katika kuvuruga amani na kuhatarisha kukua kwa uchumi wa taifa.

Aidha, alisema madhara ya kusambaa kwa silaha kuwa ni kuongezeka kwa migogoro, mauaji na makosa mengine yanayogharimu maisha ya watu.

"Leo (jana) tunaposhuhudia uteketezaji wa silaha haramu ni hatua muhimu katika kuhakikisha kwamba raia wanaendelea kustawi kiuchumi bila kuathiriwa na kitu chochote kitakacho wasababisha wakose amani ya kutekeleza majukumu yao ya kijamii," alisema Sagini.

## Jela miaka 30 kwa kumnajisi bintiye miaka 11

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela Idrisa Bayaga (32), dereva wa bodaboda mjini hapo kwa kosa la kumnajisi binti yake mwenye umri wa miaka 11.

Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya Mpanda, Gosper Luoga, alisema mshtakiwa aligundulika ametenda kosa hilo kwa kipindi miezi sita, kati yake miezi minne akiwa ametengana na mama wa kambo aliyekuwa akimlea mtoto huyo.

Kwa mujibu wa maelezo ya hukumu, Bayaga alitengana na mama wa mtoto huyo wakati ana umri wa miaka saba na akaoa mke mwingine akiendelea kumlea mtoto huyo tangu ana umri miaka saba, kisha walitengana Aprili, mwaka huu na baba huyo kubaki na mtoto.

Mapema kabla ya hukumu, mtoto huyo alitoa ushahidi mahakamani, kabla ya mshtakiwa kutakiwa ama kukiri au kukataa.

Hakimu alisema mtuhumiwa alitenda kosa hilo kinyume cha sheria za nchi na alipotakiwa kujitetea alikiri na hata alipopewa nafasi ya kujitetea kabla ya hukumu, alisema hana cha kijitetea.

Baada ya kusomwa hukumu, Nipashe ilimshuhudia Bayaga akiwa chini ya ulinzi wa askari akitokwa machozi. Kabla ya hapo, Bayaga, aliyekuwa katika dhamana, alifika mahakamani akisindikzwa na mdogo wake.

Hukumu ya kesi hiyo iliyochukua saa kadhaa, ilisomwa katika faragha, kutokana na taratibu za kesi ya namna hiyo.

# Washtakiwa mauaji askari waachiwa huru

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Arusha, imewaachia huru washtakiwa 24 waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya mauaji ya askari polisi, Koplo Garlus Mwita, aliyeuawa na watu wasiojulikana wakati wa operesheni ya uwekaji mawe ya mipaka katika Pori Tengefu la Loliondo, wilayani Ngorongoro.

Washtakiwa hao waliachiwa jana baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kuwasilisha barua ya kuonyesha nia ya kutoendelea na kesi hiyo.

Akiwasilisha barua hiyo mahakamani hapo, Wakili wa Serikali, Upendo Shemkole, alidai kuwa DPP hana nia ya kuendelea kuwashitaki washtakiwa hao na kwamba anawasilisha rasmi kusudio la kuomba kuondoa shauri hilo mahakamani hapo, chini ya kifungu 91(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Baada ya ombi hilo, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, Herieth Mhenga, alisema mahakama hiyo imeridhia ombi hilo na kesi hiyo inaondolewa na washitakiwa wote 24 inawaachia huru.

"Mahakama hii imeridhia ombi hilo la DPP na shauri hili kwa mujibu wa mamlaka niliyo nayo naliondoa mahakamani hapa na washtakiwa wote wako huru," alisema Hakimu huyo.

Kati ya washitakiwa hao walioachiwa, 10 ni Madiwani na mmoja ni Mwenyekiti wa zamani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ngorongoro, Nderango Laizer.

Wengine ni Molongo Paschal, Albert Selembo, Lekayoko Parmwati, Sapati Parmwati, Ingoi Olkedenyi Kanjwel, Sangau Morongeti, Morijoi Parmati, Morongeti Meeki, Kambatai Lulu, Moloimet Yohana na Joel Clemes Lessonu.

Wamo pia Simon Orosikiria, Damian Rago Laiza, Mathew Eliakimu, Luka Kursas, Taleng'o Leshoko, Kijoolu Kakeya, Shengena Killel, Kelvin Shaso Nairoti, Wilson Kiling, James Taki, Simon Saitoti na Joseph Lukumay.

Washitakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na makosa mawili likiwamo kula njama ya mauaji.

Katika hati ya mashtaka, ilidaiwa kuwa Washtakiwa hao kwa pamoja walipanga njama ya kuua maofisa wa serikali na maofisa wa Polisi waliokuwa wakishiriki kazi ya uwekaji mipaka katika Pori Tengefu la Loliondo.

Kosa la pili ni mauaji. Kosa ambalo Washtakiwa hao kwa pamoja walikuwa wakidaiwa kuwa Juni 10, 2022 eneo la Ololosokwan katika wilaya ya Ngorongoro, kwa nia ovu walisababisha kifo cha askari mwenye namba G 4200, Koplo Garlus Mwita.



Vifusi vya udongo vikiwa vimerundikwa katika barabara eneo la Saku Chamazi, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni maandalizi ya uboreshaji wa barabara za eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Rais atoa mil. 70/- kusaidia watoto njiti

**Na Frank Monyo**

RAIS Samia Suluhu Hassan (pichani chini) ametoa Sh. milioni 70 kwa Doris Mollel Foundation (DMF) ikiwa ni kuunga mkono jitihada za taasisi hiyo za kuboresha huduma za watoto njiti nchini.

Fedha hizo zilitolewa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto Njiti Duniani yaliyohitimishwa Novemba 20,2022 katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti mkoani Mara.

Kati ya fedha hizo alizozitoa katika mshahara wake, Sh. milioni 20 ni taslimu kwa ajili ya shughuli za kuwasaidia watoto njiti na Sh. milioni 50 kwa ajili ya vifaa tiba vya kuwasaidia watoto hao.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo yaliyofanyika Kijiji cha Robanda, Serengeti mkoani Mara, Mkurugenzi Mtendaji wa DMF, Doris Mollel, ambaye pia alizaliwa akiwa njiti, alisema anamshukuru Rais Samia kwa msaada huo. Alisema vifaa hivyo vitagawiwa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini.

"Nilipigiwa simu kutoka Ikulu nikaambiwa Doris Mollel, tumeona kazi kubwa unayoifanya kwa ajili ya watoto njiti, na tumeona pia ukihamasisha watu kuwa tayari kuangalia maadhimisho ya mtoto njiti ya mwaka huu kufanyika hifadhini (Serengeti) na kurusha ujumbe wa watoto njiti duniani kukiwa na watalii kutoka mataifa mbalimbali mbugani," alisema.



"Nashukuru sana kwa msaada huu kutoka kwa Rais kwani ameutoa siku mwafaka na tayari tumepanga hiyo Sh. milioni 20 tunakwenda kujenga chumba maalum cha mfano kwa ajili ya watoto njiti katika Hospitali ya Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza kikiwa ni zawadi kwa Rais na kumbukumbu kwa kile alichofanya kwani amenitia moyo sana," aliongeza.

Alisema katika maadhimisho ya mwaka huu, DMF kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imetoa msaada wa Sh. milioni 230 ambao utaboresha mazingira ya utoaji wa huduma kwa watoto hao nchini.

Mbali na kununua vifaa tiba, Mollel alisema taasisi hiyo imepanga kusimika mitambo ya kufua hewa ya oksijeni katika hospitali za wilaya za Siha, Monduli na Karatu pamoja na Kituo cha Afya cha Dabadi wilayani Karatu.

Alisema watoto njiti wanakabiliwa na changamoto nyingi na kwamba zinahitajika jitihada za makusudi na ushirikiano kutoka kwa wadau mbalimbali kuunga mkono jitihada za serikali ili kunusuru maisha ya watoto hao ambayo yapo hatarini kutokana na namna wanavyozaliwa.

Alikumbusha kuwa kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (ILO), asilimia 41 ya vifo vya watoto wachanga duniani vinatokana na watoto njiti na kusisitiza kuwa hali hiyo haiwezi kuachwa kama ilivyo kwa kuwa watoto hao wana haki sawa na watoto wengine.

"Watoto hawa wana uwezo wa kuishi maisha marefu kama walivyo watoto wengine endapo tutaboresha mazingira ili wazaliwe katika mazingira sahihi," alisema.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema serikali imetenga bajeti ya Sh. bilioni 23 kwa ajili ya kujenga vituo 100 vya kuhudumia watoto kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Dk. Mollel alisema fedha hizo alizotoa Rais Samia kwa taasisi hiyo zinatoka kwenye mshahara wake na alimshukuru kwa kuchangia. Alizitaka taasisi mbalimbali zinazotoa huduma katika jamii kuiga mfano wa taasisi hiyo ambayo katika kipindi cha miaka minane imekuwa ikifanyakazi ambayo imekuwa na matokeo chanya.

"Hadi kufikia hatua Rais ametoa fedha zake binafsi Sh. milioni 20 pamoja na vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 50 kwa taasisi hii ina maana kazi inaonekana. Nikupongeze mkurugenzi kwa kazi nzuri unayofanya kwani unaisaidia serikali lakini pia wengine waige mfano huu tunataka matokeo na si blabla," alisema.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara, Dk. Juma Mfanga, alisema mkoa huo una mahitaji makubwa ya vituo vya kutolea huduma kwa watoto njiti kutokana na vituo vilivyopo kutokidhi mahitaji.

Alisema mkoa huo una vituo 335 vya kutolea huduma ya afya ambapo kati ya hivyo ni vituo 13 pekee ndivyo vinatoa huduma ya mtoto njiti.

"Tuna vituo 335 vya kutolea huduma ya afya na kati ya hivyo, vituo 290 vinatoa huduma ya mama na mtoto na kati ya hivyo ni vituo 13 tu vinatoa huduma ya mtoto njiti kwahiyo mahitaji ni makubwa," alisema Dk. Mfanga.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuhuma za rushwa uchaguzi zinaharibu taswira ya CCM

**CHAMA** Cha Mapinduzi (CCM) kupitia kwa Katibu Mkuu wake, Daniel Chongolo, kilitangaza kufuta uchaguzi wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Simiyu, kusimamisha uchaguzi wa Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC) huku kikieleza kuwa kinachunguza uchaguzi wa mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Aidha, katika video iliyosambaa, walionekana vijana wanaodaiwa kuwa ni makada wa CCM wakiwa kwenye gari dogo eneo la Itilima, mkoani Simiyu wakigawana fedha, huku Mjini Magharibi kukiwa na tuhuma za kada mmoja kubeba sanduku la kura na kwenda nalo kwenye chumba cha kuhesabia.

Tayari Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imesema inafuatilia kwa karibu ili ichukue hatua madhubuti bila kujali jina au ukubwa wa mtu husika huku ikiwatahadharisha wajumbe kuacha kujihusisha na vitendo hivyo.

CCM ina ahadi 10 za mwanachama ikiwamo ile rushwa ni adui wa haki, sitatoa wala kupokea rushwa. Zingine ni pamoja na binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja; Nitaitumikia nchi yangu na watu wake; nitajitolea nafsi yangu kuondoa umaskini, ujinga, magonjwa na dhuluma.

Malalamiko ya rushwa ndani ya chama hicho kikongwe na tawala nchini hayajaanza leo wala jana. Kila kunapokuwa na uchaguzi wa ndani na nje, kwa maana ule wa kuomba idhini ya uongozi wa nchi au serikali za mitaa, yanajitokeza huku wale wenye uwezo na nguvu za kifedha na madaraka wakidaiwa kuwa ndio vinara wa rushwa.

Kwa sasa inazidi kujulikana kutokana na kukua kwa teknolojia ndiyo maana kuna mtu alirekodi video fupi ikionyesha vijana hao (Simiyu) ambao ni wapigakura wakichukua fedha ili wamchague mtu fulani.

Kuanzia ngazi ya matawi wanaogombea nafasi hupita kwa wajumbe kutoa fedha ili wachaguliwe. Jina linaporudi, wale wanaofanikiwa kupenye katika mchujo nao hutoa fedha ili wachaguliwe. Suala hilo pia liko katika ngazi za kata, wilaya, mkoa na kwenye jumuiya, kote kukiwa na viwango tofauti ambavyo ukiwaulizia wajumbe wanasema bila kuogopa. Baadhi ya wajumbe husema huo ndio wakati wao wa mavuno.


Hali hiyo huendelea hadi kwenye ngazi ya taifa ya CCM na hata wakati wa uchaguzi mkuu ambao mchakato wake huanzia ndani ya chama. Ili mtu apitishwe kugombea udiwani kwenye kata au viti maalum na ubunge wa jimbo, lazima awe amejipanga vyema kutoa fedha. Hapo ndipo ule msemo mkono mtupu haulambwi husadifu.

Uchaguzi wa sasa, rushwa imekuwa nje nje bila woga huku TAKUKURU ikiwapo, wanachama hao hao wanasigina ahadi ya kupambana na rushwa, hivyo suala hilo kubaki tu kwenye maandishi.

Hali inavyoendelea maana yake asiyekuwa na uwezo wa kifedha hatakuwa kiongozi wa kugombea kwa nafasi yoyote ile. Kwa mantiki hiyo, ni lazima CCM ikemee na ichukue hatua madhubuti vinginevyo hali itazidi kuwa mbaya maradufu. Hali hiyo itakapokomaa, itaendelea hata ndani ya serikali kwa watu wenye nguvu ya fedha kuzitumia kunyonya haki za wengine.

Ni muhimu pia TAKUKURU ikafanya kazi bila woga, tuone ikishughulikia mapapa na kuacha kuhangaika na vidagaa ili kulinda heshima yake kwenye jamii. Kama rushwa itaachwa ishike hatamu, itafika wakati na kuonekana ni jambo la kawaida na kwamba bila kutoa rushwa hakuna kupata nafasi au huduma fulani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# CCM ukipanda rushwa utaivuna rushwa zaidi

**CCM** imefuta uchaguzi wa ndani unaoendelea kwenye baadhi ya mikoa kutokana na kuwapo kwa tuhuma za rushwa, ambazo sasa chama kinataka kichunguze ili kujiridhisha na kuchukua hatua.

Licha ya viongozi wa juu wa chama kuonya tangu awali kuhusu kuwapo tuhuma za rushwa inaonekana wapo baadhi ya makada ambao wamekuwa wagumu kuelewa, badala yake wanaendelea na mchezo huo unaokwenda kinyume na maadili na ahadi namba nne ya mwanachama wa CCM.

Katika ahadi hiyo wanakiri kuwa rushwa ni adui wa haki, hawatapokea wala kutoa rushwa wakiwahimizwa kutojihusisha kwa namna yoyote na masuala ya kutoa au kupokea mlungula kwa kuwa ni kinyume cha haki.

Rushwa ni hatia, inakuwa anayezaliwa na hatia awe mwenye uadilifu? Wana CCM wasisahau kuwa daima unavuna ulichopanda, ukipanda kiongozi zao la rushwa unavuna uongozi uliojaa rushwa, usio na uadilifu, wenye ufisadi na ubadhirifu kwani ndicho kilichopandwa.

Kitendo hicho kimesababisha CCM kufuta uchaguzi wa Umoja wa Vijana (UVCCM) mkoa wa Simiyu na kusimamisha uchaguzi kwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC) katika mikoa ya Mbeya na Arusha.

Sasa chama kimetuma timu yake ya kufanya uchunguzi, baada ya kukamilisha itaikabidhi, hatua zitachukuliwa kwa watakaobainika kujihusisha na rushwa, ikiwamo kuwaondoa kabisa katika uchaguzi na kuwakabidhi kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Ninadhani kauli za viongozi wa juu wa chama hicho, akiwamo Katibu Mkuu Daniel Changolo, hasa kiuhusu vita dhidi ya rushwa, ingetosha kuwafanya makada kurudi kwenye mstari ili wachaguliwe kwa njia ya haki.

Lakini huku wakitambua kuwa rushwa ni adui wa haki, baadhi yao wameendelea kuifanya kama sehemu yao ya maisha, kwani hadi viongozi wa chama kusimamisha uchaguzi, ni wazi wamenusa harufu ya rushwa.

Hatua ya chama kutuma maofisa na viongozi kuwa wasimamizi wa uchaguzi kila mkoa na nyingine ambazo zinachukuliwa, vinatosha kuwashtua wanachama kutambua chama kimedhamiria kupambana na rushwa.

Bahati mbaya inaonekana wapo wengine ambao hawajaelewa, wanaendelea kutafuta nafasi ya uongozi kwa kutumia njia hiyo ambayo inawanyima wengine haki ya kuchaguliwa kwa sababu tu hawana fedha.

Pamoja na hayo, suala la mapambano dhidi ya rushwa linahitaji utashi wa kisiasa 'political will' wadau wote kuanzia wanasiasa, wakiwamo wabunge na madiwani kuikemea kwa nguvu zote.

Utashi wa kisiasa pamoja na uwazi katika utoaji huduma ni mambo muhimu yanayohitajika, hivyo badala ya mtu kuwapa wanachama fedha ili wamchugue awaongoze, uwezo wake wa kuongoza uwe ndio kigezo cha kuchaguliwa.

Ninaamini hatua zinazoendelea kuchukuliwa na viongozi wa chama, kuna wakati wale wanaotumia rushwa kutafuta uongozi, wataachana na mtindo huo ambao unawanyima nafasi ya kuongoza watu wenye nia njema.

Lakini ingependeza kama wanachama watakuwa na msimamo wa kuwakataa wote wanaotumia rushwa kupata uongozi, ingawa imekuwa ikidaiwa wao ndio hushawishi wagombea kutoa fedha ili wawachague.

Kwenye suala la rushwa, ni vyema wakatambua kuwa mtoa rushwa na mpokea rushwa, kapu lao ni moja, hivyo wanaweza kujikuta wamenaswa kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Vita dhidi ya rushwa inayoendelea ndani ya CCM ni mwendelezo ambao umekuwapo muda mrefu tangu awamu zote zilizotangulia, kwani aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM wakati wa awamu ya tano Rais John Magufuli, naye aliivalia njunga.

Katika uongozi wake hakusita kutengua matokeo ya uchaguzi pale alipobaini rushwa imetumika na alisisitiza kuwa amedhamiria kupambana nayo kama ambavyo uongozi wa sasa unaendelea na vita hiyo. Hivyo ingependeza kama wale wanaotumia rushwa kupata uongozi, wakaachana na mtindo huo kwani huwezi kupata kitu bora ndani ya kibovu.

HABARI KITAIFA

# Balozi Shimbo apongeza bima afya kwa wote

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

BALOZI Luteni Jenerali Mstaafu Abdulrahman Shimbo amesema mpango wa serikali wa kuwekeza kwenye sekta ya afya kwa kuanzisha bima ya afya kwa wote, utasaidia kuokoa Watanzania wengi kutokana na umuhimu wake kwenye maisha ya watu.

Alisema hayo jana wakati akizungumza katika uzinduzi wa hospitali ya kisasa ya Platinum Medical Care iliyoko Msamvu, Manispaa ya Morogoro.

Jenerali Shimbo ambaye aliwahi kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), alisema afya ni gharama na watu wachache wanaweza kumudu kikamilifu hivyo mpango huo ni muhimu sana.

"Mpango wa serikali wa kuanzisha bima ya afya kwa wote ni jambo muhimu sana kwani utatatua changamoto ya serikali ya kupambana na yale mambo makubwa matatu yaani ujinga, umaskini na maradhi. Bima ya afya inaangukia kwenye maradhi alisema.

Pia alitumia muda huo kuwashauri Watanzania kutumia fursa hiyo wajiunge kwenye bima ya afya kwa wote kwa kuwa itawasaidia kupambana na maradhi.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Meneja wa Hospitali hiyo, Rim Ngole, alipongeza hatua ya serikali kwa kuwajali wananchi wake na kupeleka muswada bungeni kuhusu bima ya afya kwa wote ambayo itawasaidia wananchi kuwa na uhakika wa matibabu wakati wowote wanapokumbwa na maradhi.

"Kwa nafasi hii naipongeza kwa dhati serikali kwa kuwajali wananchi wake , na kupeleka muswada bungeni na tunaomba muswada huu ujadiliwe vizuri na upitishwe, kwani utawasaidia sana wananchi kuwa na uhakika wa matibabu," alisema Ngole.

Akielezea hospitali hiyo, Ngole alisema huduma zao zinapatikana kwa gharama nafuu zinazowawezesha wananchi wa kipato cha chini kuzimudu pia kutoa huduma kwa wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ambao umekuwa msaada kubwa kwa wananchi.

Ngole alisema hospitali hiyo imeanza kutoa huduma chache za msingi kwa wananchi na kimepanua wigo kwa kuimarisha idara ya dharula kwa kuongeza vifaa zaidi vya kisasa vya kuokoa maisha.

Naye Mkurugenzi wa Kituo hicho, Yusuph Amiri, licha ya kuipongeza serikali pia aliishukuru Benki ya CRDB kwa kuwaamini na kuwapa mkopo kupitia CRDB Albarakah Bank usiokuwa na riba na kuwezesha uwekezaji katika sekta ya huduma za afya.




Mtoa huduma wa Vodacom M-Pesa, Filbert Mushi (kushoto), akiwapa maelezo wateja waliotembelea banda la kampuni hiyo, katika maonyesho ya wiki ya huduma za fedha kitaifa yanayoendelea jijini Mwanza jana. Vodacom Tanzania imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha inasukuma ajenda ya kulipeleka taifa katika ulimwengu wa kidijitali kwa kurahisisha huduma za malipo kupitia simu ya mkononi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EU yaipa Tanzania bil. 34/- umeme vijijini

**Na Beatrice Shayo**

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA), umetia saini mkataba wa Sh. Bilioni 34 na Umoja wa Ulaya (EU) wa Sh. bilioni 34 kwa ajili ya mradi wa kupeleka umeme vijijini katika vituo vya afya na visima vya maji, ili kupunguza maambukizi ya magonjwa ya milipuko ikiwamo UVIKO-19.

Mradi huo utanufaisha hospitali sita, vituo vya afya 57 na miradi ya maji 363 ambayo itaunganishwa kupata huduma ya nishati ya umeme katika mikoa 25 ya nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam baada ya kutia saini mkataba huo, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Hassan Said, alisema kazi hiyo itafanywa na makandarasi wazawa watatu kusambaza umeme katika vituo vya afya na vituo vya maji.

Alisema mradi huo ni mpango maalumu ambao ulilenga kusaidia jitihada za serikali kuzuia magonjwa ya maambukizi ikiwamo UVIKO-19 na mengine.

"Ni mradi wenye malengo maalum ndio maana umeenda katika vituo vya afya kwa ajili ya kuboresha huduma katika maeneo ambayo chanjo ilikuwa inashindikana kuhifadhiwa kutokana na kukosekana kwa nishati ya umeme.

"Njia ya kupambana na maambukizi ni kusafisha mikono na maji tiririka ndio maana tukalenga katika miradi ya maji ili wananchi wapate huduma hiyo kwa wakati," alisema Saidy.

Aidha, Saidy alisema utekelezaji wa mradi huo ni miezi tisa na hapatakuwa na ongezeko la muda wafanye kazi ndani ya muda au wamalize kabla ya muda uliopangwa.

"Kabla ya kusaini mjue kabisa hatutaongeza muda katika mkataba msije kutuletea vifaa vya kupasuka tunataka vifaa vyenye ubora na tufuate 'standard' (viwango) za TANESCO za miundombinu. Kama unazani hauwezi kwenda kuutekeleza huu mradi ndani ya muda wa mkataba naomba usijishughulishe kusaini nisije kusikia sijui hakuna nguzo sijui kuna vita imetokea sitaki kusikia dharura yoyote," alisema Saidy.

Alisema REA itatimiza wajibu wake ikiwamo kuwalipa kwa wakati, ili kazi hiyo imalizike kwa wakati na wananchi wapate huduma kwa wakati.

Kamishna wa Umeme wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Stydem Rwebangira, alisema katika ugonjwa wa UVIKO-19 kampeni kubwa ni kunawa na maji tiririka wakibaini kumekuwa na changamoto ya baadhi ya maeneo mengi ambayo yana shida ya vyanzo vya maji katika miradi ya maji.


Alisema hata katika uhifadhi wa chanjo zilikuwa na changamoto licha ya kuwepo kwa miradi ya umeme vijijini, hivyo EU umewaongezea fedha hizo kuhakikisha maji tiririka yanapatikana na kuhifadhi chanjo za UVIKO-19.

Meneja Miradi wa EU, Francis Songela, alisema utekelezaji wa mradi huo ni sehemu ya mchango wao katika sekta ya nishati, ikiwemo kupeleka umeme vijijini.

Alisema kuna miradi mingine tayari wamewekeza na inaendelea na walivyoona ugonjwa wa UVIKO-19 wakaona waongeze fedha katika mradi huo walioingia makubaliano na makandarasi kupeleka umeme kwenye vijiji ambavyo havina umeme, vituo vya afya na visima vya maji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya O.K Electrical and Eletronics Services Ltd, Mrisho Masoud, alisema watafanyakazi kwa ubora unaotakiwa.

## KABWELA



# Matumizi holela dawa chanzo usugu magonjwa

**Na Mary Geofrey**

MATUMIZI ya dawa bila ushauri wa daktari na kukatisha dozi vimetajwa kuwa sababu zinazochochea ongezeko la tatizo la usugu wa vimelea dhidi ya dawa za Antibayotiki kwa binadamu kwa asilimia 59.8 nchini.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua kongamano la kisayansi na usugu wa vimelea dhidi ya dawa za Antibayotiki, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

"Usugu wa vimelea dhidi ya dawa duniani unaongezeka kwa sababu nyingi ikiwamo kutotumia dawa kwa usahihi, mfano unatakiwa kutumia dawa kwa siku tano, ukitumia siku mbili ukasikia unafuu unaacha, vimelea vinakuwa havijaisha mwilini na vilivyobaki vinaendelea kujenga usugu," alisema.

"Hapa niwasihi wananchi, kutumia huduma za hospitali kupima na kugundua ugonjwa ili kupatiwa tiba sahihi. Natoa rai pia kwa madaktari kutumia vipimo sahihi vya maabara kutoa matibabu sahihi kwa wagonjwa," aliongeza.

Pia alisema kuna usugu wa matumizi ya dawa kiholela kwa wanyama ambayo madhara yake ni vimelea vya dawa kubaki kwenye mazao ya wanyama kama mayai, maziwa na nyama.

Aliwataka wafugaji kutumia chanjo zaidi badala ya kutumia dawa za Antibayotiki kutibu mifugo na kusababisha kuhamishia vimelea kwa watumiaji wa mazao ya wanyama.

Pia alitaja madhara makubwa ya kukithiri kwa vimelea dhidi ya dawa ni kukwepa dawa au kutotibika kwa urahisi pindi mgonjwa anapotumia dozi.

Sambamba na hayo, alisema Watanzania wanapaswa kuboresha mazingira yanayowazunguka na kuzingatia usafi wa mwili ili kudhibiti kupata magonjwa ya vimelea yanayosababisha matumizi ya dawa za Antibayotiki.

Mganga Mkuu wa Wanyama nchini, Prof. Herson Nonga, alisema kwa kipindi cha mwaka uliopita wa fedha dozi za chanjo milioni 700 zilitumika kwa mifugo nchini huku dawa zilizotumiwa ni asilimia 10 ya chanjo.

Alisema zipo dawa ambazo mfugaji anaweza kununua mwenyewe dukani na kuzitumia na zile ambazo lazima daktari wa mifugo ampime mnyama na kumpa tiba.

"Dawa inayotumika kutibu mifugo ni asilimia 10 tu ya dozi ambazo wanapewa wanyama. Serikali inasisitiza matumizi ya chanjo badala ya dawa pamoja na kuzingatia ufugaji bora kwa ajili ya usalama wa afya zetu na uchumi kwa ujumla," alisema Prof. Nonga.

Mwakilishi na Mfamasia wa Shirika la Afya Duniani (WHO) nchini, Rose Shija, alisema mwaka 2019 vifo milioni 4.95 duniani vilihusishwa na maambukizi ya bakteria wenye usugu dhidi ya dawa, huku vifo milioni 1.27 vikihusishwa moja kwa moja na vimelea sugu vya dawa za Antibayoti.

"WHO imetangaza kuwa vimelea vya matumizi ya dawa za antibayotiki ni mojawapo ya matishio 10 ya afya ya umma vinavyowakabili binadamu," alisisitiza.



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Malembo Farm, Malembo Lucas (kushoto), akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya JSH Farm Ltd, Husna Saidy, wakati wa utoaji wa tuzo kwa wakurugenzi vijana wa umri wa miaka 30, barani Afrika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ataka viongozi wa dini kukemea ukatili

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

VIONGOZI wa dini nchini wana jukumu la kusaidia jamii ili kuondoa matukio ya mauaji na ukatili yanayojitokeza kila siku kwenye maeneo mbambali, imeelezwa.

Mwenyekiti Mwenza wa Baraza la Viongozi wa Dini nchini, Shehe Khamis Mataka, alisema hayo jana wakati wa mkutano wa kitaifa uliowashirikisha viongozi wa dini na wanasiasa uliofanyika jijini hapa.

Shehe Mataka alisema viongozi wa dini wana nafasi kubwa ya kusaidia jamii katika kukemea vitendo vya ukatili ili kuondoa mauaji yanayoendelea kutokea.

Pia alisema viongozi hao wana kundi kubwa la watu wanaowasikiliza katika nyumba zao za ibada hivyo wajitahidi kukemea vitendo hivyo ambavyo vinatokea kila siku.

Aliyataja matukio ambayo yanajitokeza kila siku kwenye jamii kuwa ni mauaji ya kikatili ya wanandoa ,watoto kuwaua wazazi wao au wazazi kuwaua watoto.

Matukio mengine ni ubakaji wa watoto wadogo ambayo yamekuwa yakiripotiwa kila siku kwenye vyombo vya habari na Jeshi la Polisi na mengi yanafanywa na watu wa karibu wa familia husika pamoja na makundi ya vijana wanaojihusisha na kupora mali za watu.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, alisema mkutano huo una mada nzuri muhimu ambayo imekuja wakati mwafaka kwa sababu inahusu utu wa watanzania.

Alisema kwa sasa wameanza kuona vitendo vya kuharibikiwa kwa misingi ya utu ambayo ipo kwenye vitabu vya dini.

Aliitaja Mifano ya kuharibikiwa kwa misingi ya utu ni matusi, ulawiti, wizi, mauaji na akaonya vitendo hivyo si dalili njema

# Waziri aagiza kuanza kampeni kutunza mazingira

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, ameagiza kila mkoa kuanzisha kampeni maalumu ya kutengeneza mazingira ya ukijani kwa kuweka mikakati madhubuti ya kurejesha uoto wa asili.

Masanja alisema tayari kampeni hiyo inafanyika katika mkoa wa Dodoma kwa kujulikana kama 'Dodoma ya kijani' na kwamba imefika wakati ianze kufanyika katika mikoa yote nchini.

Masanja alitoa kauli hiyo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizindua warsha ya urejeshaji wa uoto wa asili iliyowakutanisha wadau kutoka katika sekta mbalimbali, ndani na nje ya Tanzania.

Kufikia mwaka 2030 Tanzania inatakiwa iwe imerejesha uoto wa asili milioni 5.2 na kwamba ili kufikia huko, kuna haja ya kila mkoa kuanzisha kampeni hiyo ya kuwa na kijani yake ambayo itatokana na kuweka mikakati madhubuti ya kutunza mazingira na kurejesha uoto wa asili.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi 54 zilizoingia kwenye mkataba wa urejeshaji wa uoto wa asili ambao kati ya hizo, tayari nchi 32 zimesaini mkataba na kuingia katika utekelezaji wa uoto huo," alisema Masanja.

"Malengo ya dunia ni kuhakikisha kwamba jumla ya hekta milioni 350 zinarudi kwenye uoto wa asili, kwa Afrika tuna malengo ya jumla ya hekta milioni 100 ambazo zinatakiwa kurejeshwa kwenye uoto wa asili. Tanzania tumejiwekea malengo ya kurejesha uoto huo wa asili kwa hekta milioni 5.2 mpaka kufikia mwaka 2030."

"Kwa hiyo serikali katika kufanikisha lengo hilo, iliamua kuhusisha wadau mbalimbali ikiwamo kutoa elimu ili waingia kenye mpango huo. Na baada ya kuingia tulibaini kwamba kuna maeneo ambayo tayari yamekwisha kuvamiwa na wananchi ambayo kiukweli yalistahili kuhifadhiwa vizuri."

Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, alisema katika kufanikisha hilo la kurejesha uoto wa asili wanahakikisha kwamba maeneo ambayo yana mito na uoto wa misitu hayaharibiwi.

"Na hata yale ambayo yameharibika kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu, iwe ni uvamizi kwa ajili ya makazi, shughuli za uvunaji wa nishati ya mkaa na nyinginezo, kuhakikisha yanarejesha uoto wake wa asili kwa kupanda miti katika maeneo yote ambayo yameharibika na hata katika maeneo mengine ambayo hayajaharibiwa ili kutoa mbadala wa mazao ya misitu katika maeneo hayo," alisema Prof. Silayo.

"Katika kufanikisha hili, wadau mbalimbali wanatakiwa kushiriki ikiwamo wananchi, serikali, mashirika na asasi za kiraia. Na mkakati huu unalenga siyo kuboresha mazingira yaliyoathirika, lakini kuhakikisha kwamba jamii zinazoishi katika maeneo mbalimbali zinanyanyuliwa kiuchumi."

HABARI KITAIFA

# Tril. 1/- kuboresha bonde Msimbazi

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya Dunia imeipatia serikali mkopo wa bei nafuu wa Sh. trilioni 1.24 kwa ajili ya mradi wa uendelezaji wa bonde la Msimbazi na kusambaza umeme vijijini.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, muda mfupi baada ya kutiliana saini, makubaliano hayo na Benki ya Dunia, alisema fedha hizo zitasaidia nchi kupiga hatua kubwa kiuchumi.

Alisema Dola za Marekani milioni 200 zitatumika katika kuboresha eneo la Jangwani kwa kujenga daraja na kuboresha miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam.

Alisema kwa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, wamefanikiwa kufanya majadiliano ya haraka na wadau wa maendeleo kwa ajili ya kusaini mikataba na kutekeleza miradi ya maendeleo.

**TAMISEMI tutatoa ushirikiano wote na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ujio wa miradi, kutoa ushirikiano na kuitunza lakini pia kuhakikisha inawanufaisha.**

Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema takribani Sh. bilioni 700 zitatumika kuunganisha umeme vijijini, kupanua gridi ya Taifa, na kufanya maandalizi ya matumizi ya nishati jadilifu.

"Wizara ya Nishati imefurahi kwa sababu sehemu kubwa ya fedha zitatumika kusambaza umeme vijijini, kwenye vitongoji na kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya umeme kwa sababu kwa sasa ni asilimia 24 tu wenye huduma hiyo," alisema Makamba.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Grace Maghembe, alisema miradi hiyo inagusa maeneo ya miji na vijijini.

Alisema miradi hiyo ina lenga kuwagusa wananchi katika kutatua changamoto za bonde la Msimbazi na kusambaza umeme katika vijiji ambavyo havijafikiwa na huduma hiyo.

"TAMISEMI tutatoa ushirikiano wote na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ujio wa miradi, kutoa ushirikiano na kuitunza lakini pia kuhakikisha inawanufaisha," alisema.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Rogatus Mativila, alisema wamepata zaidi ya bilioni 145 kupitia mradi huo, kwa ajili ya kujenga daraja la juu kuzuia mafuriko na wataanza baada ya kupatikana kwa mkandarasi kuanzia mwezi wa nne 2023.

Alisema TANROADS itajenga daraja hilo kwa miaka miwili hadi mitatu lenye urefu wa mita 390 na litanyanyuka juu kwa mita sita na kusaidia kutofikiwa tena na mafuriko ya maji.

Alisema TAMISEMI wataboresha kwenye mto kwa urefu kwa kilometa 1.8 kwenda juu na wanatarajia kuanza utekelezaji baada ya kutangaza tenda na kumpata mkandarasi.

Kaimu Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia, Preeti Arora, alisema wametoa fedha hizo kwa ajili ya kusogeza huduma muhimu za maendeleo ya Taifa yanayowagusa wananchi moja kwa moja.

## Mchengerwa ashinda ujumbe wa NEC Pwani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa amechaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) kuwakilisha mkoa wa Pwani baada ya kupata kura 792 kati ya 828.

Akitangaza matokeo hayo jana katika uchaguzi wa CCM mkoa wa Pwani uliofanyikia Kibaha, Msimamizi wa Uchaguzi, Zainab Telack, alisema kati ya kura 834 zilizopigwa sita ziliharibika na halali zilikuwa 828.

Alisema Mchengerwa alipata kura 792 akiwashinda wagombea wengine wanne akiwamo Mohamed Musa (5) na Abihud Shila (2).

Katika nafasi ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa huo aliyekuwa Mwenyekiti wa Klabu ya Mpira wa Miguu Young African, Imani Madega, ameshindwa kutamba kwenye uchaguzi huo baada ya kupata kura 61 kati ya 841 zilizopigwa kwenye awamu ya kwanza ya nafasi hiyo.

Nafasi ya mwenyekiti ililazimika kurudiwa baada ya mshindi kushindwa kufika nusu ya kura zilizopigwa ambapo katika awamu hiyo, Shaibu Mtawa alipata kura 13, Farida Mgomi (397) na Mwishehe Mlao (392) huku Madega akiambulia 61.

Baada ya kurudiwa uchaguzi huo mchuano ulikuwa kati ya aliyekuwa Mwenyekiti wa zamani wa Chama hicho, Mwishehe Mlao aliyepata (479) na aliyekuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanake Tanzania (UWT) mkoa wa Pwani, Farida Mgomi ambaye aliambulia kura 341.

Kutokana na Matokeo hayo Telack alimtangaza Mlao kuwa mwenyekiti wa CCM mkoa wa Pwani baada ya kuongoza kwa kura katika uchaguzi huo.

Akizungumza baada ya uchaguzi huo Mchengerwa aliwashukuru wajumbe kwa kumchagua kwenye nafasi hiyo huku akiahidi ushirikiano katika kukiimarisha chama.

Mchengerwa alisema ni muhimu kuwa na chama imara kitakachokuwa mstari wa mbele kuwaletea wananchi maendeleo na kutatua kero zao, huku akiahidi kufanyakazi ya kujenga chama hicho.



Mwenyekiti wa Bodi wa Benki ya Afrika, Nehemiah Mchechu (wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa Benki hiyo, Adamu Mihayo (kushoto), wakiwa na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Sauda Kassim Msemo (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha wa BoT, Sadati Musa, wakati ujumbe wa BOA ulipofanya ziara ya kikazi Benki Kuu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ATCL yajivunia kusafirisha tani 3,000 za mizigo kwa mwaka

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL), linasafirisha tani 3,000 kwa mwaka ambazo ni wastani wa kilo milioni tatu za mizigo inayoingia nchini kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mizigo cha ATCL, Raymond Manyika, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu shughuli za usafirishaji wa mizigo ya shirika hilo.

Alisema kazi ya kitengo hicho ni kusafirisha mizigo kwenda nchi mbalimbali na mizigo inayoingia nchini kutoka mataifa hayo Afrika na nje ya Afrika.

Manyika alisema kwa wastani ATCL inasafirisha tani 250 ambazo ni sawa na kilo 250,000 kwa mwezi na kwamba mizigo mingi inayoingia nchini inatoka mji wa Mumbai, India na dawa mbalimbali za binadamu kutoka nchini humo.

"Kutoka China tunasafirisha sana vifaa vya kielektroniki, vipuri vya magari na nguo ambavyo wakati mwingine tunaingiza nchini na kusambaza kwenye nchi za Zimbabwe, Zambia, Uganda, Burundi na Sudan Kusini na hapa nchini kwa wafanyabiashara Watanzania wanaosafirisha mizigo mikubwa kutoka China kuja Tanzania ni kama GSM na Vunjabei," alisema.

Alitaja mizigo mingine inayosafirishwa nje ya nchi hususan China ni mazao ya bahari kama ngadu, samaki wa mapambo wakati wanasafirisha sana maparachichi kwenye mji wa Mumbai nchini India.

"India kuna soko kubwa sana la parachichi hivyo kiwango tunachosafirisha ni kikubwa sana na tunasafirisha maua kutoka Kilimanjaro Tanzania na Nairobi Kenya tunayasafirisha kwenda China," alisema Manyika.

Akizungumzia ushindani uliopo kwenye usafirishaji wa mizigo, Manyika alisema ushindani ni mkubwa kutoka kwenye mashirika makubwa ya ndege ya Emirates Airline, Ethiopian Airline, Qatar Airways na KLM.

"Kuna mashirika mengine makubwa ya ndege ambayo nayo yanafanya safari kwenye mataifa ambayo na sisi tunaenda lakini sisi tunapata faida kubwa moja kwamba tuna ndege za moja kwa moja wakati wao wanatua kwanza kwenye nchi mbalimbali. Mfano kama ni China tunakwenda moja kwa moja China kwa hiyo baadhi ya wateja wanapenda ruti hiyo," alisema.

# Waziri asifu uwekezaji SBL

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaud Kigahe, amezindua upanuzi wa kiwanda cha bia cha Serengeti, tawi la Moshi uwekezaji uliogharimu Sh. bilioni 185 katika matumizi ya mtaji.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika jana, Kigahe alisema upanuzi wa kiwanda hicho ni tukio kubwa kwa sababu inaonyesha kiwango cha uwekezaji SBL unaendelea kufanyika nchini ili kuongeza tija na kuongeza kasi ya ukuaji uchumi.

Sambamba na hilo, alisema uwekezaji huo unachangia fursa za ajira na wakulima wa ndani kupata soko la mazao yao na kupongeza SBL kwa kuwa na mitambo na vifaa vya kisasa vinavyoendeshwa kwa teknolojia ya kisasa katika kiwanda hicho.

**Wakulima hawa kwa pamoja huipatia SBL zaidi ya tani 20,000 za nafaka kwa mwaka, zikichukua zaidi ya asilimia 80 ya mahitaji yetu ya malighafi.**

"Serikali imefurahishwa sana na uwekezaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti katika sekta ya viwanda. Tena tunatambua kuwa uwekezaji huu umekuja katika kipindi ambacho serikali inajitahidi kupunguza urasimu katika uwekezaji na kutoa motisha kubwa kwa wawekezaji kuja Tanzania, kwa sababu ndiyo nchi sahihi yenye sera za kuvutia na fursa mbalimbali za uwekezaji," alisema.

"Watu wetu wanapata fursa za ajira na wakulima wanaweza kupata soko la mazao yao ikiwa kampuni nyingi kama SBL zitaendelea kuwekeza. Kampuni ya SBL imetoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi kwa kutengeneza ajira nyingi na kulipa kodi zinazosaidia bajeti ya nchi yetu. Tena mchango wake katika kuwainua wakulima kwa kununua mazao yao ni wa mfano wa kuigwa; na ushiriki wake katika shughuli mbalimbali za kijamii hapa nchini ni wa kupongezwa wakati wote." Alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, akizungumzia uwekezaji huo alisema: "Kiwango hiki cha uwekezaji hakika ni kielelezo tosha cha imani tuliyonayo sisi Serengeti Breweries na Diageo ni mbia wetu mkuu, katika uongozi wa serikali ya Tanzania kuunda mazingira dhabiti ambayo biashara zinaweza kustawi.

"Kujitolea katika kiwango hiki cha uwekezaji, SBL haiwi tu kama mshirika wa kutegemewa wa uwekezaji katika safari ya kiuchumi ambayo sote tunaianza, lakini pia kama balozi anayestahili wa nchi kwa wawekezaji wengine ambao, kama sisi, watatafuta fursa za uwekezaji," aliongeza.

Alisema kuwa zaidi ya nusu ya chapa za bia za SBL hutengenezwa kwa asilimia 100 ya malighafi za kienyeji (kama mahindi, shayiri na mtama), ambazo hutolewa kutoka kwa mtandao wa wakulima kote nchini ambao wanapokea usaidizi wa kiufundi na kifedha kutoka kwa kampuni katika shughuli zao za kilimo.

"Wakulima hawa kwa pamoja huipatia SBL zaidi ya tani 20,000 za nafaka kwa mwaka, zikichukua zaidi ya asilimia 80 ya mahitaji yetu ya malighafi. SBL hutengeneza aina mbalimbali za vileo, zikiwamo bia na vinywaji vikali. Bia kuu ni pamoja na Serengeti Premium Lager, Serengeti Lite, Guinness Stout, Guinness Smooth na Pilsner Lager. Bidhaa hizi zote zimepokea tuzo nyingi za ubora ndani ya nchi na kimataifa.

Ocitti alisema kati ya mwaka 2019 na 2020, Sh. bilioni 31 ziliwekezwa katika kiwanda cha bia cha Dar es Salaam; Sh. bilioni 13.4 katika ujenzi wa kituo cha uzalishaji wa vinywaji vikali na Sh. bilioni 124 katika upanuzi wa kiwanda cha kuzalisha bia mjini Moshi.

Pia alisema Serengeti ilitumia Sh. bilioni 15.7 nyingine kupanua kiwanda chake cha bia cha Mwanza.



Mkuu wa Kitengo cha Ubunifu cha Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Bertha Vedastus (katikati) na wafanyakazi wenzake, wakionyesha chupa ya bia mpya ya Rockshore, ikiwa ni ishara ya kuizindua jijini Dar es Salaam juzi. Wengine (kutoka kushoto) ni wafanyakazi wa SBL, Nicholas Chonya, Malalia Mmassy, Samuel Kisyombe, Jessica Sanga na Joseph Innocent. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Benki yaendesha droo chanja kijanja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania imeendesha droo ya pili ya kampeni yake "Chanja Kijanja, Kimasta Zaidi" inayolenga kuhamasisha wateja wake kutumia kadi za Mastercard kununua mtandaoni au kufanya malipo kupitia mashine za malipo (POS) katika maduka mbalimbali na maeneo mengine nchini.

Kampeni hiyo iliyozinduliwa mapema mwezi Novemba inatoa fursa kwa jumla ya washindi 185 miongoni mwa wateja wa benki hiyo wanaotumia kadi zao za Exim Mastercard kufanya miamala.

Wakifanya hivyo watajishindia zawadi mbalimbali ikiwamo fedha taslimu, simu janja (Smart Phones) na safari zilizolipiwa gharama zote kwenda mapumziko katika mataifa ya Dubai, Uturuki na Afrika Kusini wao pamoja na wenza wao.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya uendeshaji wa droo ya pili ya kampeni hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki kwenye makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam, Ofisa wa Idara ya Huduma Mbadala Kupitia Mifumo ya Kidigitali wa Benki ya Exim, Gregory Malembeka alisema benki hiyo imeridhishwa na mwitikio mkubwa kutoka kwa wateja wake katika matumizi ya kadi hizo kufuatia kampeni hiyo.

"Kampeni hii imeonyesha mafanikio katika hatua yake ya awali kabisa. Imepokelewa kwa mwamko mkubwa kutoka kwa wateja wetu hatua ambayo tumeitafsiri kwamba ni wazi wateja wetu wananufaika na wanafurahia huduma zetu," alisema Malembeka.

Alisema kupitia kampeni hiyo kila muamala wenye thamani ya Sh. 100,000 na zaidi ukiwa umefanyika kwa mara moja zaidi kupitia card ya MasterCard ya benki hiyo muhusika atastahili kushiriki bahati nasibu ya kumpata mshindi.

"Hii ni droo ya pili ya kila wiki ambapo kila wiki wateja 15 wanaobahatika wamekuwa wakipata nafasi ya kujishindia zawadi ya fedha taslimu TZS. 100,000," alisema na kuongeza.

Akizungumzia zawadi kuu kwa washindi wa kampeni hiyo, Malembeka alisema washindi hao watazawadiwa safari ya mapumziko ya siku tano wao pamoja na wenza wao, safari ambayo itagharamiwa kila kitu na benki ya Exim ikiwamo visa, tiketi ya ndege pamoja na pesa za matumizi.

"Hivyo basi mshindi wa kwanza atajishindia zawadi ya kwenda Dubai yeye na mwenza wake na wakiwa huko watapata fursa ya kutembelea vituo mbalimbali ikiwemo 'Museum Of The Future' pamoja na Jangwa la Safari.

# Manispaa Singida yajenga majosho kwa mil. 36/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Singida imejenga majosho mawili mapya kwa Sh. milioni 36 ili kuwawezesha wafugaji kuogesha mifugo yao, hivyo kujikinga na magonjwa.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Hagai Zakaria, alisema jana kuwa kila josho limegharimu Sh. milioni 18 na yote yana ujazo wa lita 12,000.

Hagai alisema katika kijiji cha Mtisi Kata ya Mtamaa, zaidi ya ng'ombe 1,200 na mbuzi 700 wameanza kuogeshwa wakati katika kijiji cha Manga Kata ya Mtipa ng'ombe 800 na kondoo 88 wameogeshwa.

Akifafanua juu ya gharama za uogeshaji mifugo, Hagai alisema gharama kwa ng'ombe mmoja ni Sh. 100 wakati mbuzi na kondoo ni Sh. 50 na fedha zinazokusanywa hutumika kununua dawa za kuogeshea mifugo.

"Mwitikio wa wafugaji ni mkubwa na zoezi linaendelea na fedha tunazokusanya tunanunua dawa kwa kuwa zoezi ni endelevu," alisema.

Hagai alisema serikali imekuwa ikitoa dawa za ruzuku kwa majosho yote yanayofanyakazi na kwamba Manispaa ya Singida ilishapokea dawa za ruzuku lita 72 aina ya Paranex.

Aliongeza kuwa Manispaa ya Singida katika kuhakikisha mifugo inakuwa katika afya njema imetenga kiasi cha Sh. milioni 10 katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2022/2023 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ukarabati wa majosho ya Mtipa na Unyambwa.

Wakati huo huo, Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi imetoa mafunzo kwa wavuvi 83 kuhusu uvuvi endelevu, usalama mwaloni na kuorodhesha wavuvi ili kujiunga na Chama cha Jamii ya Wavuvi (BMU).

Mafunzo hayo yamelenga kujengea uwezo wavuvi juu ya matumizi ya zana bora za uvuvi zinazokubalika kisheria, madhara ya uvuvi haramu ikiwamo matumizi ya makokoro, usalama wa wavuvi wawapo katika shughuli za uvuvi, ulinzi shirikishi ili kudhibiti uhalifu na umuhimu wa kujisajili ili kupatiwa leseni za mitumbwi.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa ushirikiano baina ya wataalamu wa idara ya kilimo, mifugo na uvuvi, polisi, ofisi ya Mwenyekiti wa serikali ya Mtaa wa Bomani pamoja na Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Mughanga.

# Achaguliwa mwenyekiti mwenza Baraza la Biashara

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MFANYABIASHARA maarufu Wilfred Daniel, amechakuguliwa kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Baraza la Wafanyabiashara Wilaya ya Arumeru, baada ya kushinda kwenye uchaguzi huo.

Daniel amepata nafasi hiyo ya kuliongoza baraza hilo kwa kipindi cha miaka mitatu, baada ya kupata kura 19, kati ya kura 49 zilizopigwa na kuwashinda wagombea wenzake watatu waliowania nafasi hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Richard Ruyango, ambaye ndiye mwenyekiti wa baraza hilo, alisema kwa mujibu wa kanuni, anamtangaza Daniel kuwa mwenyekiti mwenza wa baraza hilo na makamu mwenyekiti mwenza, Maija Mchau, aliyepata kura 17.

Mkuu huyo wa wilaya aliwaagiza viongozi hao kusimamia miongozo na kufahamu dhumuni la kuwapo kwa baraza na kuweka mpango mkakati wa utekelezaji wa kazi kufikia malengo.

Pia alisema baraza hilo linapaswa kushirikishana kutatua matatizo yanayowakabili wafanyabiashara kwa maendeleo ya wananchi na taifa.

"Serikali inatambua huduma mnayoitoa kwa jamii, ninawaagiza viongozi, kaeni na wafanyabiashara wenzenu mpate maoni yao, mkaishauri serikali namna bora ya kwenda na kuweka mazingira rafiki ya kuendesha biashara kwa kuwa itasaidia kuchochea maendeleo binafsi na ya taifa kwa ujumla," alisema.

Baada ya kuchaguliwa, Wilfred aliwashukuru wajumbe wa mkutano huo kwa kumwamini na kumchagua kushika nafasi hiyo, huku akiahidi kushirikiana na wafanyabiashara wote.

Vilevile, alisema ataitumikia nafasi hiyo kwa uaminifu ili kufikia lengo la serikali kupitia Baraza la Wafanyabiashara, kwa kutumia nafasi yake kuwaunganisha na serikali.

Mkuu wa Idara ya Biashara na Uwekezaji, Halmashauri ya Meru, Noel Pallangyo, alisema majukumu ya baraza hilo ni kuzikutanisha sekta binafsi pamoja na serikali, kujadili na kupeana ushauri wa uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji na kukuza sekta ya uchumi.

Alitaja majukumu mengine ya baraza hilo, kuwa ni pamoja na kutengeneza mazingira bora ya kufanyia biashara na uwekezaji, kuibua fursa za uwekezaji, kuzinadi fursa kupitia makongano mbalimbali na kufanya matangazo ya biashara.

**Nitaitumikia nafasi hiyo kwa uaminifu ili kufikia lengo la serikali kupitia Baraza la Wafanyabiashara, kwa kutumia nafasi yake kuwaunganisha na serikali.**

# Kilio cha maji chasikika

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HATIMAYE serikali imesikia kilio cha wakazi wa Kijiji cha Samaria kilichoko Kata ya Nduruma, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, baada ya kupeleka Sh. milioni 30 za kuchimba kisima kirefu cha maji ili kumaliza adha hiyo.

Mbunge wa Arumeru Magharibi, Noah Lembris, akizungumza na wakazi wa kijiji hicho jana, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma ya majisafi na salama ndani ya mita 400.

"Kwa kuwa sasa tatizo hili limepata ufumbuzi wa kudumu, niwaombe sana viongozi wa kata hii kusimamia kwa uadilifu mradi huo ili kila mwananchi aweze kunufaika. Tunajipanga vyema namna ya kupanua na kuendeleza mradi huu, kwa kusogeza huduma karibu na wananchi," alisema.

**Tunajipanga vyema namna ya kupanua na kuendeleza mradi huu, kwa kusogeza huduma karibu na wananchi.**

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, aliwashukuru familia iliyotoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo, akisisitiza kuwa kila mwananchi ana wajibu wa kutunza miundombinu iliyojengwa iendelee kuwasaidia.

"Kwa kipindi kirefu kulikuwa na shida ya maji katika eneo hili. Mama zetu walikuwa wanahangaika huku na kule kwenda kutafuta maji kwa mateso, lakini tunamshukuru Mungu kwa kwa mradi huu, nawasihi kuendelea kutunza miundombinu ili idumu na kuwahudumia wananchi wote," alisema.

Diwani wa Nduruma, Raymond Mollel, akitoa shukrani kwa niaba ya wananchi wake, alisema kutokana na historia ya eneo hilo, walikuwa wakiaminishwa kwamba hakuna uwezekano wa kupata maji katika kijiji hicho, hivyo kujengwa kwa kisima hicho ni neema kwa wakazi wa Samaria.

Mmoja wa wakazi wa Samaria, Damari Nnko, alisema kukamilika kwa mradi itakuwa faida kwa wakazi hao, kwa kuwa itasaidia kuondoa adha iliyokuwapo awali hasa kwa wanawake ambao waliteseka kutembea umbali mrefu kutafuta maji.

"Sasa tumefikia ukomo wa mateso ya kutafuta maji, wanawake wa Samaria, tunaishukuru serikali kwa kutushika mkono kukamilisha mradi kwa kuwa itarahisisha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama na kuondoa kabisa kero kinamama. Pia tunaamini serikali itaendelea kutusaidia ili maji yafike katika maeneo yote ya kijiji hiki," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhandisi Richard Ruyango (katikati), akizungumza katika hafla kukabidhi vifaa tiba vilivyotolewa msaada na Benki ya NMB, kwa zahanati ya Kikatiti, wilayani humo mkoani Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Toima bosi mpya wa CCM Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

PETER Toima, ambaye aliwahi kuwa Mkuu wa Wilaya za Rombo (Kilimanjaro) na Kakonko (Kigoma), amechaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Manyara.

Toima alishinda kiti hicho juzi baada ya kumwangusha kwa kura 423 aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Simon Lulu, ambaye alipata kura 391 wakati akipambana kutetea nafasi hiyo.

Akitangaza matokeo hayo, msimamizi wa uchaguzi huo, Rosemary Senyamule, ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, alisema amefarijika wajumbe wa mkutano huo wa uchaguzi na wagombea walivyoufanya uchaguzi kuwa mwepesi kutokana na kuheshimu taratibu za uchaguzi.

"Wagombea waliwania nafasi hii walikuwa watatu. Fratern Kwahhison, ambaye hayumo ukumbini hapa amepata kura tatu, Simon Lulu amepata kura 391 na Peter Toima amepata kura 423. Kwa mamlaka niliyo nayo, namtangaza rasmi Peter Toima, kuwa Mwenyekiti mpya wa CCM Mkoa wa Manyara," alisema Senyamule.

Toima baada ya kustaafu, alianza kujijenga zaidi kisiasa katika wilaya zote za mkoa kupitia shirika lisilo la kiserikali la ECLAT Foundation, akijenga vyumba vya madarasa, vyoo, kutoa misaada ya mahindi kwa shule zinazokabiliwa na uhaba wa chakula na kusaidia familia au kaya maskini.

Baada ya kutangazwa kuwa mshindi, Toima aliwashukuru wajumbe wa mkutano huo, kwa kumchagua kuwa mwenyekiti mpya wa CCM mkoa huo akisema: "Nawashukuru wote kwa kuniamini na kunipa kura. Tuendelee kushirikiana ili nami nitimize yale niliyoyaahidi kupitia CCM ya uchumi Manyara."

Aidha, Senyamule, alimtangaza Joachim Muungano kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), kupitia Mkoa wa Manyara, baada ya kushinda uchaguzi huo kwa kupata kura 407.

Muungano aliwashinda washindani wake Lenganasa Soipey, aliyeambulia kura 371 na Denis Bakuza aliyepata kura 23, kati ya kura zote zilizopigwa na wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi huo.

# Asasi yachangamkia urejelezaji taka

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MCHAKATO wa urejelezaji taka za kielektroniki, umeifungua macho asasi ya Roots & Shoots kuanzisha vituo vya kikanda vya urejelezaji taka za plastiki kwenye Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ili kuzuia uharibifu wa mazingira uliogeuka tishio kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Asasi hiyo inafanya kazi chini ya Taasisi ya Kimataifa ya Uhifadhi na Ulinzi wa Mazingira ya Jane Goodall Institute.

Jana, Mratibu wa Klabu ya Roots & Shoots ya Mkoa wa Kilimanjaro, Ahimidiwe Makisa, alisema mitambo iliyofungwa katika wilaya za Moshi, Hai na Arusha, itatumika kuchakata taka zote za plastiki zinazookotwa na zingine za aina hiyo, baada ya kupelekwa kiwandani.

"Tumeanzisha 'plastic recycling' iko Shule ya Sekondari Boma (Hai) ambako tayari mradi umeshaanza kufanya kazi. Ya pili inaanza kazi hivi karibuni Shule ya Sekondari ya JK Nyerere (Manispaa ya Moshi) na Moshono Sekondari (Arusha).

**Taka ambazo ni hatari zaidi, ni taka za plastiki ambazo zinaweza zikakaa zaidi ya miaka 100 bila ya kuoza au kuharibika.**

"Kwa hiyo tulichokifanya kwa kupitia wabia wetu wengine, ambao ni Asasi ya Greenmanjaro, Sisi Roots & Shoots, tumeanzisha recycling plant (mitambo ya urejelezaji taka) za plastiki kwenye Shule ya Sekondari ya JK Nyerere. Na hawa Greenmanjaro, ndio waliotufadhili kwenda kuanzisha hiyo plant (mtambo).

"Maana yake hizi bidhaa zote za plastiki tulizookota na nyingine za aina hiyo, tutazipeleka pale kiwandani, tutazichakata na zitatoka bidhaa nyingine kwa mfano, tutazalisha vikombe, sahani, vyombo vya kuwekea maua na peving. Kwa hiyo tutakuwa tumeokoa mazingira yetu kuharibiwa," alisema.

Aidha, Makisa alifafanua kuwa asasi hiyo imeamua kuwekeza kwa kufunga mashine nyepesi. Mashine moja kazi yake ni kukatakata taka za plastiki na mashine nyingine inayeyusha na kuanza kuunda bidhaa mbalimbali kutokana na uji uji, unaotoka kwenye mashine.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, katika vituo kulikofungwa mitambo hiyo, wanufaika watakaofundishwa na kupata ujuzi mkubwa wa kuzirejeleza taka na kisha kutengeneza bidhaa mbalimbali za viwandani ni wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo ambao ni wanachama wa Roots & Shoots.

Alisisitiza kuwa kwa kupitia ubunifu huo, watakuwa wameisaidia serikali kutatua tatizo la ajira nchini, kwa sababu vijana watakaopatiwa ujuzi huo watakuwa na ndoto zaidi za kuendeleza vipaji vyao vya kisayansi.

Wiki iliyopita, Asasi hiyo ya Roots & Shoots, ilianzisha kampeni maalumu ya kuzuia uharibifu mkubwa wa mazingira unaoendelea katika Msitu wa Hifadhi Asili wa Rau, ambao wananchi wanaouzunguka wameugeuza dampo la kutupa taka.

Msitu wa Hifadhi wa Rau, unaomilikiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), ukiwa na ukubwa wa hekta 584, ndio pekee wa hifadhi ya asili nchini Tanzania, ulioko katikati ya mji. Msitu huo, uko Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Akizungumzia kampeni hiyo, Mratibu wa Roots & Shoots wa Ofisi ya Kanda ya Kaskazini iliyoko mkoa wa Arusha, Erasto Njavike, alisema kampeni hiyo inalenga kuokoa hifadhi hiyo isiharibiwe.

Katika kampeni hiyo, wadau hao wa uhifadhi na ulinzi wa mazingira, waliokota uchafu, ambao ni viroba 65 vya magunia yaliyojaa chupa za platiki za maji, sharubati, pombe kali na mafuta ya aina mbalimbali, yanayotupwa na wanaoingia ndani ya msitu huo.

"Tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba tunaondoa taka zote, kwa sababu msitu huu umezungukwa na makazi ya watu na vijiji. Wakazi wengi ambao wameuzunguka msitu huu, ambao sio waaminifu, wanatupa taka kwenye msitu.

"Taka ambazo ni hatari zaidi, ni taka za plastiki ambazo zinaweza zikakaa zaidi ya miaka 100 bila ya kuoza au kuharibika. Imetulazimu kupeleka ndani ya hifadhi na nje ya hifadhi wanafunzi 100 wa Shule ya Sekondari ya Mji Mpya, Sekondari ya JK Nyerere, Shule ya Msingi Langoni na Shule ya Msingi Shauri Moyo."



Diwani wa Viti Maalum, Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mwahamisi Maumba (kushoto), akitoa elimu ya kutengeneza sabuni za maji na vitenge kwa walimu wanawake wa shule za msingi na sekondari wilayani humo juzi ili waweze kujipatia kipato cha ziada na kuepukana kujiingiza kwenye mikopo umiza. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Achaguliwa tena mwenyekiti CCM mkoa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MFANYABIASHARA Patrick Boisafi, amefanikiwa kutetea nafasi yake ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, baada ya kupata ushindi wa 'kimbunga' wa kura 883 dhidi ya Golden Swai, aliyepata kura 31 na Alphonce Temba, kura 26.

Boisafi ambaye ataongoza Kilimanjaro kwa kipindi cha pili mfululizo, alishinda kiti hicho juzi wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi huo uliofanyika jana katika mji wa Moshi.

Msimamizi wa uchaguzi huo, Omari Mgumba, ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, alimtangaza Boisafi kuwa mshindi wa kiti hicho, huku akiwasisitiza ni lazima wagombea ambao kura zao hakikutosha na wale waliochaguliwa, kuvunja makundi yao ili kuiepusha CCM na majeraha ya uchaguzi kuelekea uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025.

"Wakati wa uchaguzi, lazima chama kiwe na pande zinazotofautiana kwa hoja kama njia ya kujenga demokrasia. Lakini baada ya matokeo, CCM inabaki kuwa moja. Kama ndivyo! Wagombea wote ambao mmekubali wenyewe matokeo mliyoyapata kwa kila nafasi, mvunje makundi na muungane na washindi kuijenga CCM," alisema.

Uchaguzi huo ulifanyika baada ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, chini ya Mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan, kuchuja majina ya viongozi wa ngazi ya mkoa, ukiwa ni mtihani wa wake wa kwanza tangu ashike wadhifa huo mwaka jana.

Safu iliyoanza kujengwa hivi sasa kuanzia shina, matawi, kata, wilaya na mikoa, chini ya Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, itafanya maandalizi yote muhimu ya mpambano wa uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025.

Aidha, Mgumba alimtangaza mfanyabiashara Suleman Mfinanga, mkazi wa Wilaya ya Mwanga kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kupitia Mkoa wa Kilimanjaro, baada ya kupata kura 862 na kuwashinda Tumaini Mushi aliyepata kura kura 51 na Yusuph Furutuni kura 11.

Akizungumza baada ya uchaguzi huo, Boisafi aliwashukuru wajumbe wa mkutano huo kwa kumwamini na kumrejesha kuendelea kuwa mwenyekiti wao.

# DC aonya viongozi ubadhirifu fedha

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, Abbas Kayanda, ametangaza vita dhidi ya viongozi wa vitongoji, vijiji na kata ambao katika maeneo yao kutabainika kufanyika ubadhirifu wa fedha za miradi ya maendeleo au wizi wa michango ya wananchi.

Amesema watakaobainika kushiriki kuihujumu serikali, watapoteza kazi na kisha kukamatwa na kuburuzwa kortini, kujibu tuhuma zinazowakabili.

Kayanda alikuwa akizungumza jana na wananchi wa vijiji vya ukanda wa tambarare, baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa viongozi wa Bodi ya Maji ya Kirua /Kahe.

"Serikali haitamvumilia mtu yoyote atakayelima pembezoni mwa vyanzo vya maji au mbadhirifu wa miundombinu ya maji. Na ninyi viongozi wa vitongoji, vijiji na kata hakikisheni kwamba mnawakamata wanaoharibu miundombinu ya maji kukamatwa na kuwapeleka mahakamani.

"Kiongozi yeyote atakayeshindwa kusimamia eneo lake la utawala na ubadhirifu ukafanyika kwenye eneo, basi kiongozi huyo atalazimika kulipa fedha hiyo. Tusiwaonee haya watu hawa, hata kama ni shemeji zenu au ndugu zako. Fedha ambayo itatumika kununulia miundombinu mingine, inaweza kupeleka maji sehemu nyingine," alisema.



Ukurasa 19

**BRIGEDIA JENERALI NNAUYE**
**Kiongozi anayestahili heshima muda wote ana alama vita vya Kagera, kuhamasisha askari**



Ukurasa 16

Migogoro ya uongozi ndani ya vyama vya siasa, vingine vilivyoishiwa 'pumzi'



Ukurasa 19

**NYANZOBE MAKWAIYA**
**Maajabu ya binti aliyeanza kuwa kiongozi akiwa na miaka mitatu**



UTEUZI FAINA ZEC

# Wanachama ACT kuamua mustakabali maridhiano

- AFP yaungana kumpinga
- TADEA yasita 'kumfosi' Rais



Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo, Juma Duni Haji akizungumza na Baraza la Wazee la chama hicho. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

CHAMA cha ACT -Wazalendo kimetangaza kuanza mchakato wa kushirikisha wanachama wake kutathmini mwenendo wa miaka miwili ya maridhiano ya kisiasa Zanzibar.

Hatua hiyo inaanza kwa kupokea maoni ya wanachama wake ili kupata hisia zao kuhusu mustakabali wa mafanikio, matatizo na changamoto za juhudi hizo, anatangaza Mwenyekiti wa chama Juma Duni Haji.

Anaeleza kuwa kimeridhia kupokea maoni kwa wananchama kuhusu kazi hiyo ya kisiasa baada ya Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi kumteua Thabit Idarusi Faina, kuwa Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), jambo analodai linazusha mjadala mkubwa ndani ya chama hicho na hivyo kutaka kusikia wanachama wana maoni gani.

Anasema wanachokilalamikia ni yale yaliyotokea katika uchaguzi wa mwaka 2020 wakati Faina akiwa Mkurugenzi wa Uchaguzi ZEC, hivyo yasijitokeze tena katika uchaguzi huo ambao ACT-Wazalendo hawayakubali.

Anasema uchaguzi ndiyo kiini cha mifarakano Zanzibar hivyo ni lazima kutayarisha uchaguzi huru, wa haki na unaokubalika na anayeshinda atangazwe bila kuwa na kona kona au mazingira yanayolalamikiwa.

Mwenyekiti Duni akizungumza juzi na wazee wa ACT- Wazalendo visiwani hapa, anasema lazima wanachama kulijadili kwa uwazi, undani na kulitafakari vya kutosha kuhusu maridhiano ya kisiasa Zanzibar ambayo chama hicho ni sehemu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

"Niwaombe wanachama msiogope kutoa mawazo yenu mnayoyaamini, kuhusu mustakabali wa maridhiano ya kisiasa na mawazo ya wengi ndiyo yatakayoridhiwa na chama"anasema Duni.

Mwenyekiti huyo anasema chama hicho kimeridhia maridhiano hayo ni miaka miwili imesalia hivyo wanahitaji kufanya tathmini kwa sababu njia ya maridhiano ndiyo pekee itayoifikisha kwenye kujenga nchi kwa salama na amani.

Anasema lengo la maridhiano hayo kuyatafutia ufumbuzi wa matatizo ya kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa visiwani humo.

Anawaeleza kuwa licha ya madhila na mateso mbalimbali waliyopitia katika chaguzi zilizopita lakini ifike mahala kusahau yaliyopita na kushikamana kwa ajili ya Wazanzibari wote na taifa zima.

"Yaliyopita si ndwele tugange yajayo Wazanzibari tutakaposhikamana na kuridhiana amani na usalama wa nchi utapatikana. Upendo na uvumilifu na kusameheana ni muhimu ili kuponya majeraha,"anasema.

Aidha, anasisitiza kuwa bila ya maridhiano hakuna maendeleo hivyo ni lazima kupendana, akiongeza kuwa kwenye mfarakano huwezi kupata maendeleo na muwekezaji akijua nchi fulani wanagombana hapeleki rasilimali zake, kwa vile anafahamu hakuna tija.

"La msingi ndugu zangu na CCM wananisikia maridhiano na sisi hatutokuwa wa mwanzo au wamwisho, Marekani na Uingereza waligombana lakini leo ni marafiki, Wajapani na Waamerika kadhalika walipigana lakini leo ni rafiki na wapo wanaishi,"anakumbusha Duni.

Pia anatoa mfano wa mapigano ya Afrika Kusini ambayo kulikuwa na mapingano kati ya Wazungu na weusi, lakini imefika mahali wamemaliza tofauti zao na sasa ni mfano wa nchi zilizoendelea barani Afrika ambazo hazina ugomvi.

Anasema miaka 17 Msumbiji walikuwa wana-

INAENDELEA UK. 14

## UTEUZI FAINA ZEC

# Wanachama ACT kuamua mustakabali maridhiano

**INATOKA UK. 13**

pigana wenyewe kwa wenyewe lakini pia Kenya hivi karibuni walipigana na kuuana leo kuna maridhiano na wamejenga umoja na kufanyakazi pamoja kuendeleza nchi yao.

"Wazanzibari na mwafaka bado tunafikiria eti tukigawana tutafanikiwa, haiwezekani kufanikiwa kwa mifarakano, "anasisitiza kuwa cha muhimu ni maridhiano na uvumilivu wa kisiasa.

**ACT WAUNGWA MKONO**

Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima AFP, Said Soud, anatangaza kuungana na ACT- Wazalendo kupinga Faina kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa ZEC ili kuiepusha nchi kuingia katika vurugu za uchaguzi.

"Ili Rais Mwinyi afanikishe kutafuta suluhisho la mwafaka litakalojenga imani za Wazanzibari amwondoe Faina na atakayemweka si vibaya akipigiwa kura na vyama vya siasa ili kuonyesha uwepo wa maridhiano ya kweli."

"Ikiwa hajaanza kazi watu wanamkataa je akianza majukumu itakuwaje? Demokrasia haitaki mivutano na hasa pale kiongozi mkuu anapoahidi atafanya maridhiano na kuyaendeleza sasa maridhiano yanaanza katika ngazi ya chini halafu yanapanda juu,"anasema Soud.

Mwenyekiti huyo anasema Rais Hussein Mwinyi, anashauriwa na ingependeza kama atakuwa tayari kusikiliza maoni ya vyama vya siasa hasa vile vyenye nguvu zaidi na vilivyothubutu kuingia katika serikali yake na kuunda SUK.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, ni miongoni mwa wanaounda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. **PICHA: MAKTABA.**

Anaeleza kuwa katika uchaguzi uliopita wa mwaka 2020 yeye alinyimwa kura wakati huo Mkurugenzi wa Uchaguzi ZEC akiwa Faina hivyo hata yeye hawezi kumhitaji mkurugenzi huyo.

**TADEA YAONYA ACT**

Juma Ali Khatib ni Mwenyekiti wa Chama cha Ada-TADEA anayesema maridhiano ya kisiasa hayajatoa uhalali wa viongozi wa chama cha ACT-Wazalendo kuingilia madaraka ya Rais wa Zanzibar ambayo yapo kwa mujibu wa katiba.

Anafahamisha kuwa viongozi wa chama hicho hawatakiwi kumpangia kazi Rais ambaye majukumu yake yako kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi ambapo halazimiki kupokea ushauri wa mtu katika shughuli za utendaji wa kazi zake za kila siku. "Mimi nawasihi wanasiasa wenzangu kuacha kufanya hivyo kuingilia majukumu ya Rais, ameonyesha nia ya dhati ya kutekeleza maridhiano ya kisiasa ambayo lengo lake ni kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar aachwe "anasema Khatibu.

Anaungwa mkono na Naibu Katibu Mkuu UVCCM Zanzibar, Mussa Haji Mussa, anasema kitendo cha kuingilia majukumu ya Rais Mwinyi katika eneo la uteuzi ni sawa na kuingilia katiba pamoja na kudharau maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa ambayo serikali imeonyesha nia ya kuyatekeleza kwa vitendo.

Anasema katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake maridhiano yametekelezwa kwa vitendo ikiwamo Rais kufanya juhudi za ziada za kuunda kikosi kazi kwa ajili ya kuyapatia ufumbuzi mambo mahususi kwa siasa za Zanzibar.

Anaongeza kuwa masuala ya kuteua mtendaji pamoja na kutengua yapo katika mamlaka ya Rais wa Zanzibar ambayo hakuna kiongozi mwenye uwezo wa kuhoji maamuzi hayo.


"Rais akiteua na kutengua hakuna kiongozi mwingine wa kuhoji maamuzi hayo na hili ni kwa mujibu wa katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hili la kumshurutisha maamuzi yake linakwenda kinyume na katiba"anakumbusha Musa.

## CHEMSHABONGO NA -00 24 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. kasirika ghafla
8. mwanzo
9. ndugu mkubwa wa kiume
10. sehemu iliyotengenezwa rasmi watu kukaa na kuzungumza
11. pengine 12. ujiuji unaotoka kwenye volkano 13. rejea mahali
14. mwisho wa kitu 17. afya
19. shauku ya kufanya jambo
21. msafiri 22. chakula chenye umbo la nyuzi 25. Kazeh ya sasa
27. kambi 28. kipaumbele


Chini:
1. taarifa
2. zama 3. magonjwa 4. Uo 5. giza
6. fikiri jambo kwa makini
7. kuwa na hamu ya kupata kitu
14. mganga
15. yenye madoadoa mwili mzima
16. weka kitu ndani
18. upungufu wa kitu 20. kata
23. korongo la maji yatiririkayo wakati wote 24. badilisha kitu kwa fedha 26. labda



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

KIUA, TUNDA, TANGAZA, ADAA, DAIMA, IMARA, ADHABU, MARAIS, HIMAYA, MUNGU, ANASA, MAALUM, MAUTI, TAWI, UTALII, MBUYU

HAU, MADA, UDI, NINI, NANI, TUMA, AMAA, ONA, TOA, AGA, ZOA, UHAI, AWA




Majibu toleo lililopita



BRIGEDIA JENERALI NNAUYE

# Kiongozi anayestahili heshima muda wote ana alama vita vya Kagera, kuhamasisha askari

• Ndiye aliyemwibua John Komba TOT, aliupenda wimbo Guajira Guantanamera

**Na Owden Kyambile**

NI mmojawapo wa viongozi wakamilifu ambao wamefanya kazi kubwa kwa taifa katika juhudi binafsi za kufanikisha majukumu yanayostahili heshima yaliyofanyika nje na ndani ya nchi.

Si mwingine ni Brigedia Jenerali (mstaafu) Moses Nnauye, ambaye hata sasa taifa linaendelea kutambua kile ambacho amekifanya kwenye utumishi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) CCM na serikalini.

Brigedia Jenerali Nnauye aliyefariki Desemba 6, 2001, ni mmoja kati ya viongozi waandamizi wasiosahaulika kutokana na utumishi wao uliotukuka, wakilitumikia taifa katika idara mbalimbali.

Ni mpiganaji mahiri aliyeshiriki kikamilifu katika vita vya Kagera, akiwa na jukumu kubwa la kuwahamasisha maofisa na wapiganaji kupitia nyimbo mbalimbali alizozitunga, akitumia bendi za muziki za JWTZ kama Mwenge pamoja na kwaya ilivyokuwa ikiongozwa na Kapteni John Komba, sasa ni marehemu.

Nnauye pamoja na Kapteni Komba walikuwa na wajibu wa kuhakikisha askari wanahamasika kwa kuburudishwa baada ya kazi ngumu za medani, kuwatia hamasa na propaganda ili wasikate tamaa.

Nnauye alipitia mafunzo mengi sana ya muda mfupi na mrefu, ni kiongozi aliyekuwa ameandaliwa, ni askari aliyekuwa amekidhi matarajio ya wananchi kwani kila idara aliyoiongoza alionyesha uadilifu, weledi na kujituma kwa hali ya juu.

Alikuwa mwasisi wa vikundi vya chama tawala kama Youth League, alivihamasisha vikundi mbalimbali kukikubali chama tawala kwa misingi ya uzalendo na umoja kwa taifa lao. Kati ya mwaka 1966 na 1967 wakati Azimio la Arusha limetangazwa, vijana wa TANU waliwahi kuwa na wasiwasi kuhusu misingi ya ujamaa uliotegemewa kuanzishwa nchini, Nnauye alishirikiana na aliyekuwa Katibu Mkuu wa TANU, Elly Anangisye, kuwafafanulia wasomi dhamira kuu na madhumuni ya Azimio la Arusha.

Brigedia Jenerali Nnauye alikuwa Muislamu kwa jina la Mussa Nnauye lakini aliamua kujipa jina la Moses ili apate nafasi ya kusoma shule za madhehebu ya Kikristo.

Enzi hizo waliotakiwa kusoma huko ni Wakristo pekee, vijana wengi Waislamu waliamua kuingia kwenye kundi hili, mmojawapo alikuwa Waziri wa Fedha awamu ya pili Kighoma Maluma.

Nnauye alikuwa mnadharia mahiri na mwenye uwezo mkubwa wa uchambuzi wa masuala ya kisiasa. Alitumia kipaji chake cha muziki katika harakati za kupigania uhuru, alianzisha na kuendeleza vikundi mbalimbali vya kwaya, taarabu na bendi, pia wasanii mbalimbali waliibuliwa kwa juhudi zake na wakalelewa kama wanawe ili waendelee katika muziki.




Mmoja wa wanamuziki wakongwe nchini alisikika hivi karibuni akisema " Kila nikisikia wimbo wa 'Guajira Guantanamera,' namkumbuka mzee Moses Nnauye ambaye kwa mara ya kwanza nilikuwa naye mwaka 1987."

"Wakati nipo katika bendi ya Tancut Almasi, wakati huo tulikuwa tumepiga kambi kwa miezi kadhaa Dodoma Hotel. Alitukaribisha nyumbani kwake na kutuonyesha santuri origino ya wimbo wa Guantanamera."

Brigedia Jenerali Nnauye ndiye aliyegundua kipaji cha Kapteni John Komba na akamtoa katika ajira yake ya ualimu na akamwingiza jeshini ili aendeleze kipaji chake cha uimbaji.

> "Wakati nipo katika bendi ya Tancut Almasi, wakati huo tulikuwa tumepiga kambi kwa miezi kadhaa Dodoma Hotel. Alitukaribisha nyumbani kwake na kutuonyesha santuri origino ya wimbo wa Guantanamera."

### MKUU WA MKOA

Wakati Nnauye alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, aliwavutia wanamuziki kadhaa kutoka bendi ya Black Star na Lucky Star za Tanga na wanamuziki kadhaa akiwamo Wazir Ally wa Kilimanjaro Band waliamua kuwa wanamuziki wa bendi ya Kingita Ngoma, iliyokuwapo mkoani Singida wakati huo.

Nnauye alikuwa mwamba wa siasa za CCM na mwanzilishi wa makundi ya chipukizi na green guards, ilikuwa ni mbinu zake kuiimarisha TANU na kuitumikia katika nafasi mbalimbali na hasa wakati alipokuwa mkuu wa mkoa Singida.

Anakumbukwa kwa kuwapa misaada makada wenzake kama ambao wakati huo walikuwa wanashika nyadhifa kama za katibu tarafa katika wilaya za mkoa huo.

Alikuwa kiongozi wa kujitoa na kusaidia wenzake wakiwamo wanajeshi kwa kuwatetea katika maeneo mbalimbali pale alipopata nafasi hiyo.

Kwa njia hiyo wengi wapandishwa ngazi za uongozi kupitia uteuzi uliosimamiwa na Brigedia Jenerali Moses Nnauye.

Alikuwa na kipaji cha ajabu cha kuhamasisha vijana katika makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), wakati mmoja mwaka 1976 aliwahi kupita kambi ya Makutupora JKT iliyoko Dodoma na kuwahamasisha vijana waongeze uzalishaji wa zabibu.

Mwitikio huo kwa vijana uliitikiwa vyema na mwaka huo walizalisha zabibu nyingi zilizomfanya mkuu wa kambi hiyo, Brigedia Jenerali Adamu Mwakanjuki (marehemu) kupata heshima kubwa kwa mafanikio.

Itakumbukwa Brigedia Jenerali Mwakanjuki alikuwa kada wa CCM, ambaye uzalishaji wa zabibu ulimpaa heshima akionekana mchapakazi mahiri.

Brigedia Jenerali Nnauye alikuwa mnadharia (theoretician) na pia mchambuzi (analyst) mahiri wa masuala ya siasa, alijikita zaidi katika mambo ya maendeleo ya Watanzania.

Mmoja wa wanasiasa wakongwe anayezungumza habari zake anasema kwa mara ya mwisho mwaka 2000 alikutana na Brigedia Nnauye huko Arusha, akiwa katika ziara ya kuimarisha matawi ya CCM.

Anasema, Brigedia Jenerali Nnauye, licha ya kuonekana kama amedhoofu, kwa wachapa kazi kama yeye ugonjwa haikuwa sababu ya kupumzika.

Anahusisha hali kama hiyo kama ilivyokuwa kwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, ambaye mwaka 1999 alipokuwa katika mazungumzo ya amani ya Burundi huko Arusha, madaktari wake walimshinikiza akubali kwenda Uingereza kwa matibabu.

Brigedia Jenerali Moses Nnauye alifariki dunia katika Hospitali ya Muhimbili jijini Dar es Salaam Desemba 6, 2001 baada ya kuugua.

Baada ya kifo chake, viongozi waandamizi wa serikali na CCM mwaka 2021 waliamua kumuenzi kwa kumbukizi ya miaka 20 ya kifo chake.

# Migogoro ya uongozi ndani ya vyama vya siasa, vingine vilivyoishiwa pumzi

**Na Sabato Kasika**

MWAKA 1992, Tanzania ilirejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa na kuwapa fursa wapenda mageuzi kuanzisha vyama ambavyo baadhi vilishiriki uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo mwaka 1995.

NCCR- Mageuzi, Chama cha Wananchi CUF na UDP ni baadhi ya vyama vilivyoweka wagombea urais, ubunge na udiwani.

NCCR-Mageuzi ni viongozi mwa vilivyong'ara kikipata wabunge na madiwani wengi, kikivipiku vingine vingi huku CCM kikiwa kinara, baada ya kushinda urais, wabunge na madiwani wengi zaidi.

NCCR- Mageuzi ilifurukuta katika uchaguzi huu ikiwa imevuka mgogoro wa kiuongozi ambao ulisababisha baadhi ya wanachama kujiengua na kuanzisha chama kingine cha siasa.

Vuguvugu la mageuzi ya kisiasa lilianza 1989, kwa mijadala iliohitimishwa kwa kongamano la mageuzi ya kisiasa na kikatiba Dar es Salaam, mwaka 1991.

Mojawapo ya maazimio ya kongamano yalikuwa kuundwa Kamati ya Kuratibu Mageuzi ya Kisiasa na Kikatiba (National Committee for Constitutional Reform-NCCR). Kwa upande wa Zanzibar kamati iliitwa KAMAHURU, ikongozwa na Shaaban Mloo, (sasa marehemu).

### MGOGORO WAIBUKA

Wakiwa katika harakati za mageuzi, kamati hiyo ilikumbwa na mgogoro wa kiungozi baada ya Mwenyekiti Chifu Fundikira, kusafiri bila taarifa kwenda nje ya nchi kuhudhuria kongamano la kimataifa la demokrasia na siasa za vyama vingi.

Baada ya kurejea, Katibu Mkuu NCCR, wakili Mabere Marando akiungwa mkono na viongozi wenzake na vijana, walitaka kumwajibisha mwenyekiti wao, wakihoji kwa nini aliondoka bila kuaga.

Hata hivyo, kabla ya kuchukuliwa hatua, aliamua kujiondoa na kuanzisha chama chake kitwacho Union for Multiparty Democracy (UMD), huku baadhi ya wazee wakiwamo Balozi Kassanga Tumbo na Kasela Bantu wakimfuata, mwaka 1991 chama kikiweka makao makuu Magomeni Mikumi nyumbani kwa Chifu Fundikira, ukawa ni mwanzo wa kumomonyoka kwa kamati ya NCCR.

Kamati hiyo iliendelea kumomonyoka kwani baadaye James Mapalala, akajiengua na kuanzisha Chama cha Wananchi (CCW), akiwa ni Mwenyekiti na Katibu Mkuu akiwa Dk. Alec Chemponda.

Mbali na Mapalala, mjumbe mwingine Mchungaji Christopher Mtikila, aliondoka NCCR pamoja na Mwinjilisti Kamala Kasupa na Mahimbo Kaoneka, wakaanzisha Chama Cha Demockasia (CCD), Kaoneka akiwa Mwenyekiti.

Kasupa alikuwa Katibu Mkuu na Mchungaji Mtikila akiwa mlezi, ambapo viongozi hao wa CCD, lakini nao walisambaratika huku Mchungaji Mtikila akiungwa mkono na wafuasi wake alitangaza kubadilisha CCD kutoka Kiswahili kuwa Kiingereza na kuwa Democratic Party (DP), akiwaachia Kusupa na Kaoneka CCD.




Mchungaji Christopher Mtikila katika harakati zake za kisiasa kwenye viwanja vya Jangwani Dar es Salaam, enzi ya uhai wake.

Ni wakati huo ambao pia KAMAHURU walijitenga na NCCR na kuungana na CCW na kuunda The Civic United Front (CUF). Mwenyekiti akiwa James Mapalala na Katibu Mkuu Seif Sharif Hamad.

### MGOGORO CUF

Mwaka 1993 halmashauri kuu za vyama vyote zilipokutana na kuanzisha nguvu ya pamoja mwaka, Mapalala aliteuliwa kuwa mwenyekiti wa kwanza wa CUF Bara na alianza rasmi kazi ya kukitangaza chama Bara na visiwani.

Lakini mwaka uliofuata, ndio ulikua mwisho wa Mapalala baada ya viongozi wa CUF Zanzibar kuibua hoja kuwa ni msaliti, kwa madai kwamba anafanya kazi mbili ni mwenyekiti CUF, lakini anatumika na CCM.

Alituhumiwa kuchana bendera ya CUF mara kwa mara ikionyesha hana uzalendo wa chama na hafai kuwa mwenyekiti, ambapo alijitetea kwa kusema ufadhili wa CUF ndio chanzo cha mgogoro.

Alidai kulikuwa na fununu za kuwapo wafadhili kutoka nchi za Kiarabu, kwamba waligoma kutoa msaada utakaosimamiwa na kafiri na kwamba ndio ulikuwa chanzo cha mgogoro kati yake na viongozi wa CUF Zanzibar.

Mgogoro huo ulifika kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, George Liundi ambaye alitupilia mbali hoja za Mapalala, ukawa mwisho wake ndani ya CUF.

### NCCR WAJIPANGA

Mwaka 1992 waliosalia ndani ya kamati hiyo, walikubaliana kubadilisha NCCR kutoka Kamati ya Mageuzi ya Katiba na kuwa chama cha siasa lakini kwa kubakiza jila la NCCR na kisha kuongeza mbele yake maneno Mageuzi.

Kutokana na mabadiliko hayo, jina likawa The National Convention for Construction and Reform (NCCR-Mageuzi), ingawa wakati wa mashauriano, wajumbe walipendekeza jina liwe ni Chama Cha Demokrasia na Maendeleo.

Baada ya mabadiliko hayo, Marando akiwa Mwenyekiti, Prince Bagenda Katibu Mkuu, Mashaka Chimoto Katibu wa Itikadi na Uenezi, Ndimara Tegambwage Katibu wa Habari na Uhamasishaji, chama kilienea nchi nzima.

Chama hicho kilibeba wanafunzi na wahadhiri wa vyuo vikuu nchini, kiliunda na kuimarisha kamati za mikoa yote nchini, kikapata misaada ya hali na mali kutoka kwa viongozi na watu mbalimbali.

Kufikia mwaka 1995, kilikuwa tayari kimeshajiimarisha na kilikuja kuongezewa nguvu na Augustine Mrema aliyehama kutoka CCM na kupewa nafasi ya mwenyekiti wa taifa na kuwania urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huo.

### WAVUTANA TENA

Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 mgogoro wa kiungozi uliibuka tena ndani ya Chama cha NCCR-Mageuzi ukiwa kati ya Mrema na Marando ambao Mrema alinusurika kuumizwa.

Ilikuwa ni mwaka 1997, ulipoibuka mgogoro huo na kusababisha Mrema kujiondoa na kujiunga na Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), na tangu wakati huo, NCCR- Mageuzi kimeendelea kudorora hadi leo.

Kule ambako Mrema aliamia, nako kulizuka mgogoro na kusababisha mwasisi wa chama hicho Leo Lwekamwa na baadhi ya watu wa karibu wa Mrema akiwamo Hamad Tao kukimbilia kwingine na kukiacha hakina nguvu.

Hali kama hiyo ndio iliopo ndani ya NCCR- Mageuzi ambako Mei mwaka huu kuliibuka tena mgogoro wa kiungozi uliohitimishwa kwa kumfukuza uanachama mwenyekiti wake James Mbatia na baadhi ya wanachama.

Kwa ujumla ni kwamba, ndani ya vyama vya siasa karibu vyote kumewapo na migogoro na kiuongozi ambayo inavitafuna na kusababisha vingine kukosa nguvu au kujipanga upya na kuendelea na kazi.

Migogoro hiyo haikuacha salama chama cha UDP ambacho kiliwahi kuwa na wabunge wanne, ambapo mwaka 1994 na 2000, kilikumbwa na mgogoro baada ya mwenyekiti wake, John Cheyo kupinduliwa mkutanoni.

Nafasi yake ilichukuliwa na Nzugule Amani Jidulamabambasi, ambaye hata hivyo, hakudumu madarakani kwa muda mrefu, kutokana na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutomtambua.

CHADEMA nao haijabaki salama katika migogoro hiyo, kwani mwaka 2013 iliwavua uongozi kina Zitto, Profesa Kitila na Samson Mwigamba waodaiwa kuandaa waraka wa kupindua uongozi wa Freeman Mbowe.

Wakati wa harakati za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, aliyewahi kuwa Waziri Mkuu, Edward Lowasa alijiondoa CCM na kundi kubwa la wanachama na kwenda CHADEMA na kupitishwa kuwania nafasi ya urais.

Mwanzoni mwa mwaka 2020 aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, alifukuzwa uanachama wa CCM kwa kwenda kinyume cha utaratibu wa chama hicho.

Hata hivyo, mwenyewe aliibuka na kudai kuwa sababu ya kufanyika kwa uamuzi huo wa kumtimua katika chama ilitokana na dhamira yake ya kutaka kuwania urais kwenye uchaguzi wa mwaka 2020.

### ATHARI YA MIGOGORO

Migogoro ndani ya vyama vya siasa inaweza kuwa na athari nzuri ya kuchochea ukuaji wa demokrasia ndani ya vyama hivyo au kusababisha vikayumba iwapo wanachama watanyimwa uhuru wa kutoa maoni yao.

Katika mfumo wa vyama vingi hasa vyama vikubwa vyenye ushawishi kwa jamii, migongano na malumbano ya ndani kwa ndani ni jambo la kawaida, na hujidhihirisha kwa kuibuka vikundi vya wanachama wachache.

Vyama vikubwa kama CCM na CHADEMA, migogoro yake ya ndani imekuwa na faida katika ustawi wa demokrasia hasa pale wanachama wanapowajibishwa kulinga na makosa yao, kisha chama kujipanga upya.

Ni muhimu vyama vikongwe vikumbwe na migogoro, kwani haiepukiki kutokana na ukweli kwamba, wanachama hawawezi kuwa na mawazo ya kufanana.

Hali hiyo imekuwa ikitafsiriwa kuwa ni mapinduzi dhidi ya mwenyekiti na uongozi wake, na kwa kuwa ila mtu anapenda kuendelea kuongoza na kuwa na ushawishi katika chama, kila jitihada hufanyika kuwasuluhisha wenye mawazo mbadala pasipo kuangalia madhara kwa chama.

Migogoro kama hiyo inaviathiri vyama vingi na kuvifanya vipoteze ushawishi mbele ya umma, na pia migogoro hiyo imekuwa ni faida kwa wanaofukuzwa hata kwa wananchi wasio na vyama ambao viongozi wanaowaongoza katika jamii, wengi wao wanatokea kwenye vyama vya siasa.



James Mapalala (kulia), akisalimiana na aliyekuwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba, Samuel Sitta (wote ni marehemu).

# Charlene Ruto anayelandana na Ivanca Trump wa Marekani

## • Bila wadhifa rasmi yumo ziarani kitaifa, kimataifa
## • Inakuwaje, mitandao ya kijamii Kenya yahoji?

**Na Gaudensia Mngumi**

CHARLENE Ruto ni binti wa Rais wa Kenya William Ruto, ambaye licha ya nafasi yake serikalini kutokufafanuliwa na kufahamika rasmi na kwa uwazi, amekuwa akishiriki mambo mbalimbali ya kiserikali zikiwamo safari za kutembelea nchi za kigeni ikiwamo Morocco.

Hayo yanajiri miezi kadhaa tangu baba yake achaguliwe kuwa Rais wa Kenya na kula kiapo Septemba mwaka huu vyombo vya habari vya nchini humo, vinaripoti.

Vinasema kuwa binti Ruto, amekutana na maofisa kadhaa wa kaunti kote nchini Kenya pamoja na mawaziri wa mataifa ya kigeni na pia kuzuru baadhi ya nchi za nje.

Charlene ambaye ni mtoto wa pili wa Rais Ruto, na anayejiita 'binti wa kwanza wa Kenya', (first daughter), hata hivyo mitandao ya kijamii haijakaa kimya inauliza kwa nini Charlene Ruto anaonekana kukutana na mawaziri wengi wa serikali na kuchukua safari za kiserikali za nje ya nchi? Ni kwa gharama za nani?.

Wasiwasi kama huo ulizuka wakati Rais wa zamani wa Marekani Donald Trump, alipochaguliwa kwa mara ya kwanza kuiongoza nchi na binti yake Ivanca Trump, akahudhuria mikutano na baba yake kama mshauri asiye rasmi.

Trump baadaye alimteua Ivanca katika jukumu rasmi la serikali la kuwa mshauri wake.


Baadhi ya Wakenya sasa wanauliza, ni nani anayesimamia masuala ya mikutano yote hiyo, na je wako katika nafasi rasmi?

Mnamo mapema mwezi huu Charlene Ruto anazungumzia taarifa za kukutana na Waziri wa Vijana wa Morocco, Mohammed Mehdi, kwa mazungumzo ya kiserikali na kubadilishana uzoefu utakaosaidia katika kuunda na kuandaa miradi ya maendeleo ya vijana kwa mataifa yote mawili.

Wakati hayo yakitokea baadhi ya Wakenya wanauliza, ni nani anayesimamia masuala ya mikutano yote hiyo na gharama za safari anazilipa nani, na kama binti huyo yuko katika nafasi rasmi?

Akiwa Morocco anaandika ujumbe kwenye jukwaa la "Kupitia Pan African Congress of Kenya @PanAfricanKe, akisema "Tunalenga kuongeza idadi ya ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Kenya huko Morocco maeneo ambayo tunayapa umuhimu ni kilimo na teknolojia," anasema kwenye ujumbe wa tweeter.

Charlene, ambaye alisafiri kwenda Morocco mapema mwezi huu, anaonekana akitembelea na kufurahia utamaduni, sanaa na miundombinu ya nchi hiyo akichapisha taarifa za mara kwa mara kwenye akaunti zake za mitandao ya kijamii.



Rais Ruto na familia yake. **PCHA ZOTE: DAILY NATION**

Zaidi ya hayo, alitetea mtindo wa kujenga uchumi wa Baba Ruro kwa utaratibu wa kuanzia chini kwenda juu akitoa mada nzuri ambao uliwaacha wasikilizaji wake mshangao mkubwa.

Charlene anasema mtindo huo wa kujenga uchumi ni muhimu katika kutengeneza fursa bora kwa vijana katika bara la Afrika na kuongeza kuwa ni mbinu mujarabu katika kufungua sera ya biashara huria ya Afrika ambayo viongozi wengi wamehangaika nayo kwa miaka mingi ili kufikia ndoto hiyo.

"Kurejesha viwango vya juu vya uhamasishaji jamii barani Afrika kuipqa sura mpya itakuwa miongoni mwa changamoto muhimu za kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kadiri tunavyosubiri kushughulikia suala hilo, ndivyo siasa zetu zitakavyozidi kuwa na misukosuko," anasema Charlote.

### KABLA YA MOROCCO

Kabla ya kuondoka kuelekea Morocco, Charlene alikuwa amezuru kaunti za Embu, Kirinyaga, Isiolo, Kitui na Tharaka-Nithi katika muda wa wiki moja, alikutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa kaunti na wawakilishi wao.

Huko Isiolo, binti Ruto alifanya mazungumzo na Naibu Gavana James Lowasa, kuhusu kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.



Charlene Ruto

Anaahidi kuanza jukumu la kupanda miti mwezi ujao, akitekeleza kile ambacho Dk Ruto amekuwa akitetea wakati wote.

Bintiye Rais Ruto anawaacha watu ndimi zikitafuta la kusema na kujadili mambo mengi kuhusu kufuatia mikutano yake hiyo na maofisa wakuu wa kaunti kadhaa za Kenya.

Charlene Ruto amefanya mazungumzo na wafanyakazi wakuu wa kaunti za Embu, Kirinyaga, Isiolo na Kitui, na kuzua gumzo kwenye mitandao ya kijamii huku Wakenya wakionyesha udadisi kuhusu nia ya ziara hizo.

Vyanzo vya habari katika bunge hilo vinasema kuwa Charlene alikutana na Spika John Mbabu na kuwa na majadiliano marefu kuhusu biashara.

Aidha kuna maelezo kuwa anazunguka kaunti mbalimbali kutafuta biashara katika Hoteli ya Weston ambayo inahusishwa na babake, kinadai chanzo ambacho hakikuwa tayari kunukuliwa.

Chanzo hicho kinaongeza kuwa pia anatembelea uongozi wa zamani wa bunge hilo bila kutoa taarifa zaidi.

Katika ziara hizo Charlene anamtembelea Naibu Gavana wa Isiolo, James Lowasa katika ofisi yake iliyoko mji wa Isiolo na kushiriki mijadala kuhusu kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na ongezeko la joto duniani.

Anasema ni katika kutimiza kile kinachoonekana kuwa nia yake kuu kutamani kuona kaunti zikikua kwa manufaa ya Wakenya wote na kwamba maendeleo ya kaunti ni maendeleo ya Kenya yote.

### AFANANISHWA NA IVANCA

Baadhi ya Wakenya wanamfananisha na Ivanca Trump, aliyekuwa mshauri mkuu katika utawala wa Rais Donald Trump, akimuwakilisha kwenye masuala mbalimbali ya kimataifa.

Aidha, alikuwa mkurugenzi wa Ofisi ya Mipango ya Kiuchumi na Ujasiriamali.

***CHANZO: DAILY NATION.***

# Meja Ngwegwe Mtanzania anayetumika ndani ya Jeshi la Marines la Marekani



Meja Khalid Ngwegwe: **PICHA :FAMILIA.**

**Na Beatrice Moses**

JINA lake ni Khalid Ngwegwe, aliyezaliwa Aprili 1993 katika hospitali ya Amana Dar es Salaam, kisha kusoma shule za msingi na sekondari Dar, leo ni meja katika Jeshi la Marekani.

Anafanyakazi kwenye vikosi vya US Marine linaolotoa huduma ya jeshi la nchi kavu na la maji linalohusika na kuendesha shughuli za uharaka na za dharura .

Anapozungumza na Nipashe hivi karibuni, anasema safari ya kuingia Marekani ilianza mwaka 1992 ni baada ya baba yake kuhamia Amerika pamoja na familia yao, hata hivyo hakusema alikokuwa akifanyakazi. Uhamisho huo ulimpa visa 'special immigrant visa' na walipowasili walipatiwa hati ya ruhusu maalumu ya kuwa raia wan chi hiyo iitwayo 'green card'.

Anasema alipomaliza kidato cha nne sikuendelea na kidato cha tano kwa sababu baba yake alipangiwa kuhamia Marekani na kuanzia Januari 2012, wakati huo akiwa na miaka 19, walikuwa wakiishi katika jiji Washington DC, ndipo alipojiunga na Chuo cha Montgomery kusomea masuala ya teknolojia ya mawasiliano ya habari (IT). Japo pia alikuwa na kazi ya kuuza duka.

Anaeleza kuwa aliingia kazini kuanzia saa 6:00 na kutoka saa 1:00 asubuhi na baada ya mapumziko, saa10 jioni anaingia darasani hadi saa mbili usiku.

Katika ajira hiyo ambayo anasema ilimnyima muda wa kulala usiku, lakini pia akipata saa tisa za kumpumzika, Meja Ngwegwe anakiri kuwa ilimshinda na baada ya miezi sita, akaiacha, lakini 2013 akapata mwajiri mwingine aliyemtaja kwa jina la Subway inayoiuza vyakula.

**ALIINGIAJE JESHINI?**

Hapo Meja Ngwegwe, anasimulia mchakato ulivyokuwa akisema ilikuwa 2015 alipotokea mteja mwanajeshi mwanamama wa Jeshi la Anga la Marekani, ambaye alivutiwa na mwonekano wa Ngwegwe, akisema mwili wake umejengeka kimazoezi, unaofaa kwa utumishi wa jeshi.

Kwa mujibu wa Ngwegwe, askari huyo alimdadisi na kumuuliza kama yupo tayari kujiunga na Jeshi la Marekani, akamuachia kadi ya mawasiliano, akisimulia kuwa baada ya kupokea mwaliko huo, alikuwa na hofu ya utumishi huo kwa kile alichotafsiri akiamini kuwa ajira ya kijeshi ni kujiweka jirani na kifo.

"Hivyo baaada ya kuchukua kadi yake, nikarudi nyumbani, nikafanya utafiti kuhusu jeshi hilo kwamba kuna la anga, la majini, la ardhini na marine wanaofafanya vyote," anaeleza na kuendelea:

"Siku tatu baadaye nikaenda ofisini kwake, lakini sikumkuta. Nikagonga sana mlango, hakuwepo! Siku ya pili, ya tatu zote hakuwepo, kwa hiyo nikajiapia 'kesho nikirudi kama hayupo basi sio riziki yangu, maana hata huko jeshini kwenyewe haikuwa ndoto yangu" anaeleza na kukumbusha kuwa hata siku ya nne hakukutana naye.

Anasema alikata tamaa akaondoka na alivyokuwa anatoka, akakutana na askari mwingine akiwa na sare za jeshi akamsalimia na akamuuliza '"vipi kwema? Mbona nakuona unakuja sana unahitaji msaada?"

> "Tulikaa miezi sita baada ya kuhitimu ndipo kila mtu anapelekwa chuo kusomea kazi ya taaluma, nikapelekwa US Army Logistics University iliyoko Fort Lee Virginia na nikaenda kumalizia masomo na kupata shahada baada ya hapo nikaanza kazi rasmi ya jeshini," anasema.

Kijana huyo anasema akajieleza kuhusu kilichomfikisha hapo na ndipo akajulishwa kuwa mwenyeji wake amepata msiba wa baba yake, amesafiri, akitarajiwa angerejea ofisini mwezi unaofuata.

"Hapo ndipo akaniuliza 'kwani unataka kujiunga na jeshi la anga Airforce?' Nikamjibu 'mi nataka nipate kazi jeshini ambayo hata nikitoka huko niendelee na kazi hiyo' nikiwa na maana, nataka jeshi linipe kazi ambazo zipo uraini. Pia, akasema 'una dakika 15? Nikamjibu ndipo akanipeleka ofisini kwake," anasema.

Anaeleza kuwa akaambiwa kama anataka kazi, nafasi zote walizonazo jeshi la anga hata marines wanazo, kazi zote walizonazo jeshi la maji zipo pia kwa hiyo kazi sio tatizo atapata, akasema anataka na anapenda kuwa marine akiambiwa kuwa jeshi haliokoti watu tu, ni lazima uwe timamu, maridadi, mwenye kijiheshimu na msimamo.

Ngwegwe anasema mwanajeshi huyo alimwambia kaulimbiu ya marines ni 'semper fidelis' , maneno ya Kilatini yanayoamanisha uaminifu daima, hivyo huchaguliwa watu wachache, akifanikiwa kufaulu kujiunga ataona mafanikio.

"Aliniambia kama unaona hutoyaweza niliokuambia mlango ule pale unaweza kwenda jinsi jamaa alavyo kuwa anajieleza kwa kujiamini ilikua tofauti na matawi mengine ya jeshi pia yeye hakuwa ananibembeleza kwa hiyo nikapenda," anasema.

Anasema baada ya kutafakari na kuelekezwa faida ya kujiunga na jeshi hilo akakubali kujisajili , hivyo akaanza mchakato wa kuingia kwenye jeshi hilo, akapimwa afya kwa vipimo maalum akaonekana yupo sawa.

"Baada ya vipimo hivyo nikapelekwa kwenye kituo kinachoitwa MEPS kirefu ni Military Entry Processing Station ambako kule ndiko unafanya mtihani mkuu wa kuingia jeshini unaoitwa ASVAB au Armed Services Vocational Aptitude Battery," anasema.

Anaelezea kuwa mtihani huo ni mmoja lakini una masomo ya hisabati, Kiingereza , Fizikia, Kemia, baiolojia, historia, jiografia, masuala ya ufahamu wa mitambo, uwezo wa akili- IQ na civics ambao unatakiwa kupata alama kuanzia 50 chini ya 99 ili kufuzu.

Anasema kuwa kwa utaratibu uliowekwa ilikuwa kadri unavyopata alama ya juu pia ndio unapata nafasi nzuri ya kuchaguliwa kwenye kazi za kitaaluma unazofanya ukiwa ndani ya jeshi, hivyo yeye alipata 95 kwa hiyo akawa na nafasi ya kuchaguliwa kwenye nafasi nzuri.

Baada ya mwezi mmoja akapelekwa Parris Island South Carolina huko ndiko kuna kituo cha mafunzo ya marine na akaanza masomo akitaja kuwapo na changamoto nyingi, kwani yalikuwa magumu mno ukitakiwa kufaulu mazoezi ya utimamu wa mwili 'physical fitness' na taalum kwa hiyo asubuhi hadi mchana ni mazoezi ya mwili kisha jioni walikuwa wanaingia darasani kwa masomo ya kitaaluma.

Anatoa maelezo ya mafunzo aliyopata, ikiwamo kuamka saa 8 usiku ukiwa umebeba mabegi yenye kila kitu chako ndani yake ambavyo vitakidhi siku tatu na walitembea maili sita hadi au kilometa 12 kwende maporini huko wanakula chakula kidogo sana kama biskuti tena alihakikisha hakuna kulala ni saa mbili pekee.

"Tulikaa miezi sita baada ya kuhitimu ndipo kila mtu anapelekwa chuo kusomea kazi ya taaluma, nikapelekwa US Army Logistics University iliyoko Fort Lee Virginia na nikaenda kumalizia masomo na kupata shahada baada ya hapo nikaanza kazi rasmi ya jeshini," anasema.

Mkuu wa Sekondari ya Agape, Dar es Salaam, Robson Fungo akizungumzia kuhusu Ngwegwe ambaye alisoma shule hapo, anasema alikuwa ni miongoni mwa wanafunzi wenye nidhamu na ari ya kujituma.

"Pamoja na kwamba alikuwa anatoka kwenye familia ya watu wenye kipato kikubwa hakuwa na kiburi alishiriki kazi zote , kama kulima bustani tena alihamia shuleni hapo kidato cha pili. Alijituma ipasavyo katika taaluma na shughuli nyingine zote shule."

Mwaka 2001 alianza darasa la kwanza Shule ya St'Marys Mbagala hadi 2006, walimu wakaamua asisome darasa la saba 2007, akarushwa na kuingia kidato cha kwanza kwenye Sekondari ya St.Matthew, baada ya mwaka mmoja alihamishiwa Agape kulimaliza kidato cha nne mwaka

JUKWAA LA VIONGOZI

NYANZOBE MAKWAIYA

# Maajabu ya binti aliyeanza kuwa kiongozi akiwa na miaka mitatu

**Na Salome Kitomari**



Ni ngumu kuona mwanafunzi wa darasa la tatu mwenye umri wa miaka tisa anaongoza wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la saba, lakini iliwezekana kwa Nyanzobe Makwaiya (22), ambaye bado anaendelea kuonyesha uwezo wake wa kuongoza katika kila eneo analokuwepo.

Nyanzobe anasoma Shahada ya Kwanza ya Usimamizi wa Mazingira, mwaka wa tatu katika Chuo Kikuu cha Ardhi, Dar es Salaam, ni mtoto pekee wa Cecilia Makwaia, amelelewa na mama pekee hadi sasa, ambaye amekuwa kiongozi wake kumjenga awe alivyo sasa.

Safari ya uongozi ilianza katika Shule ya Msingi St. Columbus akiwa darasa la tatu, ambapo mwalimu wa darasa alimweleza Mwalimu Mkuu kuwa kuna mwanafunzi (Nyanzobe) ana uwezo wa kuongoza.

"Nilikuwa nikiona wanapiga kelele hata kama ni mstarini au darasani nawafuata nawaambia achene kelele kwa sauti ya ukali, wakawa wananisikiliza, darasani kwangu nikiona wanapiga kelele naandika majina, wakati huo sio kiongozi alafu nayapeleka kwa mwalimu, ndipo nilionekana naweza kuongoza, nilianza kuhudumu kwa kuongoza wakubwa na wadogo, nikachaguliwa kuwa kiranja mdogo kuliko wote,"anasema.

Anasema aliweka historia shuleni humo kuwa ni kiongozi mwenye umri mdogo na hadi anamaliza la saba aliongoza mara mbili, anaendelea na masomo ya sekondari na akiwa kidato cha tatu aligombea nafasi ya dada mkuu, akaipata akisema hakuwa na nia ya kuongoza ila mwalimu wa jiografia alimuita akamuuliza amechukua fomu aliposema hapana, akamwambia lazima agombee nafasi hiyo lakini bado alisita.

"Walichukua fomu wakajaza wakarudisha nashangaa majina yalivyotangazwa ili kupigiwa kura langu likawepo, walivyopiga kura nikatangazwa dada mkuu. Sikuamini kumbe nina watu wananiamini, wanaona uwezo wangu ,"anafafanua.

Aidha, anasema akiwa kidato cha tano alidhamiria kuchukua fomu ya kuwania urais wa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita na kujaza fomu akafanyiwa mahojiano na kura zilipopigwa alishika nafasi ya pili, akifanya kazi na rais pamoja na mawaziri wote na alipohitimu kidato cha sita alipewa zawadi ya kiongozi bora.

**CHUO CHA ARDHI**

Nyanzobe anajiunga na Chuo Kikuu cha Ardhi, Dar es Salaam na kuendelea na uongozi akigombea ubunge jimbo la darasani na kushinda akishika usukani tangu 2020 hadi leo na akiwa mwaka wa pili akateuliwa na Rais wa Serikali ya Wanafunzi, kuwa Waziri wa Katiba, Sheria na Utawala Bora akivaa kofia mbili.

Hajaishia hapo Aprili mwaka 2021 akagombea nafasi ya Makamu wa Rais anasema "Nikiwa mwanafunzi wa mwaka wa pili ninayesoma kozi ya miaka minne, na huwa kuna mazoea nafasi kama hizo ikiwamo ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Katibu Mkuu huwa zinashikiliwa na wanafunzi wa mwaka wa tatu na nne, nilionekana sifahamu mambo mengi na ni mgeni shuleni."Nilipata maswali mengi sana, wapo walioniuliza unajiamini nini? Kwanini uchukue nafasi hii ukiwa mwaka wa pili, wengine walinikalisha wakasema huwezi usichukue hii nafasi, gombea kitu kingine kisicho na ushindani, sikukata tamaa nilishikilia msimamo wangu,"anasema.

"Nilipiga moyo konde kwamba hata kama sitapata watu, lakini nitaingia kwenye rekodi kuwa nimejaribu, niliwaeleza wanafunzi wa jimbo langu ambao walisema wataniunga mkono, walinisaidia kutafuta watu wa kuchukua fomu za kujaza,"anasema.

Alizijaza fomu na kunadi sera na kwamba wagombea walikuwa wanane na majina yaliyopita bungeni ni matatu "Niliingia bungeni kwa kujiamini nikanadi sera zangu, baadaye wabunge wakapiga kura baadaye matokeo yalitoka nikawa miongoni mwao."

Anasema walipewa siku tatu za kampeni: "Ilikuwa ngumu na uzoefu mkubwa sana maana nilifanya kampeni darasa hadi darasa, chumba hadi chumba, wakati mwingine unakwenda usiku kuzungumza na watu, unatakiwa uwe na fedha na kila anayeungana nawe ana matarajio makubwa. Kura zilipigwa ila sikushinda nafasi ya Makamu wa rais."

Katika kikao cha kwanza cha bunge rais anatakiwa amteue Waziri Mkuu, "Siku moja nikiwa kikaoni spika aliingia na bahasha yenye jina la anayependekezwa apigiwe kura, katika hali ya kushangaza na isiyoweza kuelezeka jina langu lilitajwa kwamba linatakiwa kupigiwa kura kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya 15 ya Wanafunzi, sikuwa nimetarajia, sikuwa nimeongea naye, sikuwa nimeahidiwa lolote."

Anasema rais tulifanya naye kampeni pamoja mimi nikigombea makamu, lakini katika mazungumzo na makamu wa rais walipeleka jina bungeni lipigiwe kura ya ndio au sio, na kwamba alipigiwa kura zote na alianza kazi baada ya kumaliza kiapo chake.

"Nilianza kazi na tulipata changamoto rais wa serikali ya 15 aliahirisha masomo ikabidi makamu wa rais akaapishwa kuwa rais ambaye kwa mujibu wa sheria zao anafanya uteuzi upya wa mawaziri, waziri mkuu na viongozi wengine na inakuwa serikali ya 16, niliteuliwa tena kuwa waziri mkuu.

"Ukiangalia mimi Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi Chuo Kikuu cha Ardhi, sikuwa mbali sana na namna Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, alivyoshikilia nafasi hiyo, kwamba aliongoza wakati wa serikali ya awamu ya tano na sasa yuko serikali ya awamu ya sita,"anasema.

Anasema kwa kushika nafasi hiyo amekuwa waziri mkuu wa pili wa kike tangu chuo kikuu kianzishwe miaka 15 iliyopita, na kwamba serikali ya 16 ndio walipata rais mwanamke.

"Hii inaonyesha bado tupo nyuma kwenye uongozi wa wanawake, ukiwa kijana ni changamoto lakini ukiwa mwanamke ndio changamoto mara dufu, bado nitaendelea na jitihada za kuongoza kwa kuwa naamini kuna kitu Mungu amekiweka ndani yangu,"anasema.

Aidha, anasema Julai mwaka huu alichaguliwa Katibu wa Lotary Klabu of Kijiji , tunafanya masuala ya maendeleo na kutoa huduma kwa jamii, ili kuisaidia jamii katika nyanja mbalimbali, pia ni Mwanaharakati wa maendeleo endelevu ya jamii (SDGs).

**KWANINI KIONGOZI**

Anapenda kuwa kiongozi kwa sababu anapata msukumo ndani yake kugombea nafasi mbalimbali na msukumo wa watu wanaomfahamu na kujua uwezo wake ambao wamemshawishi kugombea wakimuaminisha kuwa anaweza.

Anasema anapenda kufanya vitu kwa utaratibu na anapoona kitu kinafanyika bila utaratibu sahihi au halijafanyika vyema anaona anaweza kufanya ndio maana hushika nafasi ya uongozi.

**MAFANIKIO**

"Mafanikio ninayojivunia kwa nafasi za uongozi ni kualikwa kama mgeni rasmi kwenye mafunzo ya jinsia ya uongozi wa kifeminia kwa viongozi wanawake, kupewa heshima kubwa kama hii kwa wanawake kutoka vituo vya maarifa na taarifa na pia kujenga moyo wa uthubutu kama kugombea nafasi ya juu ya urais.

Aidha anataja jingine kuwa ni kupata nafasi nyingine nyingi za majukumu tofauti na ukiwa huna nafasi yoyote kwenye jamii, ndio maana amehudhuria mikutano na mafunzo mengi ya kumkuza kijamii na kiuongozi.

"Unajuana na watu wengi, unajua mambo mengi, Oktoba mwaka huu nilipata safari kushiriki jumuiko la vyuo vikuu vya Afrika Mashariki, iliyogharamiwa na chuo, ni fursa kubwa ya kujifunza zaidi "anasema.

"Fursa nyingine unapokuwa kiongozi unatoka kwenye eneo ulilozoea na kwenda kwenye mazingira tofauti au kazi tofauti, unalazimika kujifunza. Sikufikiria kwamba kuna siku nitapiga kampeni usiku na mchana lakini kupitia uongozi nilifanya, niliweza kuongea haraka na watu kuwaeleza sera na wakanielewa hadi kunipigia kura,"anasema.

**CHANGAMOTO**

Nyanzobe anataja muda si rafiki kwa wanawake kwa kuwa wakati mwingine zinafanyika usiku wa manane, na hakuna kupumzika, gharama wapo wanaotaka fedha wakisema nakusaidia ili unisaidie, unaombwa maji inakulazimu kuingia mfukoni na unapogombea unatakiwa kuwa na uhakika wa mapato, akitaja pia uwezekano wa wagombea wengine kuanzisha siasa ya kukuchafua.

Anasema nyingine ni dharau kutoka kwa watu ambao hawaamini katika utendaji kazi, unaweza au kwa sababu ni mwanamke, bado jamii yetu haiamini kwa mwanamke, wanaleta dharau na wengine wanatoa lugha za kukatisha tamaa, hali inayokurudisha nyuma.

# Yaelekea Afrika Mashariki ni moja kwa bendera, wimbo na mikutano

## •Inakuwaje ni Kenya pekee inazima uasi wa M23 DRC?

**Na Anil Kija**



Askari wa Kenya wakiwasili DRC wiki iliyopita kukabili waasi wa M23. **PICHA: SPUTNIK NEWS**

VIKOSI vya Kenya vimeanza kuchukua nafasi katika uwanja wa mapambano jimbo la Kivu Kaskazini la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Wanajeshi hao wamepelekwa kama sehemu ya mkakati wa vikosi vya pamoja vya Jumuia ya Afrika Mashariki kuondoa uasi mashariki ya DRC, kunyang'anya silaha makundi yanayopigana kupinga serikali.

Inamaanisha kuwa kulihitajiwa mkakati wa pamoja kuzuia hisia kuwa ni jitihada ya nchi moja au nyingine kubeba mzigo wa amani nchini humo uwe wake.

Bado hakuna taarifa za kudhihirisha kuwa ziko nchi nyingine zimepeleka vikosi huko kuacha Kenya, licha ya kuwa hapakuwa na upinzani kuhusu ulazima wa kurudisha amani DRC kwa utengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa jumla, ambako ni mwanachama. EAC ina bendera na wimbo wa kuunganisha nchi hizi zote unaoimbwa na vikosi vya ulinzi na usalama kila mara kukiwa na matukio ya kiserikali ndani ya mataifa hayo kama ndani ya bunge na hata wakati wa ziara za wakuu wa nchi. Hivyo inaelekea ni muungano dhaifu.

Bado ni kitendawili vikosi hivyo vikishirikiana na vile vya DRC ambayo sasa kuna ishara kuwa vinajiamini zaidi, vinaweza kuondoa hatari kwa umoja wa nchi na usalama wa raia unaotokana na kundi la M23.

Kuna uwezekano wa mkakati wa kuunda nchi au kitaifa kidogo ndani ya DRC kinachotokana na waasi wa M23 ambacho kimsingi ni mwendelezo wa nchi ya Rwanda, kutumia migawanyiko ya ndani ya DRC, wakati huo wachunguzi wa habari wanasema yako makundi ya wanamgambo huria zaidi ya 1,000 nchini humo.

Hivyo uwepo wa M23 na jitihada za kikanda au muungano wa kimkakati kati ya DRC na Kenya ni hatua nyingine ya mabadiliko kwanza ndani ya DRC na halafu kwenye jumuiya ya EAC.

Ndani ya DRC migawanyiko ya kikabila na maslahi ya tabaka la kupora maliasili za nchi, wakiwamo na washirika maridhawa katika nchi jirani na hata za mbali kama kampuni moja muhimu ya madini ya Israel, makundi ya mamluki wa Kirusi Wagner, yamefikia hatua ya juu.

Inavyoelekea hakuna tena mazingira ya uporaji wa madini kimyakimya na kutumia kundi la wanamgambo waasi kulinda eneo hilo la Kivu Kaskazini, M23 wanaunda eneo zima wanalotaka kulitawala.

Mkakati wao ambao haukubaliki DRC ni kuunganishwa na jeshi la nchi hiyo na siyo kuweka silaha chini, jambo ambalo halikubaliki na limekataliwa huko Tigray Ethiopia hadi jimbo hilo likakubali kuweka silaha chini.

Ni pale wakazi wa jimbo hilo walipokuwa katika hatari halisi ya kuangamia, kwa njaa, kutofikiwa na misaada ya kibinadamu kutoka nje, na mwisho kufungwa kwa hospitali ya mji wa Mekele iliyokuwa ndiyo tumaini lao. Ilikuwa ni vita ya kufa na kupona wakati vita ya M23 na washirika wake ni ya kutumia fursa, kuibana serikali ya Congo.

Endapo madai ya waasi kuingizwa jeshini DRC yangekubaliwa, kinachotazamiwa ni kuwa baada ya muda wangekuwa wameteka kwa kiwango kikubwa njia za kimkakati za jeshi la kitaifa.

Wangekuwa na mazingira ya kutwaa madaraka ambayo kimsingi walikuwa nayo wakati Rais Kabila alipoingia madarakani kwa uvamizi uliosaidiwa na Uganda na Rwanda, mkakati ambao DRC inaufahamu bila mashaka yoyote. Ila kuna udhaifu wa DRC kusimamia jeshi la kitaifa kuwapa morali askari wake, na hilo sasa linaanza kufanyiwa kazi, wakisadiwa na vikosi kutoka Kenya na washirika wengine.

Kenya imekuwa katika mstari wa mbele kupambana na makundi ya kigaidi nchini Somalia na sasa DRC, na jitihada kubwa za kusuluhisha mizozo ya kina nchini Ethiopia na Sudan Kusini, ambayo hivi karibuni inaelekea kutulia.

Nje ya masuala ya morali kwa wanajeshi wa DRC, swali ambalo wachunguzi wanauliza ni kiwango gani cha vita ambacho Kenya imejiandaa kwa shughuli ya kukabiliana na M23?

> Kuna uwezekano wa mkakati wa kuunda nchi au kitaifa kidogo ndani ya DRC kinachotokana na waasi wa M23 ambacho kimsingi ni mwendelezo wa nchi ya Rwanda, kutumia migawanyiko ya ndani ya DRC, wakati huo wachunguzi wa habari wanasema yako makundi ya wanamgambo huria zaidi ya 1,000 nchini humo.

Picha za televisheni zilionyesha askari wenye bunduki nzito wakishuka, na kimsingi ndiyo silaha ya mapigano makali. Kuna mizinga na vifaru lakini hapo inaelekea M23 walikuwa na silaha zaidi, hasa vikosi vya Umoja wa Mataifa vikaacha kuwakabili. Kimsingi hata hivyo hawakupewa jukumu la kupigana nao.

Ukiangalia kilichotokea vitani Ukraine, ambako jeshi la nchi hiyo limewafagia wavamizi wa Russia kutoka sehemu kubwa ya eneo la mashariki waliloteka awali, unakuta kuwa mkakati wa msingi ulikuwa ni kuzuia vikosi vamizi kupata misaada kwa maana ya mahitaji ya kawaida kutoka upande wa pili, yaani wa uvamizi.

Hali ya vikosi vya uvamizi ikawa haivumiliki pale Ukraine ilipoanza kutumia mizinga ya kupiga mbali, kuvuruga misafara ya kupeleka shehena kwa vikosi vya mstari wa mbele. Hapo vilikosa mwelekeo vikahitaji kutawanyika, yaani kurudi.

Ni dhahiri kuwa Kenya itakuwa imepanga operesheni hii kwa uangalifu hasa tofauti kati yake na Somalia ambako vikosi vya nchi kadhaa havikuwa na uwezo wa kuzuia Al Shabaab kuchipua na kushamiri katika miji na vijiji vya Somalia, au kulinda mipaka dhidi ya magendo, uingizaji silaha au kutoza kodi za ki-sharia kwa wakazi wa maeneo yote hayo.

Wasingeweza pia kuzuia Al Shabaab kutwaa vijana vijijini na miji au viunga vya miji kuwapa vijisenti, sare na kuwaweka katika kambi zenye chakula, na kufidia familia zao kwa njia moja au nyingine endapo kijana atapoteza maisha, kulemaa. Ni mfumo wa jihadi.

Kinachotakiwa eneo la Kivu Kaskazini au kimsingi la Goma, Bunagana na miji ya ziada au wilaya ambako M23 wamejichimbia ni kutawanya vikosi vya Kenya na DRC kulikabili jeshi la magaidi kwa vifaru na silaha ndogo (kulinda njia kuu kwa vifaru, halafu njia ndogo kwa askari waliotawanywa na kujificha). Halafu mizinga na ndege zisizo na rubani, kama wanazo, vinatumika kuvuruga njia za kupitisha mahitaji kwa walio mstari wa mbele, kubamiza makambi muhimu ya kuhifadhi shehena zinazowezesha ugavi kwa vikosi tofauti vya M23. Pia njia kuu za kuingia au kutokea Rwanda zinaweza kuvunjwa kwa silaha nzito au kwa operesheni maalum kuzunguka vikosi vya adui. Katika uangalizi wa ziada, na kwa mustakabali wa kidiplomasia, Rwanda itakuwa haina uwezo wa kutumia ndege kupeleka mahitaji M23, hivyo hawatadumu kubaki vitani; wavue magwanda, wawe raia.

## Wakazi vijiji vilivyoondolewa Mbarali waomba msaada

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa vijiji vitano na vitongoji 41 vya Wilaya ya Mbarali ambavyo serikali imetangaza kuvifuta kupisha Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, wameomba waandaliwe maeneo ya kuhamia kabla ya kushurutishwa kuondoka ili kuepuka kuathiri shughuli zao.

Wananchi hao ambao asilimia kubwa ni wafugaji na wakulima, wameiomba serikali kutumia utaratibu uliotumia kuwaondoa wafugaji waliokuwa wanaishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro waliohamishiwa mkoani Tanga.

Walitoa ombi hilo juzi walipozungumza na waandishi wa habari kuhusu adha wanayoipata kwa sasa baada ya serikali kutangaza kuvifuta vijiji vyao kwa maelezo kuwa viko ndani ya hifadhi hiyo kutokana na tafsiri ya Tangazo la Serikali namba 28 la mwaka 2008 (GN.28).

Madumba Kashu ambaye ni mfugaji na mkazi wa kijiji cha Mwanavala alisema kwa sasa maisha yao yameanza kuwa magumu kutokana na uamuzi huo wa serikali.

Alisema mpaka sasa hawajui watahamia wapi hali ambayo inawafanya washindwe kufanya shughuli zao za maendeleo ikiwamo shughuli za kilimo ambacho wamekuwa wakikifanya miaka yote katika eneo hilo.

Pia alisema wamekuwa wakishuhudia katika baadhi ya maeneo wananchi wanapohamishwa wanakuwa wameshaandaliwa maeneo ya kwenda lakini wao mpaka sasa bado hawajui wataenda wapi.

"Tumeishi kwa miaka mingi sana kwenye kijiji hiki na tumekuwa tukifanya shughuli zetu hapa, uchumi wetu hutegemea zaidi kilimo na ufugaji lakini sasa hivi tumebaki njiapanda baada ya tangazo la Waziri wa Ardhi alipokuja na mawaziri wenzake," alisema Kashu.

Isaya Isaya, mkazi mwingine, alisema kwa sasa hata watoto hawaendi shuleni kutokana na wazazi wengi kutokuwa na mwelekeo unaoeleweka baada ya kuambiwa vijiji vyao vinaondolewa.

Aliiomba serikali kuwaruhusu waendelee na maisha kwenye maeneo hayo kwa maelezo kuwa kabla ya hapo walishawahi kuhamishwa kwenye vijiji vingine vilivyokuwa ndani ya hifadhi.

Alisema kitendo cha kuhamishwa mara kwa mara kinawafanya wakose uhuru wa kuishi huku akieleza kuwa kwa sasa wanaishi kwa hofu kwenye maeneo hayo.

# Kiwanda chajengwa kuondoa upotevu mboga na matunda

**Na Nebart Msokwa,** MPANDA

WAKULIMA wa matunda na mboga mkoani Katavi, wameondokana na tatizo la upotevu wa mazao ambao umekuwa ukisababishwa na mazao hayo kuoza baada ya kuvunwa na kukosa soko.

Hatua hiyo inatokana na kujengewa kiwanda cha kuchakata mazao hayo kwa lengo la kuyaongezea thamani kabla ya kuuzwa jambo ambalo litasaidia pia kupunguza tatizo la lishe kwa watoto.

Kiwanda hicho kimejengwa kwa ushirikiano kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Shirika la HELVETAS Tanzania kupitia Mradi wa Kilimo Bora kwa wanawake na vijana (KIBOWAVI) na Umoja wa Wasindikaji wa Mboga na Matunda Katavi (UWAMBOMAKA).

Mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa Mnyororo wa Thamani wa Kahawa, Chai na Mazao ya Bustani ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Kiwanda hicho kilizinduliwa mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Ushauri ya programu ya AGRI-CONNECT ya mkoa huo iliyowashirikisha pia wawakilishi wa EU na baadhi ya maofisa wa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha na Mipango.

**Pia tumefunga mfumo wa kamera za ulinzi, mfumo wa umeme wa jua, kaushio (Solar drier), mtambo wa kutengeneza wine na miundombinu mingine na miundombinu hii lazima ilindwe ili iwasaidie.**

Mkurugenzi wa Mradi wa KIBOWAVI, Daniel Kalimbya, alisema mradi huo umegharimu Euro 93,000 ambazo ni sawa na Sh. milioni 213. Alisema wameboresha jengo lililokuwapo awali, kujenga majengo mapya, kujenga uzio na kupanda bustani.

Alisema mbali na majengo ya kusindikia matunda na mboga pia wamejenga duka la kuuzia bidhaa za wasindikaji, mashine za kusagia unga wa lishe, mashine za kukatia viungo, jiko, vyoo viwili na vyumba viwili vya kubadilishia nguo.

"Pia tumefunga mfumo wa kamera za ulinzi, mfumo wa umeme wa jua, kaushio (Solar drier), mtambo wa kutengeneza wine na miundombinu mingine na miundombinu hii lazima ilindwe ili iwasaidie," alisema Kalimbya.

Mwenyekiti wa UWAMBOMAKA, Elizabeth Mzalla, alisema umoja huo ulianzishwa mwaka 2021 ukiwa na zaidi ya wanachama 100 ambao ni wasindikaji lakini kwa sasa wanachama hai wamebaki 71 ambao wanazalisha bidhaa mbalimbali.

Alisema walianzisha umoja huo kutokana na matatizo ambayo yalikuwa yanatokea kutokana na kila msindikaji kufanya shughuli hizo nyumbani ikiwamo ugumu wa kupata nembo ya ubora pamoja na mazingira kutokuwa bora.

Mkurugenzi wa HELVETAS Tanzania, Felix Bachmann, aliwapongeza wanachama wa chama cha wasindikaji wa bidhaa hizo kwa uthubutu akieleza kuwa wao ndio waanzilishi wa mpango huo.

Alisema wao walipata msukumo wa kufadhili ujenzi wa kiwanda hicho baada ya kuona wananchi hao tayari wameshaanza uzalishaji na hivyo wakaingia kwa lengo la kuboresha mazingira.

Alisema walifanya ziara katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Katavi na kushuhudia wananchi wakizalisha matunda na mboga kwa wingi na hivyo kuwa na uhakika wa kiwanda kuwa na mwendelezo.

Mwakilishi wa Balozi wa EU nchini, Anna Constantine, alisema katika ziara hiyo walifurahishwa na utekelezaji wa miradi ya AGRI-CONNECT katika mkoa wa Katavi.

Alisema walishuhudia matokeo mazuri ya fedha ambazo zinatolewa na EU kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini ikiwamo ya kwenye sekta ya kilimo, miundombinu ya barabara na miradi mingine.

Akifungua kiwanda hicho kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Crensencia Shayo, aliagiza miundombinu ya kiwanda hicho kulindwa na kutunzwa ili idumu kwa muda mrefu.



Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Mbeya, Nuhu Suleiman (wa pili kulia), akikabidhi msaada wa vyandarua kwa Ofisa Muuguzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo, Maridhia Mvungi, jana kwa ajili ya kuwasaidia kinamama na watoto wanaopata huduma za matibabu hospitalini hapo. TRA ilitoa vyandarua 100 ikiwa ni wiki ya shukrani kwa mlipakodi mkoani humo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanufaika wa TASAF wafadhili miradi maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KIKUNDI cha wanufaika wa Mpango wa Taifa wa Kunusuru Kaya Maskini cha Tujengane katika Kata ya Iganzo jijini Mbeya, kimesema kwa sasa wanachama wake wameondokana na umaskini na wameanza kushiriki kuchangia shughuli za maendeleo.

Katibu wa Kikundi hicho, Joseph Mboya, aliyasema hayo wakati maofisa wa jiji la Mbeya walipokuwa wanakagua vikundi vya wanufaika pamoja na shughuli za kiuchumi zilizoanzishwa na wanufaika wa mpango huo.

Alisema kikundi hicho kilianzishwa mwaka 2016 baada ya kuhamasishwa na maofisa maendeleo ya jamii wa jiji la Mbeya wakiwasihi kuwa wakiwa kwenye kikundi ni rahisi kupata maendeleo zaidi.

Kwa mujibu wa Mboya, kikundi chao kina wanachama 20 ambao kati yao wanawake ni 18 na wanaume ni wawili na kwamba wakati wanaanza walikuwa wanachangishana Sh. 2,000 kama ada ya kila mwezi lakini kwa sasa wanachangishana Sh. 10,000.

Alisema mpaka sasa kikundi kina mtaji wa Sh. milioni 3.4 ambazo kiasi zipo benki na zingine wanazo wanaendelea kuzungusha kwa ajili ya kujiinua zaidi kiuchumi.

Kikundi hicho, alisema kimeshiriki ujenzi wa miradi mbalimbali ikiwamo kuchangia ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, ujenzi wa daraja katika mtaa wao pamoja na ujenzi wa choo katika Shule ya Msingi Itiji ambayo ni ya watoto wenye mahitaji maalumu.

"Kwa sasa maisha yetu ni mazuri na kila mmoja anajiweza. Tumetoka kwenye mazingira ya kukosa hata mlo mmoja lakini kwa sasa tunaweza kuchangia hata shughuli za maendeleo, ni jambo ambalo tunajivunia sana," alisema Mboya.

Mwenyekiti wa Kikundi hicho, Angelina Mwakijolo, alisema mbali na kushiriki kwenye shughuli za maendeleo lakini kikundi kinamiliki ng'ombe mmoja wa maziwa ambaye kwa sasa amefikia umri wa kuzaa.

Alisema walimnunua ng'ombe huyo kutokana na michango ambayo walikuwa wanachangishana pamoja na faida walizokuwa wanapata kwenye kukopeshana.

Mbali na miradi ya pamoja, alisema kila mwanachama ana shughuli yake nyingine hasa ufugaji wa mifugo midogo kama kuku, bata, sungura na nguruwe ambayo mbali na kuwapatia kipato pia inawapatia lishe bora.





# Elimu kutolewa matumizi matokeo ya sensa 2022

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kuhakikisha wananchi wanatambua matumizi sahihi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika Agosti 23, mwaka huu, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) limeahidi kushirikiana na serikali ya Tanzania kutoa elimu.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapo baada ya kufanya mazungumzo na mwakilishi mkazi wa UNFPA, Wilfred Ochuan, Kamisaa wa Sensa nchini, Anne Makinda, alisema matokeo hayo yanatakiwa yalete tija kwa wananchi katika kufikishiwa shughuli za maendeleo na huduma za kijamii.

Makinda alisema moja ya shirika kati ya yale yaliyosaidia kufanikisha sensa ya watu na makazi ni UNFPA, kwasababu kimataifa wao ndio wanaosimamia mambo ya idadi ya watu.

Alisema walikuwa wanasaidia kwenye mambo ya ufundi, vifaa na kuwashirikisha na mataifa mengine ikiwamo kupata vishikwambi 600 kutoka Korea Kisini, 200 kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na Masuala ya Wanawake (UN- Women) na China.

"Huyu Wilfred Ochuan, ameteuliwa kwenda Ghana kuwa mwakilishi wa UNFPA, hivyo alikuja kutuaga na kuaga wafanyakazi wa hapa.

"Yeye ameahidi kwamba wataendelea kutusaidia ili watu kujua matumizi ya takwimu, hatuna mila sana ya kutumia takwimu lakini kwa sasa tunataka hilo liweze kuonekana kabisa," alisema Makinda.

Kadhalika, alisema watatumia takwimu hizo kufanya mipango yao, ufuatiliaji wa maendeleo mbalimbali ili ziweze kutumika kwenye bajeti ya serikali na waliahidi kutoa Euro 200,000.

"Tujaribu kutafuta mbinu zote Watanzania tuanze kutumia hizi sensa, kwani sensa zinagharama sana kwahiyo huwezi kufanya kitu kwa gharama halafu baadaye unakiacha tu," alisema.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema Tanzania ina watu wakarimu kama ilivyo kwa wananchi wa Ghana ambao nao pia siku zote wameonekana wakarimu, hivyo anaimani atakwenda kusaidia kupeleka picha ya nchi ya Tanzania ilivyo.

"Bila shaka tunaimani utachukua yale yote mazuri yaliyoko Tanzania kwani hata Rais wetu Samia Suluhu Hassan amekuwa akiishangaza dunia kwa mambo makubwa anayoendelea kuyafanya," alisema.

Dk. Chuwa alisema katika suala la takwimu nchi ya Tanzania imekuwa bingwa na imeonekana ni nchi inayoendelea kukua kiuchumi kwa takwimu za Afrika.

"Mafanikio hayo yote yamekuja kutokana na kuwa na mawasiliano na uwazi kwani ndio kitu kikubwa kwetu na pia tunajivunia kuwa na mtu kama mama Anne Makinda ambaye ndio aliyekuwa kamisaa wa sensa Tanzania Bara," alisema.

Naibu Mwakilishi Mkazi wa UNFPA anayemaliza muda wake nchini, Wilfred Ochang, aliishukuru serikali kwa kushiriki katika sensa kwani amejifunza mambo mengi mazuri na makubwa.

"Nawahakikishia kuwa naenda kupeleka mazuri yote yaliyomo na niliyoyapata katika nchi ya Tanzania na hongereni kwa kuweza kufanikisha zoezi zima la sensa ya watu na kazi.



Mwenyekiti Mwenza wa Baraza la Viongozi wa Dini mbalimbali nchini, Sheikh Hamisi Mataka (kushoto), akijadiliana jambo na Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa (kulia), Mkurugenzi wa Baraza hilo, Mchungaji Canon Thomas Muyya (wa pili kulia) na Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, kwenye mkutano wa baraza hilo ulioshirikisha wanasiasa na Jeshi la Polisi jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wakulima wafundwa matumizi mbegu asilia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKULIMA nchini wameshauriwa kutumia kilimo cha ikolojia matumizi ya mbegu bora na mbolea za asili ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ushauri huo ulitolewa juzi katika kijiji cha Msanga wilayani Chamwino kwenye mkutano wa wadau wa kilimo ikolojia kwa maisha na maendeleo endelevu ulioandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Action Aid Tanzania.

Akitoa elimu kwa wakulima wenzake, Magreth Malogo, alisema katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, wakiwa Jukwaa la Vijana Chamwino wamebuni maganda ya mayai yanayotumika kufukuza vidudu kwenye mimea.

"Maganda ya mayai unayachukua unayatwanga kwa njia ya kienyeji kwenye kinu au unayafikicha ukishamaliza kuyatwanga unaenda kumwaga kwenye mimea yako, ile harufu yake inasaidia kuzuia wadudu wasumbufu," alisema.

Pia alizishauri halmashauri kuboresha mashamba darasa, kutenga bajeti ndani ya vyanzo vya mapato ndani ya halmashauri kununua kipimia udongo ili kusaidia kujua afya ya udongo inayotakiwa.

Kaimu Mwenyekiti wa Halmashauri wa Wilaya ya Chamwino, Samweli Kaweya, aliwataka wakulima kutumia zana, mbolea, na dawa za asili katika kilimo.

Ofisa Kilimo Wilaya ya Chamwino, Living Kilawe, alisema wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na athari za mabadiliko tabianchi kwa kuwa na joto kali, mvua kutonyesha kwa wakati na ukame wa muda mrefu.

Pia alisema wilaya imegharamia upatikanaji wa hati ya shamba la ekari 8,000 katika kijiji cha Membe na ujenzi wa bwawa kubwa la kuvuna maji kwa ajili ya shughuli za mifugo na kilimo unaendelea na kiasi cha Sh. bilioni 11.96 kitatumika.

Mratibu wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia wa Action Aid, Tema Hassan, alisema lengo la kuandaa mkutano huo wa wadau ni kuwakumbusha wananchi wa wilaya hiyo kuhusu umuhimu wa kilimo ikolojia kuelekea msimu wa kilimo 2022/23.

# Hemed ahimiza usimamizi wa fedha za umma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amezitaka taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kusimamia matumizi ya fedha za umma ili zitumike kwa mujibu wa mipango iliyowekwa na si vinginevyo.

Hemed alibainisha hayo juzi ofisini kwake jijini hapo alipokutana na kufanya mazungumzo na watendaji wa Idara ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma.

Alisema taasisi nyingi za serikali baadhi ya huduma husitishwa kwa kisingizio cha ukosefu wa fedha kutokana na kukosekana kwa busara na maamuzi sahihi katika matumizi ya serikali.

Kadhalika, alieleza kufurahishwa kwake kuona watendaji wa idara hiyo wanavyowajibika ipasavyo licha ya kero mbalimbali wanazokabiliana nazo.

Vilevile, alisema ni dhahiri juhudi zinazofanywa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi zinaonekana na wengi hivyo ofisi yake itaendelea kuunga mkono kazi nzuri zinazofanywa hivi sasa visiwani humo.

Sambamba na hayo pia Makamu huyo wa Pili wa Rais wa Zanzibar aliipongeza Idara hiyo kwa kuendeleza ushirikiano baina yake na taasisi za serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hali ambayo itawarahisishia marais wote wawili kutimiza malengo yao ya kuwatumikia wananchi wao.

Kuhusu uendeshaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) Tawi la Dodoma, alisema amefurahishwa na hatua ya benki hiyo kufungua tawi jijini hapo eneo ambalo ndiyo makao makuu ya Tanzania.

"Benki hiio imeonesha utayari wa uwajibikaji kwa kuanza vyema biashara na niwatake kuingia katika ushindani wa kibiashara wa ubora wa huduma mkizingatia PBZ ni benki kongwe nchini," alisema.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Dk. Islam Seif Salum, alimweleza Hemed kuwa wizara itasimamia kero zote zinazoikabili idara hiyo ikiwamo ukosefu wa magari upungufu wa wafanyabiashara na nyinginezo.

Aliutaka uongozi wa idara hiyo kuwasilisha taarifa ya mapendekezo ya utatuzi wa kero na kuzingatia mfumo wa mtandao (E Office) katika kuandaa miundombinu ya ofisi.



# Kampuni yapaisha hadhi uwanja ndege

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Dnata inayotoa huduma katika jengo la abiria la tatu (Terminal Three) katika Uwanja waa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar, imebadilisha hadhi ya kiwanja hicho kwa kutoa huduma bora.

**Zanzibar imepata bahati ni kiwanja pekee Afrika kwa kampuni hiyo kutoa huduma zake.**

Hayo yalisemwa jana visiwani hapo na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhammed, wakati akifungua mafunzo kwa watoa huduma wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) yalioandaliwa na mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Dnata.

Alisema huduma bora zinazotolewa katika uwanja huo, imesababisha idadi ya wageni kuongezeka na kuridhishwa na huduma wanazopatiwa.

Waziri huyo alitaja sababu zingine zilizofanya Zanzibar kupokea watalii wengi ni juhudi za Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuitangaza Tanzania kupitia filamu ya The royal Tour.

"Mapato yatokanayo na watalii wanaopokewa katika viwanja vya ndege yameongezeka kutoka Sh. bilioni moja kwa kota moja hadi kufikia Sh. bilioni 6.7," alisema.

Waziri huyo alisema serikali ya Zanzibar inachukua juhudi kuhakikisha inatengeneza miundombinu ya kiuchumi na lengo la Rais Dk. Mwinyi liko katika ujenzi wa miundombinu ikiwamo ya kiuchumi na huduma za kijamii.

"Serikali inafanya kazi kubwa ya kutaka kuhakikisha uchumi wa nchi hii unakuwa na inapotengeneza miundombinu ya kiuchumi kuna viwanja vya ndege, barabara, ujenzi wa shule na hospitali za kisasa na huduma zingine," alisema.

Alisema kwa sasa serikali inatarajia kujenga jengo la nne la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na kujenga viwanja vya ndege vya Pemba na Nungwi ili kuwezesha wageni kuingia kwa wingi.

Pia aliwataka watoa huduma hao katika viwanja vya ndege kuongeza kasi ya utendaji wa kazi ili kupokea wageni wengi na serikali kupata mapato mengi yatokanayo na wageni wanaotumia viwanja vya ndege.

Waziri aliwataka watoa huduma hao kuwa na bashasha kwa wageni lakini kuwa waaminifu kwa sababu kufanya kinyume cha hayo ni kuwakimbiza wageni.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa ZAA, Seif Abdallah Juma, alisema Dnata ni kampuni kubwa duniani ambayo miongoni mwa huduma inazotoa ni kuhudumia ndege na iko katika zaidi ya viwanja vya ndege 120 duniani.

"Zanzibar imepata bahati ni kiwanja pekee Afrika kwa kampuni hiyo kutoa huduma zake," alisema.

Pia alisema serikali imechukua juhudi kubwa ya kuweka miundombinu hivyo kuhakikisha wafanyakazi wao wanauwezo wa kutosha wa kutoa huduma kulingana na viwango vya kimataifa.

Alisema abiria wanaowahudumia wengi wao wanapanda ndege za daraja la tano na wengi wanakwenda katika hoteli za nyota tano hivyo watahakikisha wanatoa huduma zinazoendana na kiwango cha kimataifa.

## Mkutano wa Baraza la Wawakilishi leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUTANO wa tisa wa Baraza la 10 la Wawakilishi unatarajiwa kuanza leo visiwani Zanzibar.

Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Issa Mselem, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa ya shughuli za baraza kwa waandishi wa habari huko Chukwani, nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema katika kikao hicho kutakuwa na shughuli mbalimbali ikiwamo kuwasilishwa miswaada minne ya sheria ambapo kati ya hiyo miswada miwili italetwa kwa hati ya dharura.

Alitaja miswada hiyo ni wa sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake na muswada wa sheria ya kufuta sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar na kutunga sheria mpya ya bodi ya mapato mwaka 2022.

Alisema miswada hiyo ya dharura itasomwa kwa mara ya kwanza na ya pili na utasomwa kwa kupitishwa vifungu vyake na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Pia alisema miswada hiyo mara nyingi huwa inakuja kwa hati ya dharura iliyotiwa saini na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Katibu huyo alitaja miswada mingine itakayowasilishwa katika kikao hicho ni wa sheria ya kufuta sheria ya watu wenye ulemavu (haki na fursa) namba tisa ya mwaka 2006 na kuweka masharti yanayohusiana na watu wenye ulemavu na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Pia mswaada wa sheria ya kurekebisha sheria ya chuo cha utawala wa umma namba moja ya mwaka 2007 na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Katibu huyo alisema miswada hiyo ya sheria iliwasilishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa Septemba, mwaka huu.

Hata hivyo, alisema katika kikao hicho, maswali 138 yameratibiwa kuulizwa na wawakilishi na kutolewa taarifa ya serikali ambayo itahusisha uwasilishwaji wa ripoti ya sita ya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2021/22.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akionyesha moja ya medali jijini Zanzibar jana, zitakazotolewa kwa washindi watakaoshiriki mbio katika shamrashamra za siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia zinazotarajiwa kufanyika kesho kutwa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wapewa mbinu kuhusu majanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Operesheni na Huduma za Kibinadamu kutoka Idara ya Maafa Zanzibar, Haji Faki Hamduni, amewataka wananchi kufuata maelekezo wanayopewa na viongozi wa kamati za maafa hasa linapojitokeza tatizo la dharura au majanga.

Hamduni aliyasema hayo jana katika ofisi ya kukabiliana na maafa huko Maruhubi wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kuna matukio mengi ya majanga ambayo yanatokea katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar, hivyo wananchi wanatakiwa kufuata maelekezo ya viongozi hao ili kuepusha maafa.

Mkurugenzi huyo alisema Kamisheni ya Maafa ina utaratibu wa kutoa elimu kupitia kamati za maafa za shehia ili kuwajengea uelewa wa kukabiliana na majanga yakitokea katika maeneo yao pamoja na kuwa mabalozi kwa jamii.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya ya Magharibi 'A', Juma Abdalla Hamad, alisema kupitia mapendekezo ya kamati ya kukabiliana na maafa ya wilaya kutasaidia kuandaa mbinu ya kugawana majukumu ya kiutendaji.

Alisema kikao cha kujadili mapendekezo ya mpango kazi wa kukabiliana na maafa kitasaidia kuandaa mbinu bora ya kujihami wakati wa dharura kama upepo, ajali, moto, mlipuko wa maradhi na mengineyo.

Mpango huo, alisema ni mwendelezo kwa watendaji kutoka taasisi mbalimbali kwa kupanga utaratibu wa kila mdau kutekeleza majukumu yake wakati wa dharura, majanga au maafa.

Mkuu wa Kituo cha Zimamoto na Uokozi Bandarini, Mrakibu Msaidizi (ASF) Jokha Patrick Bundala, alisema katika utekelezaji wa majukumu ya kituo hicho kuzimamoto, kuokoa wahanga na kuielimisha jamii kupitia vyombo vya habari.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa mapema katika vituo vya zimamoto na uokozi kwa kupiga simu namba 114 ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa.



# Mbinu mpya kukomesha walimu wakware Msalala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Halmashauri ya Msalala, Kahama mkoani Shinyanga, wameingia makubaliano ya kutoa adhabu kwa walimu wa shule za msingi na sekondari watakaobainika kujihusisha na vitendo vya mapenzi na wanafunzi wa kike.

Katika makubaliano hayo, mwalimu atakayebainika kufanya vitendo hivyo, atatozwa faini ya ng'ombe mmoja na kubadilishiwa kituo chake cha kazi.

Kwa vijana na watu wazima watakaobainika pia kujihusisha kimapenzi na wanafunzi, hao watatozwa faini ya ng'ombe mmoja kabla ya kufikishwa katika vyombo vya sheria kujibu tuhuma zinazowakabili.

Makubaliano hayo ni sehemu ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari wilayani hapo.

Hayo yalisemwa jana wilayani hapo na wasaidizi wa vituo vya taarifa na

**Makubaliano hayo ni sehemu ya kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari wilayani hapo.**

maarifa wa halmashauri katika kikao cha kubadilishana uzoefu katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

Mmoja wa wasaidizi hao kutoka Kata ya Shilela, Joseph Mbunge, alisema adhabu zingine walizokubaliana ni pamoja na kutozwa mabati matano na mifuko mitano ya saruji ambavyo vitatumika kukarabati vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari.

Alisema kuwa tangu wananchi wameingia makubaliano hayo, matukio ya mimba na ndoa za utotoni yamepungua kwa kiasi kikubwa kwa kuwa mengi yalikuwa yakifanywa na vijana waendesha bodaboda, wachimbaji wadogo wa madini na baadhi ya walimu hususani wa shule za sekondari wasio waadilifu.

Msaidizi mwingine, Soji Jonas, alisema kwa wale wanaofanyiwa vitendo vya kikatili ndani ya jamii na familia zao, wamekuwa wakiwaelekeza namna ya kupata haki zao kwa kutoa taarifa katika ofisi za ustawi wa jamii na dawati la jinsia lililoko kituo cha polisi kwa ajili ya kupata msaada wa kisheria.

Pia alisema mpaka sasa wameshafikisha malalamiko 38 yanayohusiana na ukatili wa kijinsia katika ofisi hizo na kati ya hayo 25 yanatokana na vipigo ndani ya familia baada ya kuvuna mazao hususani zao la mpunga na baadhi zimeshaanza kufanyiwa kazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Msaada wa Kisheria mkoani Shinyanga, John Shija, aliwashauri wananchi kuendelea kufanya vikao katika vijiji vyote vya Msalala na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwani maeneo ya pembezoni yanaongoza kwa matukio hayo.

Alikemea wazazi wanaokutana na kufikia makubaliano ya kulipwa fidia na watuhumiwa wanapofanya vitendo vya ukatili wa kijinsia pale hususani msichana anapopewa mimba.



Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma ya Msaada wa Kisheria Mkoa wa Shinyanga, John Shija, akibadilishana uzoefu, kuhusu mafanikio na changamoto katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia ili kupata matokeo bora, wakati wa mkutano wa walaghabishi na wasaidizi wa kisheria wa Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama, mkoani humo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Kiwanda pamba chateketea moto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KIWANDA cha Jielong kilichoko Manispaa ya Shinyanga, ambacho kilipewa kazi ya kuzalisha mbegu za pamba na kusambaza kwa wakulima, kimeungua moto huku tani 210 za mbegu zilizokuwa ndani zikisalimika.

Tukio la kuungua moto lilitokea juzi majira ya saa 10:00 jioni wakati wafanyakazi wa kiwanda hicho wakiwa katika uzalishaji wa mbegu.

Wakati wafanyakazi hao wakiendelea na kazi zao, ghafla ulizuka moto uliounguza kiwanda hicho na kujeruhi baadhi ya wafanyakazi.

Mmoja wa wafanyakazi wa kiwanda hicho, Thomas Mayunga, alisema wakati wakiendelea na majukumu yao, mashine moja ilipata tatizo kwa kuingiliwa na mchanga na kusababisha msuguano na kisha moto kuanza kuwaka.

Ofisa Kilimo kutoka Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), Thomas Tilihongerwa, alisema baada ya kupata taarifa ya tukio hilo, alifika hapo kwa ajili ya kujionea uharibifu uliotokea. Alisema mbegu za wakulima ambazo zilikuwa tayari zimezalishwa zinazofikia tani 210 hazikuungua na moto huo.

Alilishukuru Jeshi la Zimamoto na Ukoaji mkoani Shinyanga kwa kufika kwa wakati eneo la tukio na kufanikiwa kuuzima moto huo.

"Niwatoe wasiwasi wakulima wa pamba kuwa mbegu zetu zipo salama tani zote 210 hazikufikiwa na moto na hivi karibuni tutaanza kuzisambaza," alisema Tiluhongerwa.

Msemaji wa kiwanda hicho, Qi Fengzhou, alisema kitendo cha jeshi hilo kufika kwa wakati kilisaidia kuzima moto huo na kwamba hakuna madhara makubwa yaliyotokea.

# Wachaguliwa wenyeviti wa-NEC mikoa

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetangaza washindi wa nafasi mbalimbali kwa ngazi ya mkoa katika uchaguzi uliofanyika juzi na jana katika maeneo mbalimbali.

Katika Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa amechaguliwa kuwa mwenyekiti wake kwa muhula wa pili kwa kujinyakulia kura 668 na kuwabwaga wapinzani wake katika uchaguzi huo.

Akitangaza matokeo juzi mjini hapa, msimamizi wa uchaguzi huo, Thobias Andengenye, alisema wajumbe walioshiriki kupiga kura katika uchaguzi huo walikuwa 757 na kura moja iliharibika.

Alisema kura halali zilikuwa 756 na mshindi alipata kura 668 huku Costantine Nkuba akipata kura 35 na Eliaza Kanuya kura 53.

Alimtangaza Mlowa kuwa mshindi katika nafasi hiyo ya uenyekiti wa chama hicho kwa kipindi cha miaka mitano huku katika nafasi ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya chama hicho, Gasper Kileo alibuka mshindi.

Pia mkutano huo uliwachagua wajumbe wa mkutano mkuu wa Mkoa wa Shinyanga kutoka Wilaya za Kahama, Shinyanga Vijijini, Shinyanga Mjini na Kishapu.

Katika Mkoa wa Tabora, wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM, walimchagua Hassan Wakasuvi kuwa mwenyekiti wa chama hicho kwa kipindi cha miaka mitano.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo uliofanyika jana katika ukumbi wa Chuo cha Tabora Polytechnique (TPC) msimamizi wa uchaguzi huo, Martin Shigella, alisema Wakasuvi alipata zaidi ya asilimia 90 ya kura zote.

Alibainisha kuwa nafasi hiyo ilikuwa na wagombea watatu ambao mbali na Wakasuvi, wengine ni Waziri Jumbe na Stella Enock.

Licha ya Jumbe kutangaza kujitoa, bado alipigiwa kura 14 na baadhi ya wajumbe, huku Stella Enock akipata kura 80 na Wakasuvi kura 1,030 kati ya kura zote 1124 zilizopigwa.

katika uchaguzi huo, Mohamed Hamdan Nassoro (Meddy) alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM baada ya kupata asilimia 90.6 ya kura zote.

Kwa nafasi za wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ngazi ya mkoa, waliochaguliwa kwa kila wilaya ni Alcard Ilagila na Leonard Amando (Urambo), Iddy Moshi na Razack Juma (Uyui) na Lucas Selelii na Getrude Pius (Nzega).

Wengine ni John Kadutu na Denis Kilatu (Kaliua), Regina Tadeo na Aneth John (Igunga), Jaha Kaducha na Zabibu Nyamwelu (Tabora Mjini) na Said Maulid na Alijah Mwiga (Sikonge).

Katika Mkoa wa Mwanza, CCM ilimchagua Sixbert Reuben kuwa mwenyekiti na kuwashinda wenzake wawili aliogombea nao katika nafasi hiyo.

Msimamizi wa uchaguzi huo, Gilbert Kalima, alimtangaza Reuben kuwa mwenyekiti wa chama hicho katika kipindi cha miaka mitano.

Alisema kura zilizopigwa zilikuwa 1127 na kati ya hizo mbili ziliharibika huku mshindi wa kwanza akipata kura 876, Nyilizu Makongoro akipata kura 236 na Nyanda Elias kura saba.

Katika nafasi ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC), Babu Jamal alishinda nafasi hiyo kwa kupata kura 940 na kuwapita washindani wenzake, Elizabeth Nyimbi kura 876 na Limbu Festus aliyepata kura 78.

Mkoani Geita CCM imemchagua Nicolaus Kasendamila kuwa mwenyekiti wake katika uchaguzi uliofanyika juzi mjini Geita.

## Chama tawala chapata kura asilimia 99 Guinea

**CONAKRY, Guinea**

MATOKEO ya awali ya uchaguzi yaliyotolewa na serikali ya Equatorial Guinea yameonyesha chama tawala kimepata zaidi ya asilimia 99 ya kura zilizohesabiwa katika uchaguzi wa rais, wabunge na manispaa.

Taifa hilo liliendesha mchakato wa upigaji kura kumchagua Rais na wabunge, mwishoni mwa wiki iliyopita, huku Rais aliyeongoza kwa zaidi ya miaka 43 anatajwa kuongoza katika kura.

Wagombea wawili wa upinzani waliokuwa wakigombea, Buenaventura Monsuy Asumu, ambaye tayari amegombea katika chaguzi tano zilizopita, na Andrés Esono Ondo, ambaye anagombea kwa mara ya kwanza walishindwa.

Zaidi ya watu 400,000 walijiandikisha kupiga kura katika nchi hiyo yenye takriban watu milioni 1.5, ambapo wapinzani walilalamika kuwa ulitokea udanganyifu na ukiukaji wa sheria kwenye uchaguzi huo. Obiang aliingia madarakani mnamo mwaka 1979 baada ya kuuangusha utawala wa rais wa kwanza aliyeingia madarakani tangu nchi hiyo ilipopata uhuru wake kutoka kwa Uhispania mnamo mwaka 1968.

Katika uchaguzi huo Obiang anatarajiwa kupata zaidi ya asilimia 95 ya kura, na hivyo kuendelea na muhula wa sita.

**VOA**

## 180 wafariki kwa tetemeko Indonesia

**JAKARTA, Indonesia**

WAOKOAJI wameendelea leo kutafuta miili na manusura wa tetemeko la ardhi lililoikumba Indonesia juzi mchana na kusababisha vifo vya watu 182 pamoja na kujeruhi maelfu.

Mitambo ya kufukua vifusi, malori na vifaa vingine vya uokozi vilitumwa usiku wa kuamkia jana kwenda eneo lililoathiriwa zaidi la kitongoji cha Cianjur, kusini mwa mji mkuu Jakarta kusaidia juhudi za uokoaji.

Mbali ya watu waliopoteza maisha mamlaka za nchi hiyo zimeripoti kuwa zaidi ya watu 300 wamejeruhiwa vibaya, wengine 600 wamepata majeraha madogo na haijafahamika hadi sasa idadi ya watu wasiojulikana walipo.

Tetemeko hilo la ukubwa wa 5.6 katika kipimo cha Ritcher lilisababisha mitetemo iliyoporomosha majengo, kuharibu miundombinu na kuwafukia watu chini ya vifusi vikubwa vya udongo.

Gavana wa Mkoa wa Java unaotajwa kupoteza watu 50, Ridwan Kamil, alithibitisha kutokea kwa maafa hayo, huku wengine, zaidi ya 700 wakijeruhiwa.

Kuna wasiwasi kuwa huenda idadi ya vifo ikaongezeka kwa sababu idadi kubwa ya watu bado wamekwama kwenye vifusi vya majengo yaliyoanguka.

**DW**

# Uganda kutuma wanajeshi 1000 DRC

**KAMPALA, Uganda**

SERIKALI ya Uganda imesema itatuma wanajeshi wake 1000 katika nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kufikia mwishoni mwa mwezi huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, wanajeshi hao wanaingia mashariki mwa DRC chini ya makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Ilielezwa kuwa nchi saba za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kutuma wanajeshi kupambana na makundi ya waasi ambayo yamesababisha ukosefu wa usalama mashariki mwa DRC kwa miongo kadhaa.

Uganda itakuwa nchi ya tatu kutuma wanajeshi wake nchini DRC baada ya Kenya na Burundi.

Msemaji wa jeshi la Uganda Brigendia Jenerali, Felix Kulaigye alisema kwamba wanajeshi wa Uganda wapo tayari kusaidia katika kurejesha amani katika nchi hiyo jirani.

Hata hivyo, baadhi ya makundi ya kijamii yamekuwa yakidai kwamba Uganda inahusika pakubwa na vita vinavyoendelea Congo, yakidai kwamba inaunga mkono waasi wa M23.

Tayari Uganda ina wanajeshi wake nchini DRC, wanaopigana na kundi la waasi la Allied Democratic Forces ADF.

Pia ilibainishwa kuwa Uganda imeilipa DRC dola milioni 65 kama sehemu ya dola milioni 325 ilizoagizwa kulipa Congo kwa hasara ambayo Congo ilipata wakati wanajeshi wa Uganda waliingia nchini humo miaka ya 1990.

Licha ya mabilioni ya dola kutumika kwa kikosi cha jeshi la umoja wa mataifa kulinda amani nchini DRC, bado kuna zaidi ya makundi ya waasi 120 likiwemo kundi la M23, yanayopigana na wanajeshi wa serikali.

DRC imeshutumu Rwanda kwa kuunga mkono waasi wa M23, madai ambayo Rwanda imekuwa ikikanusha kila mara.

***VOA***



Mwonekano wa majengo yaliyoharibiwa na tetemeko la ardhi Indonesia. **PICHA: MTANDAO.**

# Marekani yaishutumu Urusi kufanya uhalifu Kherson

**WASHINGTON, Marekani**

OFISA mwandamizi wa Marekani amesema Urusi imefanya uhalifu wa kivita kwa kuwaua, kuwatesa na kuwateka nyara raia wa Kherson nchini Ukraine kwa mfumo wa wazi uliopangwa.

Haya yanafanyika wakati ambapo Ukraine inasema imegundua maeneo manne yaliyokuwa yanatumiwa na Urusi kuwatesa Waukraine katika eneo lililokombolewa hivi majuzi la Kherson.

Kwa mujibu wa taarifa ya DW iliyochapishwa jana, balozi wa Marekani kuhusiana na Sheria ya Uhalifu Duniani Beth Van Schaack, alisema kuna ushahidi mkubwa kwamba vitendo vya mateso vya Urusi nchini Ukraine havikutekelezwa kwa kushtukiza.

Van Schaack, alisema kuna ushahidi kwamba uvamizi wa Urusi nchini Ukraine umeandamana na vitendo vya uhalifu wa kivita katika kila eneo ambalo majeshi ya Urusi yalitumwa.

Balozi huyo alisema ushahidi kutoka maeneo yaliyokombolewa unaonyesha raia na wafungwa wa kivita walishambuliwa na kuteswa kwa kusudi. Huku Waukraine wakiwemo watoto waliondolewa na kupelekwa Urusi kwa lazima na zaidi ya hayo kulikua na mauaji na udhalilishaji wa kingono.

Nayo ofisi ya mwendesha mashtaka mkuu wa Ukraine, ilitoa taarifa iliyosema kwamba imegundua maeneo manne yaliyotumiwa na Urusi kuwazuia na kuwatesa watu huko Kherson, ofisi hiyo ya mwendesha mashtaka ilisema imegundua maeneo hayo baada ya kufanya uchunguzi kwa ushirikiano na maofisa wa polisi na wataalam.

Taarifa hiyo ilisema walipata sime na kifaa kilichotumiwa na majeshi ya Urusi kuwatesa watu kwa kutumia umeme. Mamlaka za Urusi pia ziliacha nyaraka zilizoonyesha uongozi wa maeneo hayo ya mateso, huku mkaazi mmoja wa Kherson akiliambia shirika la habari la Ufaransa AFP kuwa aliteswa kwa wiki kadhaa katika mojawapo ya maeneo hayo.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy kwa mara nyengine aliitaka Jumuiya ya Kujihami ya (NATO) na marafiki zake kuitambua Urusi kama taifa la kigaidi.

"Natoa wito kwa jumuiya ya NATO kuchukua hatua madhubuti kutekeleza mpango wa amani wa Ukraine unaoweza kuhakikisha amani na haki kwa Ukraine na jamii nzima ya Ulaya na Atlantiki.

"Natoa wito pia kwa mabunge yote ya nchi wanachama wa jumuiya ya NATO kuchukua uamuzi wa kuitambua Urusi kama taifa la kigaidi. Naamini kwamba polepole tutafika hapa, hivi ndivyo Urusi itakavyoonekana duniani," alisema Zelenskiy.

***DW***

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**DAVID ROBERT SUNGI** anatangaza kupotea kwa **RESULT SLIP** ya kidato cha sita chenye index namba **S0612/0677** kilichotolewa na **KAGANGO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/452519/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**
**Shauri Na. 80/2022**
**Jina la Mdai ......................HADIJA JAICY KAYERA**
**Jina la Mdaiwa ............... BAKARY ENEZA MSUYA**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

**(Kanuni ya 18 ya kanuni ya taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA. BAKARY ENEZA MSUYA**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TALAKA, MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA MTOTO**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 06 mwezi 12 mwaka 2022 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shihidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo. Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 22 mwezi 11 mwaka 2022.

---

**FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 858 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late JOSEPH AMBROSE**

**and**

**In the Matter of Application for Letters of Administration by**
**JOHN CYPRIAN NYEBINA**

### GENERAL CITATION
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12th day of December, 2022.

Dated at DAR ES SALAAM this 22 day of November, 2022.

Senior Resident Magistrate

---

## KUPOTELEWA NA CHETI



**MARY CHRISTOPHER SOTTA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S3914-0547** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Alphagems Secondary School February, 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/452917/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENEDICTOR ANTONY SINDABAHA.** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 628 CIG aina ya SUZUKI ESCUDO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi. **KAHA/RB/ 763/ 2022.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**BONIPHACE GERVAS SEMBUA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1222/0263** kilichotolea na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIHONDA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **DAR/CHU/453218/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA /HAKIMU MKAZI**
**KINONDONI/KIVUKONI**
**SHAURI LA MADAI NA 211 YA 2022**
**HAMIS RAMADHANI .............MDAI**
**DHIDI YA**
**SAID KASSIM KANYORO.........MDAIWA**
**Kwa**
**SAID KASSIM KANYORO**
**MIS MM DISTRIBUTORS**
**ALLIANCE INSURANCE CORPORATION**

### KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria mahakama hii binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya Alhamisi Tarehe 15 Mwezi 12 Mwaka 2022 saa 2:00 Asubuhi.

Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIZO:**
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 21 Mwezi 11 Mwaka 2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 74 YA 2021**

**ABEID RASHID NITU(msimamizi wa mirathi ya marehemu)**

**RASHID RAMADHANI NITU......................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**SAID AHMADI KONDO.................................MJIBU MAOMBI**
**BEATUS LYIMO..........................................MJIBU MAOMBI**

### WITO/KUITWA SHAURINI KWA
**BEATUS LYIMO**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 06/12/2022 mbele ya mwenyekiti M.KHASIM wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 17 Mwezi November 2022.


M. KHASIM
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DIAMOND AJISHANGAA KUKONDA

MSANII wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, kwa mara ya kwanza amezungumzia mwonekano wa mwili wake na kusema kuwa hata yeye haelewi ni kwa nini kila siku anazidi kupungua.

Akiandika katika moja ya picha ambazo Mbosso alipakia kwenye ukurasa wake wa Instagram, Diamond alionyesha kushangaa kwake kutokana na kuendelea kupunguka kwa mwili.

Alisema si yeye tu anazidi kushangaa kutokana na mabadiliko hayo ya mwili wake bali pia hata Watanzania wote wamekuwa wakiibua maswali kama hayo.


"Halafu nimekuwa mdogo, kila siku nazidi kuwa mdogomdogo. Hilo suala linawachanganya Watanzania wengi," aliandika Diamond.

Jibu la Mbosso ndio liliwaacha wengi katika gumzo kubwa kwani walionekana kutolielewa.

Kwa kawaida wengi wanamjua Diamond kuwa wa miaka chini ya arobaini, lakini kwa jibu la Mbosso alionekana kudokeza kuwa msanii huyo tajiri wa WCB Wasafi ana miaka zaidi ya 40.

"Kweli kaka kama hauna miaka 40 vile safi sanaa," aliandika Mbosso.

## ZUCHU AWASIFIA NANDY, MAUA SAMA



NYOTA wa kike wa muziki wa Bongo Fleva, Zuhura Othman 'Zuchu', amewapongeza wasanii wenzake wa kike Watanzania katika jukwaa la tuzo za Afrimma nchini Marekani.

Baada ya kushinda tuzo ya msanii bora wa kike wa Afrika Mashariki, Zuchu alipata nafasi ya kutoa hotuba yake.

Na katika hotuba hiyo aliwashukuru watu mbalimbali na kuwasifia wasanii wote wa kike wa Tanzania.

"Tuzo hii ni ya kwetu wote, nawakubali wasanii wenzangu wa kike kina Nandy, Maua Sama, Rose Ree na wengine wote ambao tunawakilisha Afrika Mashariki," alisema Nandy.

## BABY MADAHA AFUNGA NDOA



MSANII Baby Madaha amefichua kwamba amefunga ndoa na mpenzi wake wa muda mrefu.

Baby amesema kwamba, amefunga ndoa hiyo Novemba 19, mwaka huu ambapo kupitia ukurasa wake wa Instagram, ameposti picha mbalimbali za shughuli hiyo ambayo hakueleza imefanyikia wapi.

Lakini ameweka picha za kanisani pamoja na ukumbini huku akisema amefunga ndoa kwenye siku yake ya kuzaliwa.

"Nimebarikiwa, nimefunga ndoa Novemba 19 siku yangu ya kuzaliwa," ameandika Baby Madaha.

Baby ni msanii wa muda mrefu ndani ya kilinge cha Bongo Fleva na amejipatia umaarufu zaidi kupitia ngoma yake ya mwanzoni kabisa inayokwenda kwa jina la 'Amore'.

# MFAUME, PIARALI KUFUNGA MWAKA ULINGONI ARUSHA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanya mapambano mbalimbali ndani na nje ya Dar es Salaam kuanzia Januari hadi Novemba, mwaka huu, Promota wa Ngumi za Kulipwa nchini, Selemani Semunyu, sasa ameahidi kufunga mwaka 2022 na kukaribisha 2023 kwa pambano la Usiku wa Mabingwa litakalofanyika jijini Arusha.

Pambano hilo ambalo linatarajia kufanyika Desemba 26, mwaka huu litawakutanisha mafahari wawili wa Dar es Salaam, Mfaume Mfaume kutoka Mabibo na Idd Piarali wa Manzese.

Akizungumza na gazeti hili jana, Semunyu, alisema baada ya kufunga mwaka 2022 jijini Dar es Salaam kwa pambano la Dar Boxing Derby, lililofanyika juzi katika Uwanja wa Kinesi uliopo Urafiki, sasa anaenda kuufunga mwaka kwa kuandaa pambano la Usiku wa Mabingwa.

Alisema kwa mwaka huu ameandaa mapambano katika mikoa mbalimbali nchini, hivyo sasa anaenda kuufunga mwaka katika Jiji la Arusha kwa kuwakutanisha wababe hao wawili.

"Nawashukuru kwa sapoti kubwa wanayonipa Watanzania hasa katika mapambano yote pamoja na hili la Dar Boxing Derby lililofanyika Dar es Salaam, kutokana na mchango wa wakazi wa jiji hili kuniunga mkono sasa tunaingia mwaka 2023 vizuri.

"Kabla ya kuanza 2023 tunamaliza huu mwaka kwa kuwapelekea watu wa Arusha na vitongoji vyake pambano la Usiku wa Mabingwa litakalokutanisha mabondia wawili Mfaume na Piarali. Mapambano mengi mwaka huu nilifanya mikoani, hivyo nimeona si jambo jema kumaliza mwaka bila kuwapa tena burudani, " alisema Semunyu.

Alisema pambano hilo la Desemba 26, litakuwa kali kutokana upinzani na utani (Derby) kati ya mabondia kutoka Manzese (Piarali) na Mabibo (Mfaume).

## TUMECHOMOA...



Gareth Bale akishangilia baada ya kuisawazishia Wales kwa mkwaju wa penalti dakika ya 82 wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Marekani kwenye mechi ya Kombe la Dunia nchini Qatar juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

## Mexime atoa pole kwa TZ Prisons

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Mexime, ametoa pole kwa Klabu ya Tanzania Prisons baada ya timu yake kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi miamba hiyo ya jijini Mbeya, akisema anaelewa hali ngumu wanayoipitia.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi, Mexime aliwapongeza wachezaji wake kwa ushindi licha ya kueleza hawakucheza vizuri katika mchezo huo.

"Niwape pole Prisons kwa sababu najua hali wanayopitia, hawajapata matokeo mazuri kwa mechi kadhaa, kama kocha unajua kabisa jinsi gani wanavyojisikia, ni hali ngumu kidogo, lakini mimi nawapongeza wachezaji wangu, walifuata kile tulichoelekezana kwenye uwanja wa mazoezi, mchezo ulikuwa mgumu, ingawa leo hatukucheza vizuri sana, lakini kikubwa ni kupata matokeo," alisema kocha huyo.

Alisema Prisons walikuwa wanataka matokeo kwa sababu wametoka kupoteza mechi.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Prisons, Shaaban Mtupa, alisema waliutawala mchezo kwa kiasi kikubwa, lakini makosa yaliyofanywa na walinzi wake dakika za mwisho ndiyo yaliyowagharimu.

"Haikuwa matarajio yetu, tulitaka kupata matokeo mazuri, vijana walicheza vizuri muda mwingine mchezo tumetawala, tumefanya makosa dakika za mwisho wapinzani wetu wakapata bao, Kagera Sugar walikuwa na bahati kwenye mechi ya leo ndiyo maama tumefungwa.

Alisema mipango yao walitengeneza mazingira ya kuwafanya Kagera Sugar wachoke, na kweli walifanikiwa, lakini mastraika wake hawakuwa makini kwani tayari wapinzani wao walikuwa hoi.

Matokeo hayo yameifanya Kagera Sugar kupaa hadi nafasi ya tisa kwa pointi 15 ikicheza mechi 13, na kuiacha Prisons kwenye nafasi ya 11 ikiwa na pointi 14.

# Shikalo, Mtibwa ndio basi tena

**Na Hadija Mngwai**

BAADA ya kuachana na Kocha wa Makipa, Razack Siwa, Uongozi wa Mtibwa Sugar umesema kuwa upo hatua za mwisho za kuachana na mlinda mlango wao, Farouk Shikalo baada ya kufikia makubaliano.

Shikalo alitua Mtibwa Sugar akitokea Yanga na msimu huu hajaonyesha kiwango chakuvutia hatua ambayo Mtibwa inaona ni bora kuachana naye.

Mechi ya mwisho Shikalo kuichezea Mtibwa aliruhusu mabao manne wakati wakichezea kichapo cha 4-3 dhidi ya Azam FC katika Uwanja wa Benjamin Mungu, Turiani mkoani Morogoro.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema uongozi upo katika hatua za mwisho za kuachana na nyota huyo huku wakiwa tayari wameshaachana na kocha wa makipa, Siwa.

"Tupo katika mazungumzo ya mwisho na Shikalo na ndani ya siku mbili hizi tutatoa taarifa, maamuzi haya ni makubaliano ya pande zote mbili uongozi na mchezaji.

"Kwa upande wa Kocha wa Makipa, Razack Siwa, tayari tumeshaachana naye na ameshaondoka nchini kuelekea Kenya baada ya kufikia makubaliano ya pande zote mbili," alisema.

Akizungumzia ushindi wao wa juzi, Kifaru alisema: " Tunashukuru baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union ni faraja kwetu, lengo letu ni kuhakikisha tunafanikiwa kuibuka na ushindi michezo inayofuata.

"Tulifungwa mabao matano na Simba pia tulipoteza kwa mabao 4-3 dhidi ya Azam, hivyo ushindi huu ni muhimu kwetu kuhakikisha tunajiweka katika nafasi nzuri ya msimamo wa Ligi Kuu."

Matokeo hayo yanaifanya Mtibwa Sugar kufikisha pointi 21 huku ikikaa katika nafasi ya nne ya msimamo wa ligi hiyo baada ya kushuka dimbani mara 13 msimu huu. Kabla ya mechi ya jana kati ya Dodoma Jiji FC na Yanga, iliyochezwa Uwanja wa Liti mkoani Singida, Azam FC ndiyo iliyokuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 29 zilizotokana na kushuaka dimbani mara 13, ikifuatiwa na Simba yenye pointi 27 zikitokana na michezo 12, huku watani zao wakiwa na alama 26.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE AFUATILIWA LIVERPOOL
KLABU ya Liverpool inamfuatilia Declan Rice wa England kwenye Kombe la Dunia kabla ya kuweka dau la kumnunua kiungo huyo mwenye miaka 23 anayeichezea West Ham. ***(Football Insider)***

### PSG KUMCHUNGUZA MARTINELLI
KLABU ya Paris St-Germain imetuma maskauti kumtazama mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Martinelli mwenye umri wa miaka 21, akiichezea Brazil kwenye Kombe la Dunia. ***(Todofichajes)***

### GUARDIOLA KUONGEZA MKATABA
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anakaribia kukubali mkataba mpya utakaomuweka klabuni hapo hadi msimu wa majira ya joto wa 2025. ***(Sport)***

### PICKFORD ASAKWA SPURS
MCHEZAJI wa kimataifa wa England na Everton, Jordan Pickford, mwenye umri wa miaka 28 na wachezaji wawili wa Hispania, David Raya wa Brentford na Robert Sanchez, 25, wa Brighton wanasakwa na Tottenham. ***(90Min)***

### NKUNKU ATAKIWA CHELSEA
CHELSEA inakaribia kukamilisha dili la kumnunua Christopher Nkunku, mshambuliaji wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 25 akitokea RB Leipzig. (Le10 Sport)

### RONALDO HATAKIWI MADRID
REAL Madrid haina mpango wa kumsajili tena mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 kutoka Manchester United kwenye dirisha la Januari. ***(Marca)***

### VLAHOVIC AMULIKWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United inamuwania mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 22 ikiwa watafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa ULaya msimu ujao. ***(Calciomercatoweb)***

### O'NEIL NA BOURNEMOUTH
KLABU ya Bournemouth inatazamiwa kumteua kocha wa muda, Gary O'Neil kuwa wa kudumu baada ya mazungumzo na kocha wa zamani wa Leeds United, Marcelo Bielsa kuvunjika. ***(Football Insider)***

### ASENSIO KUONGEZA MKATABA
MKATABA wa kiungo wa kati wa Hispania, Marco Asensio na Real Madrid unamalizika msimu wa majira ya joto na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amesema anatumaini kuwa anaweza kukubaliana mkataba mpya na klabu hiyo ya Bernabeu, huku uamuzi kuhusu mustakabali wake ukitarajiwa kufanywa baada ya Kombe la Dunia. ***(Radio Marca, via Goal)***

### ZIDANE KUMRITHI DESCHAMPS
KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amekubali kurithi mikoba ya Didier Deschamps kama kocha mpya wa Timu ya Taifa ya Ufaransa baada ya Kombe la Dunia. ***(Mundo Deportivo)***

### DYCHE KUTUA BURNLEY
ALIYEKUWA Kocha wa Burnley, Sean Dyche, ana nia ya kuzungumza na Rangers kuhusu kuifundisha baada ya kumfukuza kocha wao, Giovanni van Bronckhorst. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOUTHGATE AANIKA HALI YA MAGUIRE KOMBE LA DUNIA

Alijisikia mgonjwa, aliashiria kabla ya bao la kwanza, zaidi ya hiyo hakuna sababu...

**DOHA, Qatar**

GARETH Southgate amefichua kwamba Harry Maguire alitolewa katika ushindi wa mabao 6-2 wa England dhidi ya Iran kutokana na ugonjwa na si kuumia.

Kujumuishwa kwa Maguire katika kikosi cha Southgate cha Kombe la Dunia kumejadiliwa vikali baada ya kutokuwa na nafasi pale Manchester United, lakini alionyesha kiwango kizuri wakati England ilipoanza kampeni ya Kundi B kwa mtindo wa kuvutia Jumatatu.

Uwapo wa mlinzi huyo ulisumbua Iran muda wote, na alitoa pasi ya bao la Bukayo Saka kuwaweka England mbele kwa mabao 2-0.

Nafasi ya Maguire ilichukuliwa na Eric Dier baada ya kuonekana kufanyiwa uchunguzi wa mshtuko baada ya mapumziko, lakini Southgate aliamua kupunguza hofu kuhusu hali yake baada ya ushindi huo.

"Harry Maguire alijisikia mgonjwa. Aliashiria kabla ya bao la kwanza la Iran," alisema Southgate.

"Hakukuwa na sababu ya kuendelea, lakini zaidi ya hiyo, hakuna sababu za wasiwasi."

Akiandika kwenye Twitter, Maguire alisema: "Nilijisikia vibaya katika kipindi cha pili kwa hiyo nilitoka kama tahadhari. Nikitazamia Ijumaa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,053,2

MECHI KALI

MBEYA CITY
VERSUS
SIMBA

1 | 5.26
X | 3.12
2 | 1.70

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# UHOLANZI KUTATHMINI UTIMAMU WA DEPAY



**DOH, Qatar**

LOUIS van Gaal amesema Uholanzi itatathmini utimamu wa kuwa 'fiti' kwa Memphis Depay baada ya ushindi wao dhidi ya Senegal, juzi kwenye Kombe la Dunia.

'Oranje' hao waliadhimisha kurejea kwao kwa fainali za Kombe la Dunia kwa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya mabingwa wa Kombe la Mataifa ya Afrika, huku mabao ya dakika za lala salama kutoka kwa Cody Gakpo na Davy Klaassen yakiwapa pointi zote tatu katika Kundi A.

Depay alianza mchezo huo akiwa benchi kutokana na tatizo la misuli ya paja linaloendelea, lakini aliingizwa dakika 28 za mwisho kwenye Uwanja wa Al Thumama na fowadi huyo wa Barcelona atatarajia kucheza dhidi ya Ecuador Ijumaa.

"Tulikubaliana kabla ya mchezo kwamba angecheza takriban nusu saa," alisema Van Gaal kuhusu Depay, ambaye amecheza mechi mbili pekee za LaLiga msimu huu.

"Akiwa na Ecuador, atataka kucheza, lakini lazima nipime kiwango chake baada ya mchezo huu. Sikuwahi kufikiria kwamba tutapoteza na kwa kuingia kwa Depay, nilitaka kupata nafasi nyingi za kufunga. Ni mchezaji anayeweza kuleta tofauti."

Van Gaal alisimamia ushindi wake wa 38 akiwa kocha wa Uholanzi, akiweka rekodi kwa kushinda mechi nyingi zaidi kuliko kocha yeyote aliyekiongoza kikosi hicho.

Pia alisifia kiwango cha Gakpo na kipa Andries Noppert, ambaye alifunga bao lake la kwanza kwenye mechi yake ya kwanza ya kimataifa.

"Gakpo alikuwa na maamuzi, nilimuacha ndani kwa sababu anajua kufunga mabao na ni mwepesi sana," aliongeza.

"Senegal walikuwa na nafasi tatu, lakini tuna kipa ambaye anajua mambo yake kati ya nguzo.

"Hatukucheza vizuri sana, mara nyingi sana tuliwapa mpira na nafasi ya kufunga."

# Asensio kukaa Madrid miaka 10

**MADRID, Hispania**

MARCO Asensio amesema kuwa anataka kubakia Real Madrid kwa "miaka 10 zaidi" huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania akiendelea na mazungumzo ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo.

Asensio, ambaye yuko na Hispania kwenye Kombe la Dunia, anatazamiwa kuwa mchezaji huru wakati mkataba wake wa sasa na Madrid utakapokamilika mwishoni mwa Juni, huku akiwa anahusishwa na kuondoka Santiago Bernabeu na Barcelona ikiripotiwa kuvutiwa naye.


Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, anatumaini kuwa anaweza kurefusha mkataba wake na washindi hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambao amewachezea mechi 250 tangu awasili kutoka Mallorca Desemba 2014.

Asensio ameongeza kwa kusema kuwa kuna mazungumzo kwamba anabadilisha mawazo yake na Real Madrid, lakini siku zote amejaribu kutoa kiwango cha juu alichonacho ndani, halafu itajulikana baadaye.

Lakini pia kinachomuumiza ni kwamba klabu hiyo haimtegemei yeye tu, hivyo baada ya Kombe la Dunia wote watafanya uamuzi. Anatamani kusalia Madrid kwa miaka mingi na kila kitu nitaweza kusalia miaka 10 zaidi alisema.

Asensio pia alitoa salamu zake kwa mchezaji mwenzake, Karim Benzema, ambaye aliondolewa kwenye Kombe la Dunia baada ya kupata jeraha kwenye paja lake la kushoto.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa amekuwa mshindi wa kwanza wa Ballon d'Or kukosa fainali hizo tangu Allan Simonsen raia wa Denmark kushindwa kufuzu kwa michuano hiyo ya mwaka 1978.



232,366/-

# SIMBA KUANZA NA MBEYA CITY KUSAKA 12 UGENINI LEO

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwasili salama juzi usiku jijini Mbeya, Kikosi cha Simba, kimesema kipo tayari kupambania pointi zote tatu dhidi ya wenyeji wao, Mbeya City kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa leo katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine.

Simba ambayo imeeleza kuwa inataka kuvuna pointi zote 12 katika safari ndefu ya mechi nne mfululizo za ugenini ikianza na mchezo wa leo, itashuka katika dimba hilo huku ikiwa na kumbukumbu ya msimu uliopita kuanza kwa kupoteza muelekeo wa kutwaa ubingwa kwa kukubali kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Mbeya City.

Hata hivyo, kitendo cha kupoteza pointi tatu msimu uliopita, kimekuwa funzo kwao kuelekea mchezo huo wa leo baada ya kusema wamechukua tahadhari zote kuhakikisha hawarudii makosa hayo zaidi ya kusaka pointi tatu.

Simba itashuka dimbani ikiendelea kuwakosa baadhi ya wachezaji wake, Nelson Okwa na Peter Banda ambao ni majeruhi huku Jimmyson Mwanuke na Israel Mwenda licha ya kupona majeraha yao hawatakuwapo katika mchezo huo kwa sababu ya kutokuwa fiti na wameachwa jijini Dar es Salaam wakiendelea na mazoezi maalum pamoja na Sadio Kanoute.

Lakini pia Simba wanashuka dimbani leo wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Ruvu Shooting wiki iliyoisha, shukrani kwa mshambuliaji wao mkongwe, John Bocco aliyerejea akitokea chumba cha majeruhi na kupiga hat-trick na Shomari Kapombe aliyeifungia bao la nne.

Akizungumzia mchezo huo, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, alisema maandalizi yamekwenda vizuri na wachezaji wako tayari kwa ajili ya kupambana kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo ambao ni muhimu kwa kila timu.

"Mechi itakuwa ya ushindani kwa sababu hatutakuwa tayari kurejea makosa ya msimu uliopita mbele wenyeji wetu hao, tulipoteza mechi hiyo na sasa hatukubali kupoteza tena, tunahitaji kupata pointi tatu katika mchezo huu," alisema Mgunda.

Alisema mechi itakuwa ya ushindani mkubwa ikizingatiwa walinzani waou watakuwa nyumbani na kutaka kufanya yale ya msimu uliopita, hivyo kuingia kwa tahadhari kubwa na kucheza kwa heshima na nidhamu kubwa katika mchezo huo wa leo.

"Mechi itakuwa yenye ushindani mkubwa, zile nafasi tunazotengeneza tunapaswa kuzitumia vizuri na hutakiwi kuingia uwanjani ukiwa na matokeo mfukoni mwetu.

"Tutacheza kwa nidhamu ya hali ya juu na umakini mkubwa kwa kuhakikisha tunaendelea kufanya vizuri na kutumia vizuri nafasi tunazotengeneza," alisema Mgunda.



## YANGA, MAYELE HAWASHIKIKI

INATOKA UK. 32

ka mbili baadaye, ila alikuwa mchoyo na hakuwa sehemu nzuri ya kufunga, lakini alilazimisha kupiga na mpira ukaambaa na kutoka nje.

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alilazimika kutoka dakika ya 37 baada ya kupata maumivu yeye mwenyewe bila kuguswa na mtu, nafasi yake ikachukuliwa na Ibrahim Abdullah 'Baka', kitambaa cha unahodha akakabidhiwa Feisal Sulum 'Fei Toto', ambaye naye aliumia kipindi cha pili na nafasi yake ikachukuliwa na Gael Bigirimana, kitambaa kikihamia kwa Mayele.

Dakika nne kabla ya mapumziko, Yanga ilipata bao jepesi lililofungwa na Mayele, baada ya krosi iliyopita kwa Kisinda, ikimkuta mfungaji akiwa peke yake hajakabwa na mtu, akapiga shuti dhaifu lililotinga wavuni na kuwaacha mabeki wa Dodoma Jiji waliojazana golini na kipa wao wakijaribu kuokoa bila mafanikio.

Mayele alifunga bao lapili lililofanana na la kwanza dakika ya 67 kutokana na uzembe wa mabeki wa Dodoma Jiji wakiongozwa na Gerald Mgeveke, wakiwa watatu, walishindwa kumkaba akiwa anatazamana na kipa, akipata pasi fupi kutoka kwa Denis Mkane akaupachika wavuni.

Angeweza kufunga 'hat-trick' dakika ya 81 kama si kupiga mpira nje akiwa anatazamana na kipa Mgore, akiwazidi mbio mabeki, lakini ikatoka sentimeta chache. Dakika nne baadaye alitolewa na nafasi yake ikachukuliwa na Clement Mzize.

Kwa matokeo hayo, Yanga imefikisha jumla ya pointi 29, ikicheza mechi 11, huku Dodoma Jiji ikisalia kwenye nafasi ya 15 kwa pointi zake tisa.

## Saudi Arabia yawafunza soka

INATOKA UK. 32

kwa kile kinachoonekana huo ni ushiriki wake wa mwisho kwenye Kombe la Dunia.

Argentina itashuka tena uwanjani Jumamosi dhidi ya Mexico wakati Saudi Arabia yenyewe ikivaana na Poland siku hiyo.

Katika mchezo mwingine wa Kundi D, Denmark ilishindwa kufurukuta mbele ya Tunisia baada ya timu hizo kugawana pointi ikiwa ni mechi ya kwanza katika michuano hiyo mwaka huu kumalizika bila bao.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/11/22 | 18:00 | Walsall FC vs Carlisle United | 2.28 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/11/22 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Chesterfield FC | 2.44 | 3.35 | 2.75 |
| 03. 26/11/22 | 18:00 | Shrewsbury Town vs Peterborough United | 3.10 | 3.25 | 2.27 |
| 04. 26/11/22 | 18:00 | Hartlepool United vs Harrogate Town | 2.75 | 3.30 | 2.47 |
| 05. 26/11/22 | 20:00 | Dagenham and Redbridge FC vs Gillingham FC | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 06. 26/11/22 | 20:00 | SC Pisa vs Ternana Calcio | 2.21 | 3.30 | 3.20 |
| 07. 26/11/22 | 20:30 | Albacete Balompie vs Racing Santander | 2.27 | 3.05 | 3.30 |
| 08. 27/11/22 | 13:30 | Ankara Keciorengucu vs Samsunspor | 2.48 | 3.35 | 2.75 |
| 09. 27/11/22 | 13:30 | Pendikspor vs Eyupspor | 2.40 | 3.35 | 2.80 |
| 10. 27/11/22 | 16:00 | Burgos CF vs Real Zaragoza | 2.48 | 2.90 | 3.10 |
| 11. 27/11/22 | 16:00 | Erzurumspor FK vs Bandirmaspor | 2.34 | 3.35 | 2.90 |
| 12. 27/11/22 | 17:00 | Como 1907 vs SSC Bari | 2.85 | 3.20 | 2.46 |
| 13. 27/11/22 | 17:00 | FC Sudtirol Bolzano vs Ascoli Calcio 1898 | 2.40 | 3.15 | 3.00 |
| 14. 27/11/22 | 18:00 | CD Leganes vs Granada CF | 2.55 | 3.00 | 2.90 |
| 15. 27/11/22 | 20:00 | Palermo FC vs Venezia FC | 2.35 | 3.25 | 2.95 |
| 16 27/11/22 | 20:00 | FC Cartagena vs SD Eibar | 2.38 | 3.10 | 3.05 |
| 17. 27/11/22 | 22:00 | Spain vs Germany | 2.50 | 3.25 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO- 23/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3427 | Morocco vs Croatia | 3.74 | 3.14 | 2.06 |
| 14:00 | 1272 | Edirnespor vs Derincespor | 4.17 | 3.44 | 1.76 |
| 14:00 | 1429 | Sile Yildizspor vs Elazigspor | 2.20 | 3.12 | 3.07 |
| 14:00 | 1780 | Singida BS FC vs KMC | 2.06 | 2.88 | 3.75 |
| 14:00 | 2007 | Erbaaspor vs Adliyespor | 5.25 | 3.64 | 1.57 |
| 14:00 | 2664 | Karsiyaka vs Catalcaspor | 2.07 | 3.25 | 3.55 |
| 14:00 | 3057 | Gazovik Orenburg vs Rostov | 2.04 | 3.49 | 3.10 |
| 14:00 | 3216 | Efeler 09 Sfk vs Bergama Bld | 2.42 | 2.87 | 2.96 |
| 14:00 | 3555 | SC Dnipro 1 vs Oleksandria | 1.82 | 3.51 | 3.75 |
| 14:00 | 4142 | Ofspor vs Gumushanespor | 3.25 | 3.00 | 2.33 |
| 14:00 | 4433 | Gaddafi FC vs Dove All Stars | 2.78 | 2.83 | 2.59 |
| 14:00 | 5801 | Minerva FC vs Rajasthan United | 1.82 | 3.35 | 3.98 |
| 14:00 | 5814 | Yomraspor vs Amasyaspor | 2.48 | 2.87 | 2.87 |
| 14:00 | 5886 | Turgutluspor vs Ayvalikgucu | 2.87 | 2.97 | 2.41 |
| 15:00 | 1451 | Shakhtar Donetsk vs Vorskla Poltava | 1.30 | 4.88 | 8.00 |
| 16:00 | 1023 | Sportive Zarzis vs EGS Gafsa | 3.22 | 2.73 | 2.36 |
| 16:00 | 1123 | Stade Gabesien vs Kalaa Sport | 2.01 | 2.71 | 4.26 |
| 16:00 | 3351 | Germany vs Japan | 1.50 | 4.24 | 6.03 |
| 16:00 | 3520 | Akhmat Grozny vs Dinamo Moscow | 2.67 | 3.50 | 2.27 |
| 16:00 | 3829 | AS Oued Ellil vs AS Mhamdia | 1.86 | 2.87 | 4.67 |
| 16:00 | 3874 | Mbeya City vs Simba | 5.26 | 3.12 | 1.70 |
| 16:00 | 4042 | Ethiopian Medhin vs Dire Dawa Kenema FC | 2.10 | 3.25 | 3.50 |
| 16:00 | 5207 | AS Djerba vs SC Moknine | 2.00 | 3.00 | 4.20 |
| 16:00 | 5797 | Onduparaka FC vs Wakiso Giants FC | 4.86 | 3.55 | 1.63 |
| 16:00 | 5976 | PAO Rouf vs Proodeftiki FC | 4.66 | 3.49 | 1.67 |
| 16:30 | 1016 | Mohammedan SC vs Neroca FC | 1.50 | 4.10 | 5.27 |
| 18:00 | 1100 | Pyramids vs National Bank | 1.46 | 4.07 | 6.95 |
| 18:00 | 1106 | Kryliya Sovetov vs Spartak Moscow | 3.31 | 3.55 | 1.94 |
| 18:00 | 1306 | Farco FC vs Ismaily SC | 3.12 | 2.73 | 2.58 |
| 18:00 | 1890 | Hlucin vs Slovacko B | 1.74 | 3.99 | 3.65 |
| 18:00 | 5799 | Coca Cola vs Aswan | 1.25 | 4.98 | 12.95 |
| 18:30 | 1097 | Al Ahli Manama vs Al Hidd Club | 2.50 | 2.79 | 2.94 |
| 19:00 | 1237 | Ethiopia Electricity vs Ethiopia Bunna SC | 2.12 | 3.20 | 3.15 |
| 19:00 | 1536 | Spain vs Costa Rica | 1.14 | 7.02 | 19.05 |
| 19:00 | 3066 | APR FC vs Kiyovu Sports | 2.07 | 2.86 | 3.74 |
| 20:00 | 2049 | Banga Gargzdai vs Futbolo Akademija Siauliai | 3.70 | 3.31 | 1.90 |
| 20:00 | 2253 | FC Krasnodar vs Lokomotiv Moscow | 2.10 | 3.31 | 3.11 |
| 20:00 | 3397 | FK Panevezys vs Lietava Jonava | 1.03 | 10.68 | 29.12 |
| 20:00 | 4542 | FC Hegelmann Litauen Kaunas vs Vilniaus Riteriai | 2.00 | 3.26 | 3.40 |
| 20:00 | 4553 | Zalgiris vs Zalgiris Kaunas | 1.81 | 3.20 | 4.27 |
| 20:00 | 5127 | Suduva vs Dziugas | 1.63 | 3.60 | 4.76 |
| 20:00 | 5833 | FC Schalke 04 II vs Preussen Munster | 3.16 | 3.55 | 1.99 |
| 20:30 | 2113 | Esbjerg vs Thisted FC | 1.42 | 4.55 | 5.62 |
| 22:00 | 4715 | Belgium vs Canada | 1.50 | 4.21 | 6.01 |
| 22:30 | 3135 | Port Vale vs Barnsley | 2.52 | 3.25 | 2.52 |
| 22:30 | 3374 | Swindon Supermarine vs Gosport Borough | 1.72 | 4.08 | 3.65 |
| 22:30 | 4588 | Colchester vs Bristol Rovers | 2.82 | 3.55 | 2.15 |
| 23:00 | 1518 | Chelsea W vs Real Madrid W | 1.58 | 3.83 | 4.85 |
| 23:00 | 4044 | AS Roma W vs Wolfsburg W | 5.06 | 4.18 | 1.51 |
| 23:45 | 3850 | Leixoes vs Santa Clara | 2.86 | 3.10 | 2.34 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Novemba 23, 2022

Nipashe



UKURASA 29

**Southgate aanika hali ya Maguire Kombe la Dunia**

**CHINI YA ULINZI...**


Mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, akiwekwa mtu kati na mabeki wa Timu ya Taifa ya Saudi Arabia kwenye mechi ya Kundi C ya Kombe la Dunia iliyopigwa Uwanja wa Lusail Iconic, Qatar jana na Argentina kuchezea kichapo cha mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA, MAYELE HAWASHIKIKI

**●●●Ni mwendo wa kutupia na kurudi yeye na timu yake kileleni mwa wafungaji na msimamo...**

**Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Yanga, Fiston Mayele, amekaa kileleni mwa orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu baada ya jana kupachika mabao mawili, akiiwezesha Yanga kuiadhibu Dodoma Jiji FC 2-0 na kurejea katika uongozi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.

Katika mchezo huo uliochezwa Uwanja wa Liti mkoani Singida, Mayele, ambaye kwenye mechi iliyopita, Alhamisi dhidi ya Singida Big Stars, alifunga mabao matatu 'hat-trick', ameweka rekodi ya kufunga mabao matano kwenye mechi mbili mfululizo akifikisha jumla ya mabao nane, akimzidi kwa bao moja aliyekuwa kinara kabla ya mechi ya jana, Sixtus Sabilo wa Mbeya City.

Hata hivyo, Sabilo anaweza 'kupindua meza' kama atafunga leo kwenye mechi ambayo timu yake inacheza dhidi ya Simba, Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Ni ushindi uliowafanya Yanga kukaa kileleni huku ikifikisha mechi 48 bila kupoteza ikizidi kuendeleza rekodi inayoiweka yenyewe, baada ya kupoteza mara ya mwisho dhidi ya Azam FC mabao 1-0, Aprili 26, mwaka jana kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita.

Dodoma Jiji itabidi ijilaumu yenyewe kwa kushindwa kupata angalau sare kwenye mechi hiyo, kwani walikosa mabao mengi ya wazi kuliko wageni wao, Yanga ambao hawakucheza vema hasa kwenye sehemu ya ulinzi ambako kulikuwa na makosa mengi ambayo hayakutumiwa na wapinzani wao kuwaadhibu.

Straika Paul Peter aliikosesha mabao mawili ya wazi ambayo kama angekuwa makini mechi hiyo ingeweza kuwa sare, lakini Christian Zigah na Hassan Mwaterema nao wakikosa.

Mechi ilianza bila utulivu kwa pande zote mbili ambapo zilionekana kuwa na papara, huku wachezaji wake wakipiga mipira juu, na pasi fupi fupi hazikuwa nyingi.

Yanga ilipeleka shambulio la hatari zaidi kwenye lango la Dodoma Jiji dakika ya 23 wakati Tuisila Kisinda alipowatambuka mchezaji mmoja baada ya mwingine na kujikuta ana kwa ana na kipa Daniel Mgore, lakini shuti lake liliishia mikononi.

Mayele angeweza kumpasia Kisinda daki-

INAENDELEA UK. 31

## Saudi Arabia yawafunza soka Messi, Argentina

**Lusail, Qatar**

UJASIRI na vipaji ndani ya Timu ya Taifa ya Saudi Arabia, umezua mshtuko kwa moja ya timu kubwa katika historia ya Kombe la Dunia baada ya kutokea nyuma na kuwafundisha soka kwa kuwachapa mabao 2-1 mabingwa mara mbili wa michuano hiyo, Argentina kwenye mechi ya ufunguzi ya Kundi C ya michuano hiyo iliyopigwa katika Uwanja wa Lusail Iconic, Qatar jana huku wawakilishi wa Afrika, Tunisia wakitoka suluhu dhidi ya Denmark.

Ikiwa katika nafasi ya 51 ya viwango vya soka duniani, Saudi Arabia chini ya Kocha Mfaransa, Herve Renard, ingeweza kumalizwa na kutimuliwa vumbi katika kipindi cha kwanza baada ya Lionel Messi kufunga bao la kuongoza kwa mkwaju wa penalti kabla ya Argentina kufunga mengine matatu na kukataliwa kwa madai ya kuotea.

Lakini 'Green Falcons' hao waligeuza mchezo huo kichwani mwao dakika 10 baada ya mapumziko, Saleh Al-Shehri akisawazisha kabla ya Salem Al Dawsari kuzua taharuki uwanjani hapo kwa kutupia bao la pili.

Wakiwa wameonyesha kucheza kwa jihadi, wakiinyima nafasi safu ya ushambuliaji ya Argentina, Saudi Arabia imeweza kupata ushindi wao wa nne pekee wa Kombe la Dunia katika historia yake na kuweka kundi hilo kuwa wazi kwa yeyote kuweza kusonga mbele.

Kocha wa Argentina, Lionel Scaloni, amekiongoza kikosi chake kutinga kwenye michuano hiyo kikiwa miongoni mwa timu zinazopewa nafasi ya kutwaa ubingwa kutokana na kucheza mechi 36 bila kupoteza ikiwamo zile za Copa America 2021 walipotwaa taji hilo, lakini rekodi hiyo ilivunjwa jana.

Sasa Scaloni na Argentina yake wana kazi ya kufanya ili kuweka hai matumaini yao ya kutwaa ubingwa huo wa kwanza tangu 1986 na kumpa Messi kwaheri njema

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >